ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID	-	SPIKA
1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais

9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13.Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais

19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
22. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
23. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
24. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
25. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
26. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
27. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
28. Mhe.Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
29. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe

30. Mhe. Ali Salum Haji - Jimbo la Kwahani
31. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) - Jimbo la Kijitoupele
32. Mhe. Ame Haji Ali - Jimbo la Nungwi
33. Mhe. Amina Iddi Mabrouk - Nafasi za Wanawake
34. Mhe. Asha Abdalla Mussa - Jimbo la Kiwengwa
35. Mhe. Bahati Khamis Kombo - Jimbo la Chambani
36. Mhe. Bihindi Hamad Khamis - Nafasi za Wanawake
37. Mhe. Hamad Abdalla Rashid - Jimbo la Wawi
38. Mhe. Hamida Abdalla Issa - Nafasi za Wanawake
39. Mhe. Hamza Hassan Juma - Jimbo la Shaurimoyo
40. Mhe. Hassan Khamis Hafidh - Jimbo la Welezo
41. Mhe. Hidaya Ali Makame - Nafasi za Wanawake
42. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa) - Jimbo la Mtoni
43. Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Jimbo la Paje
44. Mhe. Khadija Omar Kibano - Jimbo la Mtambwe
45. Mhe. Machano Othman Said - Jimbo la Mfenesini
46. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti - Jimbo la Mtopepo
47. Mhe. Makame Said Juma - Jimbo la Kojani
48. Mhe. Maryam Thani Juma - Jimbo la Gando
49 Mhe. Masoud Abrahman Masoud - Jimbo la Bububu
50. Mhe. Mihayo Juma N'hunga - Jimbo la Mwera
51. Mhe. Miraji Khamis Mussa - Jimbo la Chumbuni
52. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha - Jimbo la Mtambile
53. Mhe. Mohamed Said Mohamed - Jimbo la Mpendae
54. Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohamedali- Jimbo la Uzini
55. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini
56. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake
57. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole
58. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani
59. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake
60. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake
61. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani
62. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani
63. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni
64. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde
65. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake

66. Mhe. Rashid Makame Shamsi - Jimbo la Magomeni
67. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Nafasi za Wanawake
68. Mhe. Said Omar Said - Jimbo la Wingwi
69. Mhe. Said Hassan Said - Mwanasheria Mkuu
70. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma - Nafasi za Wanawake
71. Mhe. Salma Mussa Bilal - Nafasi za Wanawake
72. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman - Nafasi za Wanawake
73. Mhe. Shaib Said Ali - Jimbo la Chonga
74. Mhe. Shamata Shaame Khamis - Jimbo la Micheweni
75. Mhe. Simai Mohammed Said - Jimbo la Tunguu
76. Mhe. Suleiman Makame Ali - Jimbo la Ziwani
77. Mhe. Suleiman Sarahan Said - Jimbo la Chakechake
78. Mhe. Tatu Mohamed Ussi - Nafasi za Wanawake
79. Mhe. Ussi Yahya Haji - Jimbo la Mkwajuni
80. Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Nafasi za Wanawake
81. Mhe. Wanu Hafidh Ameir - Nafasi za Wanawake
82. Mhe. Yussuf Hassan Iddi - Jimbo la Fuoni
83. Mhe. Zaina Abdalla Salum - Nafasi za Wanawake
84. Mhe. Zulfa Mmaka Omar - Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem - Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Ishirini na Nane – Tarehe 27 Juni, 2016

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Naibu Spika (Mgeni Hassan Juma) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha hati mezani ya Mswada wa Sheria ya Kuidhinisha Makisio na Matumizi ya Shilingi Bilioni Mia Nane na Arobaini na Moja, Mia Nne na Sabini na Saba Milioni na Laki Tano kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina na Serikali kwa Mwaka wa Fedha unaoishia siku ya tarehe 30 Juni, 2017 na kuruhusu Utoaji na Uhaulishaji wa Fedha hizo pamoja na Mambo Yanayohusiana na Hayo. Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, nashukuru kwa kupata fursa hii, namshukuru Mwenyezi Mungu sote tukiwa na afya njema na wazima. Nanaomba kuwasilisha mezani Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Hospitali ya Mnazi Mmoja na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo. Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Tatu Mohamed Ussi (Kny: Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii): Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kuwasilisha mezani maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kuhusu Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Hospitali ya Mnazi Mmoja na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo. Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

UTARATIBU

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kunipa nafasi hii nikapata utaratibu tumeona Mhe. Waziri pamoja na Mwenyekiti wa Kamati wamewasilisha hati mezani. Sasa naomba kidogo nirekebishwe inawezekana pengine huu mswada uliposambazwa inawezekana mimi wangu pengine sikuupata. Kwa hiyo, sijajua kama wajumbe wengine wameshasambaziwa huu mswada au vipi, kidogo tu nilikuwa nataka utaratibu. Ahsante mheshimiwa.

Mhe. Naibu Spika: Hata na mimi sijauona huo mswada vile vile, Mhe. Waziri labda utupe ufafanuzi kidogo.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kweli nafikiri labda mawasiliano yangefanyika na meza yako ya Katibu, mswada huo sisi tumewasilisha wiki moja kabla katika Ofisi ya Baraza na tayari ulishapangiwa kwa wajumbe wote na nilihakikisha *process* hiyo mimi mwenyewe, kwamba kila mjumbe amepangiwa wake. Kwa upande wa kamati tuliwapatia mapema zaidi.

Mhe. Naibu Spika: Sawa nimeuona hata hapa ninao mbele yangu na nadhani kwamba sijui Waheshimiwa Wajumbe wote hawajapata, lakini natarajia kwamba tunaweza kupata sasa hivi. Kwa hiyo, niwaombe mvute subra kidogo Waheshimiwa Wajumbe wacha tuendelee kwanza na majadiliano ya Wizara ya Fedha halafu baadae hivi sasa utakuja mimi nitamuomba Katibu ili uweze kufika kwenu kwa haraka sana.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Naibu Spika, nadhani huu mswada ni muhimu sana kwetu sisi kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, na utaratibu wa Kanuni zetu za Baraza kawaida miswada huwa inatakiwa tuipate siku 21 kabla ya kuwasilishwa Barazani. Kwa kuwa mswada huu umekuja kwa hati ya dharura au basi tungeliupata hiyo wiki moja ambayo aliyosoma Mhe. Waziri, na kwa sababu Mhe. Naibu Spika ili tunapopata miswada utaratibu tunatakiwa tukae na wadau mbali mbali ili tuweze kupata mawazo yao. Mimi si daktari, mimi si mtaalamu wa afya leo nakuja kupitisha mswada huu muhimu kama hivi ni upate leo, niujadili leo au kesho. Kwa kweli Mhe. Naibu Spika, huu mswada tutakuwa tunaupitisha bila ya kujua tunapitisha kitu gani.

Sasa labda niombe muongozo wako Mhe. Naibu Spika, kwa sababu sasa hivi hata mfano huo mswada tukipewa hatuwezi tuka-*concentrate* katika mswada wakati tuna kitu muhimu kiko mezani kweli. Kwa hiyo, hili kwa kweli labda Mhe. Naibu Spika tupate utaratibu mwengine na sijui siku zetu ziko vipi angalau lazima tupate siku tuupitie, tuulize masuala kwa wadau wa afya, kwa wadau wengine ili tupate kushauri. Kuna sheria tuna wenzetu wa hospitali ya Muhimbili tayari ile ni hospitali ya rufaa tunataka tuangalie sheria za wenzetu zinasemaje yale masharti, kwa sababu tunataka tusije tukapitisha kitu halafu baadae tukaja hapa tukaja kuanza kulaumiana. Nilikuwa naomba muongozo wako mheshimiwa.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Hamza nimefahamu sana *concern* yako na *concern* yako iko *valid* kabisa nimefahamu sana, lakini kwa utaratibu huo ambao

unaouelezea hauko katika mswada wa dharura, utaratibu huo wanasema kwamba tuangalie na hospitali nyengine. Sasa mimi naomba utupe muda tuendelee na hii ya sasa Wizara ya Fedha halafu baadae nitaipeleka kwa serikali tuone vipi namna gani tunaweza kulifanyia kazi hilo ambalo unalolizungumza. Nakushukuru sana.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana na namshukuru Mhe. Hamza kwa hoja yake ambayo ameitoa. Kama ambavyo Mhe. Waziri wa Afya amesema mswada huu uliletwa katika Ofisi ya Baraza wiki moja iliyopita na umeletwa kwa hati ya dharura chini ya kifungu cha 80 ili mswada huu usipite kwenye Kanuni ya 79 ambayo inataka mswada huu ukidhi matakwa ya kusoma kwa mara ya kwanza, mara ya pili na mara ya tatu. Sasa kama kuna *miscommunication* ni baina sasa ya Ofisi ya Katibu na Wajumbe wa Baraza.

Mimi sioni tabu kama Waheshimiwa Wajumbe watapewa siku moja kupitia huu mswada, lakini kwa sababu imeshaletwa kwa hati ya dharura na Mhe. Rais ameshatia saini hiyo hati ya dharura ni wajibu wetu kuupitisha na kuusoma mswada huu kwenye kipindi hiki cha Baraza.

Sasa kama kuna hoja ya Wajumbe kupewa siku moja ya ziada mimi nadhani hilo ni baina ya ofisi yako Mhe. Naibu Spika ya kutafuta utaratibu, lakini kwa sababu matakwa yote ya kikanuni yametimizwa kwa ajili ya kuletwa mswada ule, mimi nadhani yaliyobaki ni *accommodation* baina ya hoja ambazo ametoa Mhe. Hamza na ambazo ni hoja za wajumbe wengi nadhani kama angalau wapate muda wautizame. Lakini muda wenyewe hatuna kwa sababu tunatarajiwa kumaliza Baraza kesho kutwa na ndio maana unaona ratiba nyingi hizi sasa zimekuwa zote zimewekwa pamoja. Lakini kwa upande wa Kanuni mimi nadhani sisi kama serikali tumetimiza masharti yote ya kikanuni Mhe. Naibu Spika. Nakushukuru.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Mwanasheria Mkuu, mimi bado nasimamia lile ambalo nimelisema hapa kwamba naomba mnipe muda niweze kujadiliana na Ofisi ya Katibu pamoja na Mhe. Spika yupo hapa hapa tutajadiliana na tutapata *fatwa* ya hili. Lakini sasa tuendelee na wizara kwanza halafu baadae tutakuja na hilo. Nashukuru sana.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, wachangiaji waliobakia ni Mawaziri, Manaibu Waziri kwa hiyo nitaanza na Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri, atafuata Mhe. Mohammed Ahmada ambaye ni Naibu Waziri wa Mawasiliano na baade ni Said Soud Said Waziri Asiyekuwa na Wizara Maluum.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya awali katika shughuli za leo.

Mhe. Naibu Spika, na mimi nachukua fursa hii kutoa mchango juu ya hotuba ya Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, na ningependa kulizungumzia suala la elimu ya mlipa kodi.

Mhe. Naibu Spika, ni muhimu tukaelewa kwamba ili raia aweze kulipa kodi anahitaji kuwa na muamko wa kujitambua na kujielewa kwamba yeye anapaswa kulipa kodi, na ili aweze kupata mwamko huo Mhe. Naibu Spika mwananchi analazimika kuwa na muamko, kuwa na uzalendo, kuwa na hisia kwamba anahusika katika maendeleo ya jamii. Kwa hivyo, ni muhimu kwanza Mhe. Naibu Spika sisi wawakilishi lakini pia na serikali tukawatambua nani…

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, Mhe. Naibu Waziri anachangia lakini nasikia zogo hatutomsikia na majibu mengine hatutoyapata. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wajumbe naomba sana utulivu wenu.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, ni vyema tukawatambua nani wanahusika katika kulipa kodi, maana yake inawezekana kwamba kutokana na ufinyu wa elimu hii ya walipa kodi huenda kwamba baadhi yetu tukawa hatujitambui kama tunapaswa kulipa kodi. Kwa hiyo, ndio maana pengine tunapofanya huduma zetu mbali mbali kwa mfano katika shughuli za biashara hujui kwamba unapaswa kupewa risiti na hata pale muuzaji anapojua kama akupe risiti utamkatalia unamwambia hakuna haja. Kwa hivyo, hii ni dalili kwamba elimu hii ya mlipa kodi iko katika kiwango cha chini katika jamii zetu.

Kwa hivyo, pamoja na taasisi inayohusika kutoa elimu ya mlipa kodi, lakini sisi kama ni viongozi wawakilishi na sisi pia tunapaswa kuisaidia taasisi hii

kuwaelimisha wananchi, kuwakumbusha wananchi umuhimu wa kulipa kodi. Mhe. Naibu Spika, kwa sababu hakuna nchi hata moja duniani inayoendeshwa bila ya kodi, kwa hivyo hata hawa wenzetu ambao wanatusaidia hizi nchi hisani basi fedha zao zinatokana na walipa kodi. Kwa hivyo, na sisi hatuna budi kutilia mkazo, ili kuona kwamba kila anayepaswa kulipa kodi katika nchi yetu basi analipa kodi.

Mhe. Naibu Spika, lakini muhimu hasa ni kuona kwamba huyu mwananchi analipa kodi kwa hiari, analipa kodi bila ya shuruti hili ni jambo muhimu sana. Lakini jambo hili haliwezi kupatikana moja kwa moja linakwenda hatua kwa hatua chini ya usimamizi wa misingi bora ya kutoa elimu ya mlipa kodi.

Kwa hivyo, sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa upande mmoja na serikali kwa upande wa pili tunahitaji kuchukua hatua madhubuti za kubadilisha mienendo na fikra za wananchi wetu, ili waelewe kwamba kuna haja na umuhimu wa kulipa kodi.

Mhe. Naibu Spika, ingawa wanaelewa kwamba suala la ulipaji kodi, suala la elimu ya ulipaji kodi linakwenda sambamba na suala la malezi, na suala la malezi kwa kweli inapaswa watu wote ambao wanapaswa katika kuelewa wawe na kauli moja. Hii maana yake Mhe. Naibu Spika, kwamba sote tunasema kuwa wananchi walipe kodi basi asitokee mwengine akasema wasilipe, hapo kidogo mchakato huu wa malezi utakuwa umeathirika. Kwa hivyo, sote tunapaswa kuwa na msimamo mmoja na kauli moja kuwaelekeza watu wetu.

Mhe. Naibu Spika, lakini pia kunyamaza kimya katika suala hili la kulipa kodi pia nalo linadhorotesha. Kwa hivyo, kama sisi viongozi tunaelewa kwamba kuna haja ya kulipa kodi, halafu ikawa hatuwashawishi watu wetu basi pia na sisi tunachangia kwa watu wetu kutokulipa kodi.

Kwa hivyo, ushauri wangu ni kwamba tuwe mstari wa mbele katika suala hili, kwa sababu sisi tunaelewa kwamba hizi kodi ndizo ambazo zinafanya serikali kufanya shughuli zake za kiserikali, bila ya kodi serikali itashindwa kufanya shughuli zake na sisi ambao wawakilishi ambao tunaidai serikali itufanyie hili na hili kwa niaba ya wananchi wetu, kwa hivyo nguvu hizo zinapatikana kwa kodi. Kwa hivyo, sisi hatuna budi pia kusimamia kama watu wetu wanalipa kodi.

Mhe. Naibu Spika, lakini pia si sisi wawakilishi peke yetu tu ambao tunapaswa kutoa elimu hii, lakini pia na taasisi nyengine za dini, *NGO's* na nyengine zote

tunapaswa kufanya kazi hiyo ya kuwaelimisha watu kulipa kodi. Lakini katika kuelimisha watu kuna mabadiliko ya tabia za watu, kwa kuwa kuna mabadiliko ya tabia za watu basi mbinu na njia za kusomeshea watu lazima nazo zibadilike. Kwa hivyo, *TRA* na *ZRB* lazima wabuni mbinu na mikakati sahihi ya kutoa elimu kwa mlipa kodi, njia ya mazoea *confessional approach* kwa kweli nafasi yake ni ndogo. Sasa kama tunavyojua Mhe. Naibu Spika, ni kwamba wanasema baadhi ya vimelea vinavyosababisha maradhi vimebadilisha tabia zao basi na watu pia wamebadilisha tabia zao.

Kwa hivyo, lazima tubuni mbinu mpya ambayo itawafanya wananchi wetu walipe kodi bila ya shuruti. Hili ni wajibu wetu kulisimamia kwa nguvu zetu.

Nimalizie maelezo yangu kwa kuwasihi wawakilishi wenzangu tufanye kazi hiyo kwa upande mmoja ya kuwaelimisha watu, lakini pia na kwa upande wa pili wa serikali tuendelee kufanya kazi chini ya misingi ya mbinu mpya ya kuwaelimisha watu kulipa kodi. Tukifanya hivyo labda mwakani au miaka inayokuja bila shaka kutakuwa na ongezeko la makusanyo ya mapato katika nchi yetu. Kwa kumalizia naunga mkono hoja hii. Ahsante Mhe. Naibu Spika. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Naibu Spika, awali ya yote na mimi nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kutuamsha asubuhi hii tukiwa katika hali ya afya njema hadi kuweza kuwasili hapa leo kushirikiana na wenzetu katika kuliongoza gurudumu letu la maendeleo ya nchi yetu. Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako na mimi naomba nichangie hoja hii tuliyowasilishiwa tokea juzi na Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango ambapo wajumbe walitaka maelezo kuhusiana na baadhi ya changamoto ambazo kwa kiasi kikubwa tulijibu katika bajeti yetu iliyopita katika siku zilizopita na ikapita kwa baraka zote za Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Naibu Spika, katika masuala yaliyoulizwa kuhusiana na wizara yetu moja yapo ni kuhusu barabara ya Fuoni, kama nilivyosema mwanzo barabara ya Fuoni tulipewa sisi mwanzo *UUB* kuitengeneza, lakini baada ya kukaa tukaamua ile hatua ya awali tuwape Mkandarasi *MECCO* ambapo Mkandarasi huyu alimaliza ile hatua ya awali kwa ufanisi mkubwa.

Hivi sasa ipo katika hatua ya kuwekwa lami na kama walivyokuwa wajumbe wanatuhimiza siku zote basi taratibu za sheria zifuate hata katika mambo haya ya manunuzi, kwa hiyo ndio maana sisi tukaamua kutangaza tena *tender* upya

baada ya kuona ile barabara tusiwape *UUB* kwa sababu tutakuwa na mzigo mwengine wa kutengeneza barabara ya Jendele mpaka Unguja Ukuu.

Kwa hiyo, tumeona tufuate taratibu zinazohusika, ili baadaye kusiweko na malalamiko yoyote kutoka kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, ndio tukafunguwa *tender* tarehe 15 Juni mwezi huu.

Mhe. Naibu Spika, naomba sana Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waelewe kwamba sisi nia yetu ni kuhakikisha kwamba barabara ile inamalizika kuwekewa lami kabla ya muda tuliowekewa wa mwezi wa Disemba. Nina imani kubwa sana Mkandarasi atakaepewa *tender* hiyo itakuwa tumempa kwa kuangalia zaidi uwezo wake na vile vile kumuangalia kazi alizozifanya hapo kabla. Nina imani Mkandarasi aliyekuwa bora na mwenye vigezo zote vya kimataifa, basi niwahakikishie wawakilishi kwamba ndiye tutakayempa *tender* ya kuijenga barabara ile kwa lami, ili iweze kumalizika kwa haraka na wananchi wetu tuwaondolee shida waliyokuwa nayo pale ya vumbi.

Mhe. Naibu Spika, wajumbe vile vile walihoji kuhusu mapato ya bandari, kama ninavyopenda kuwaelezea kwamba serikali sisi tuko makini sana kuhakikisha kwamba mapato si ya bandari tu bali ya sehemu zote katika nchi yetu basi yanadhibitiwa na yanaingia kwa njia zinazotakiwa za kiserikali.

Mhe. Naibu Spika, napenda wawakilishi waangalie kitabu hiki cha Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango ukurasa wa 28 anaelezea namna gani ya kuimarisha mfumo wa ukusanyaji wa kodi za serikali ambapo kifungu nambari nne anaeleza wazi kwamba, katika kuhakikisha kwamba mapato ya serikali yanakuwa hayavuji na yanaongezeka amesema kwamba ataimarisha mfumo wa ukusanyaji wa kodi za serikali kwa kuweka mfumo wa kodi wa kielektroniki ambao kitaalamu unaitwa e-*tax* kuimarisha matumizi ya mfumo wa udhibiti wa malipo EFMS na kuanzisha rasmi matumizi ya mashine za kielektroniki za utoaji wa risiti.

Mhe. Naibu Spika, hivi ni vipaumbele vya Wizaraya Fedha na Mipango na nina imani kubwa sana iwapo bajeti hii itapita basi, kwa vile waziri wetu ni mkereketwa mzuri wa maendeleo ya nchi yetu atafanikisha hili kwa hali ya juu kabisa. Naomba sana Waheshimiwa Wawakilishi wenzangu wamuachie Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango tupitishe bajeti hii ya serikali kwa ajili ya mambo mazuri ambayo yatakuwepo hapo baadaye.

Mhe. Naibu Spika, vile vile lilizungumziwa suala la Bodi ya Wakandarasi katika Wizara yetu ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, suala hili liliulizwa

na Mwenyekiti wa *PAC*. Napenda kumuarifu Mhe.Miraji kwamba kweli hili suala sisi wenyewe tumeliona ni tatizo na atupe muda basi tutalifuatilia kwa umakini na kuhakikisha kwamba, kama kuna aina yoyote ya uzembe imefanyika basi hatua zitachukuliwa kwa wale wote waliofanya uzembe huo.

Mhe. Naibu Spika, la mwisho kabisa ningependa kuzungumzia barabara hii ya Jendele mpaka Unguja Ukuu. Aliuliza Mhe. Miraji, je pale kuna tatizo lolote? Kusema kweli kulikuwa kuna tatizo pamoja na Mkandarasi ambaye alikuwa ni SHAPRIYA na Mkandarasi huyo baada ya kufikia hatua tuliamua kukubaliana naye katika kuhakikisha kwamba, zile pesa ambazo sisi za awali kuhusu asilimia 40 ambazo zinakuwa zinawekwa kwa ajili ya mkataba kama Mkandarasi hatotimiza yale masharti. Pesa hizo ni kama Tanzania shilingi bilioni moja nukta nne, ambazo hizo ndio ambazo tunahakikisha kwamba hizi pesa tunazipata. Kwa hiyo ninamwambia Mhe. Miraji kwamba tutahakikisha kwamba baada ya kukaa na Mhe. Mwanasheria Mkuu zile pesa tunazipata, ili tuendelee na kazi yetu kama kawaida. Namuhakikishia kwamba ile barabara wakati wowote tutaianza ujenzi wake ambao utakuwa chini ya Mkandarasi wetu wa UUB.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache, mimi naomba sana Waheshimiwa Wawakilishi wenzangu tuipitishe bajeti hii kwa mustakabali wa nchi na maslahi yetu na maendeleo yetu, hakika tunakubaliana kwamba kulikuwa na changamoto na kama nilivyosema mwanzo changamoto hizo tumekabiliana nazo, kulikuwa na matatizo na matatizo tumeyatatua. Kwa hiyo watuamini na tunahakikisha kwamba yale yote tuliyoyaahidi katika vikao vyetu hivi vya bajeti, basi tutaifanyia kazi na ule ushauri wao waliotupa tutaufanyia kazi.

Mhe. Naibu Spika, mwisho kabisa nawaomba sana Waheshimiwa Wawakilishi kama nitakavyokuwa mimi naunga hoja mkono kwa asilimia mia, basi na wao waunge mkono hoja hii, ili tupate kufanya kazi ili ilani yetu ya uchaguzi ya CCM ya 2015-2020 itekelezwe kwa ufanisi mkubwa na nina imani kubwa kwamba itawezekana kwa serikali hii makini.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Naibu Waziri. Sasa tumpishe Mhe. Said Soud Said na baada ya Mhe. Said Soud Said atachangia Mhe. Salama Aboud na ajitayarishe vile vile Mhe. Rashid Ali Juma.

Mhe. Said Soud Said: (Mhe. Waziri asiye na Wizara Maalumu): Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipatia nafasi hii asubuhi hii ya leo. Kwanza kabisa nachukuwa nafasi hii kuunga mkono hoja mia kwa mia. Vile vile nachukuwa

nafasi ya kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar kwa kumteua bwana Khalid kuwa Waziri wa Fedha katika visiwa hivi vya Unguja na Pemba, kwa kuongoza vizuri wizara katika awamu hii tunayoielekea.

Mhe. Naibu Spika, katika kipindi cha kampeni iliyopita niliwahi kusema kwamba kama kuna mema yaliyofanyika ndani ya serikali iliyopita yalifanywa na Chama cha Mapinduzi pamoja na Chama cha CUF. Kama kuna mabaya yalifanywa na watu hao hao wa Chama cha Wananchi CUF na Chama cha CCM. Sasa leo ni wajibu wetu kusema kwamba tunapiga mstari kwa yale yote yaliyopita awamu hiyo na tunaanza upya awamu ya miaka mitano ijayo. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, mimi nina imani kabisa wawakilishi wote tuwe tayari kuangalia kwamba serikali iliyopo madarakani hivi sasa ni serikali ya awamu mpya inayohitaji kuongozwa miaka mitano ijayo akiwa Waziri wa Fedha ni mpya ambaye anataka kupewa sasa majukumu, hajapewa majukumu, anataka sasa kupewa majukumu, sasa kukiwa kutakuwa na hoja zitakazoibuka za miaka mitano iliyopita kuhusu yeye, mimi nadhani tutakuwa hatufanyi *fair*, naomba hilo lifahamike. Kwa vile ni wajibu wetu sisi wawakilishi kukubali bajeti hii tukaipitisha, ili ikaweza kufanya kazi kwa miaka mitano ijayo na katika mazingira haya tukaangalia awamu kwa awamu 2016/2017 tukatizama sasa hapo kati kati pametokea nini, lakini hakuna haja ya kuleta mahoja yaliyopita huko nyuma wakati wale watu ambao wa kuhojiwa hawapo.

Mhe. Naibu Spika, Waziri wa Fedha hayupo ni mpya, waliokuwa wakisimamia serikali ya umoja wa kitaifa kundi lile jingine halipo, kuna kundi jipya, sasa leo mnakuja kuleta hoja ya kusema kwamba tutaunda kamati teule kwa madhumuni gani, yale madhumuni ya kuundwa kamati teule kwa madhumuni yepi? Maana serikali iliyopo ni mpya na wengi wetu sisi ni wapya, hatujui kilichotumika, hatujui kilichoharibika, sasa tunaunda kamati teule kwa mantiki ipi? Zaidi ya kumpa nguvu waziri aliyeteuliwa akatumia nafasi yake kuongoza wizara hii tukaja tukamhoji baadae kwa maendeleo yaliyopo, atayakosea au atayafanya.

Mhe. Naibu Spika, kwa mimi nataka niseme wawakilishi sisi ni kioo cha serikali, tunatakiwa tutunge sheria, tusimamie sheria, tuhoji sheria zile ambazo tumezipitisha, zile ambazo tumezifanya. Sasa ikiwa mimi, nashangaa sana nataka niseme nashangaa ikiwa mimi nyumba ni yangu na wapangaji waliomo ni wangu, lakini narudi sasa nakuja kuhoji kwa nini muliingia ndani kwa wakati fulani, kwa nini mulifanya hivi wakati fulani ni jambo la kushangaza sana kwa kweli. Nashangaa sana wanachama wa Chama cha Mapinduzi

waliondani ya Baraza hili na walio nje ya Baraza hili, wanajua kwamba serikali iliyoko madarakani ni ya Chama cha Mapinduzi, sasa leo kuhoji Chama cha Mapinduzi serikali yake wewe ukiwa mwanachama ni jambo la ajabu sana.

Mhe. Naibu Spika, naomba ifahamike kwamba...

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Hamza si utaratibu huo.

Mhe. Said Soud Said: (Mhe. Waziri asiye na Wizara Maalumu): Mhe. Naibu Spika, kuelewa kwamba serikali hii ni serikali inayoangaliwa na dunia na inayoangaliwa na wapinzani. Sisi tumeingia na mara baada ya kuingia kwenye serikali tumekabidhiwa ilani ya Chama cha Mapinduzi, kulinda na kutetea sera ya Chama cha Mapinduzi, sasa leo tutashangaa tukiona kwamba wao ambao wanaongoza serikali hii wanafika pahala wanataka kuhoji mambo yaliyopita na serikali iliyopita.

Mhe. Naibu Spika, mimi naomba ikiwezekana kuchukuwa nafasi Baraza lako likafanyiwa semina na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wakajielewa wao ni nani na wana wajibu gani ndani ya serikali hii, ili kufikisha zile adhma za wananchi juu ya kutumwa kwao humu ndani. Lazima waelewe, naomba munielewe sana wawakilishi wenzangu. Humu ndani muna vyama vinne, lakini chama chetu cha CCM ndio kinachoongoza serikali, sasa nyinyi mukiwa munapinga sera ya chama chenu, ilani ya chama chenu mnatuambia nini sisi, mnatufunza nini sisi, mnatuelekeza wapi sisi.

Mhe. Naibu Spika, unaposema unapinga unaunda kamati teule uchunguze serikali iliyopita ilikuwa ikiongozwa na nani na hii inaongozwa na nani. Serikali iliyopita ilikuwa inaongozwa na Dkt. Shein na serikali hii inaongozwa na Dkt. Shein, sasa ina maana wewe Dkt. Shein humuamini wakati ule unamkubali leo. Naomba tuelewe wajibu wetu kama wawakilishi. Sisi tunatakiwa tulete hoja za wananchi kwenye Baraza ili tuzifanyie kazi kuondoa changa moto zilizowakabili na tusilete hoja kwenye Baraza za kukwamisha serikali ikiwa katika safari yake ya kuwatafutia wananchi maendeleo.

Mhe. Naibu Spika, utaratibu mzima wa Baraza la Wawakilishi, ni utaratibu uliokubalika kisheria kwa wananchi wa Zanzibar kungojea kusimamiwa maendeleo yao na harakati zao za kiuchumi za kisiasa na za kijamii katika kulinda mustakabali wa taifa hili.

Mhe. Naibu Spika, ndugu wawakilishi, nakuombeni kwa pamoja tupitishe bajeti hii mia kwa mia ili kumpa Mhe. Khalid uwezo wakuendeleza yale yote

ambayo yaliwekwa kiporo na wenzetu waliopita, yale yote waliyoyaharibu wenzetu waliopita ili na sisi tuje tupate nafasi ya kuhoji baadaye kafanya lipi kaacha lipi.

Mhe. Naibu Spika, naunga mkono hoja.

Mhe. Naibu Spika: Nakushukuru Mheshimiwa. Mheshimiwa Salama, Mhe. Waziri wa Ardhi, karibu, baada ya hapo ajitayarishe Mhe.Rashid Ali Juma na baada ya Mhe. Rashid Ali Juma atafuata Mhe. Issa Gavu.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Naibu Spika, na mimi naomba nianze kwanza kwa kumshukuru *Allah Subhana Wataala* asubuhi kutuamsha tukiwa wazima, lakini kwa kunipa nafasi asubuhi hii. Lakini nianze tu kwa kumpongeza waziri mwenzangu kwa kazi kubwa aliyoifanya lakini na uwasilishaji wake mzuri lakini pia na kutupa matumaini makubwa sana. Naomba niunge mkono hoja mia juu ya mia na naomba pia niwaambie wenzangu kwamba hotuba hii aliyoitoa Mhe. Waziri wa Fedha ni hotuba yenye matumaini makubwa, kwa hiyo kwa pamoja tumuunge mkono, ili tumalize bajeti hii na tuweze kufanya kazi vizuri zaidi na zaidi.

Mhe. Naibu Spika, lakini vile vile naomba nichukuwe nafasi hii kujibu suala ambalo liliulizwa moja kwa moja kwa Mhe. Waziri wa Fedha lakini ninaona linanigusa zaidi ndani ya ofisi yangu, suali la ubadilishaji au uhaulishaji wa hoteli. Lakini naomba niseme kwamba ubadilishaji wa mahoteli au kampuni waliopewa mikataba yako ya aina mbili; aina ya kwanza ni kubadili jina bila ya kubadili umiliki; kwa hiyo hii mara nyingi inafanywa na wakala wa usajili na mali za biashara ambapo mapato yatokanayo na kubadili jina hukusanywa ofisi hiyo hiyo na hakuna athari katika makusanyo ya kodi ya ardhi.

Mhe. Naibu Spika, lakini pia katika hili naomba niseme tu jumla ya shilingi milioni tano laki nane zilikusanywa kwa mikataba saba ambayo iliweza kubadilishwa katika kipindi cha 2014/2016 na katika hili wenyeji huwa wanabadilishiwa kwa shilingi laki saba na kwa wageni shilingi milioni moja.

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba niitaje mikataba ambayo imebadilishwa katika kipindi hicho ambayo haikubadilishwa umiliki imebadilishwa tu jina. Kuna *Khajesta Butt* iko Bwejuu ambayo sasa hivi inaitwa *Khejesta Khesal* ambayo hii ilibadilishwa kwa mgeni kwa jumla ya shilingi milioni moja, kwa sababu unalipia tu ule ubadilishwaji wa mkataba, lakini Jambiani Karibu Bungalows sasa hivi inaitwa *Villa de Coco Company Limited* ambayo ni ya mwenyeji imebadilishwa kwa shilingi laki saba. Nungwi

Spice Villa ambayo sasa hivi inaitwa *Bagamoyo Spice Villa* nayo ni mwenyeji kwa shilingi laki saba, *Coral Beach Hotel* imebadilishwa na sasa hivi inaitwa *Coral Rock Hotel Limited* ni mwenyeji ni shilingi lakini saba, lakini kuna *Nungwi Company Limited* ambayo sasa hivi inaitwa *Nungwi Limited* ni ya mwenyeji imebadilishwa kwa shilingi laki saba.

Mhe. Naibu Spika, lakini vile vile kuna *African Queen Limited* sasa hivi inaitwa *Zanzibar Queen Hotel Limited* hii ni ya mgeni na imebadilishwa kwa shilingi milioni moja na *Mayur Muljibhai Madhvani* ambayo iko Bwejuu sasa hivi inaitwa *Marasa Beach Resort Hotel* nayo ya mgeni imebadilishwa kwa shilingi milioni moja, jumla zinakuwa milioni tano laki nane.

Mhe. Naibu Spika, lakini ubadilishaji wa pili ni ule wa kubadilisha umiliki wa moja kwa moja na hii hufanywa na Bodi ya Uhaulishaji Zanzibar ipo chini ya wizara yangu na makusanyo ya asilimia tatu hutozwa na bodi hiyo ya uhaulishaji ambayo labda nizitaje pia hapa kuna *Tamarind Beach Hote*l ni ya mwenyeji nayo sasa hivi inaitwa *Mayfair Gardens* imebadilishwa kwa shilingi laki saba, kwa sababu katika hili la uhaulishwaji zimekusanywa jumla ya shilingi milioni kumi laki tano na ninaomba nizitaje.

Mhe. Naibu Spika, kuna *Repisarda Sergio* ambayo sasa hivi iko Michamvi inaitwa *Case Del-mar* ambayo ni mgeni imebadilishwa kwa shilingi milioni moja. Kuna *Bwejuu Beach Resort* sasa hivi *inaitwaThe White Wave Resort* ambayo ni mwenyeji pia imebadilishwa kwa shilingi laki saba, Hassan Hamid Ahmed iko michanvi nayo sasa hivi inaitwa *Malo General Trader* ni ya mwenyeji kwa shilingi laki saba.

Kuna *Cleto Martinel* ambayo iko Pwani Mchangani na sasa hivi inaitwa *Lorela Martinel* imebadilishwa kwa shilingi millioni moja, Shumbana Amani Karume iko Kiwengwa sasa hivi hivi inaitwa *Zanzisun* imebadilishwa kwa shilingi milioni moja sasa hivi anayo mgeni, na *Sadrudin AnandjiGovindji* iko Kiwengwa sasa hivi pia inaitwa *Zanzisun* imebadilishwa kwa shilingi milioni moja halafu.

Kuna *Zanzibar Health and Leisure Resort* iko Pongwe sasa hivi inaitwa *Tulipt (T) Limited* ambayo anayo mgeni imebadilishwa kwa shilingi milioni moja.

Mhe. Naibu Spika, lakini vile vile kuna *Rechard Nightgale* iko Paje sasa hivi inaitwa *Lachezar Antanasov Todorv* imebadilishwa kwa milioni moja anayo mgeni, halafu kuna Amina Amani Karume iko Buyu sasa hivi inaitwa *Alma Company Limited* na imebadilishwa kwa shilingi laki saba, lakini kuna *Matlai*

Limited iko Chuini sasa hivi inaitwa *Mahsen Muhamed* imelipa kwa shilingi laki saba ya mwenyeji na *Javier Oliveras Castells* iko Matemwe sasa hivi inaitwa *Cristian Vaorel and Cristina Gontaru* imebadilishwa kwa milioni moja ya mgeni.

Mhe. Naibu Spika, kwa hiyo kwa kipindi chote hicho kwa hizi za uhaulishaji imekuwa ni milioni kumi laki tano kama nilivyosema mwanzo kwa ajili ya utengenezaji wa mikataba mipya. Kwa hivyo jumla tuna shilingi milioni kumi na sita laki tatu kwa ajili ya ubadilishaji mikata kwa mwaka 2014/2016.

Mhe. Naibu Spika, nilikuwa nimependa nilijibu hili, kwa sababu Waziri wa Fedha kaulizwa lakini lilikuwa liko moja kwa moja ndani ya Wizara yangu na iko chini ya taasisi zangu, kwa hiyo nimependa nilijibu hilo vyenginevyo naendelea kuunga mkono hoja na ninaomba Wajumbe wa Baraza lako tukufu hasa sisi wanawake tukiwa *beneficiaries* wakubwa ndani ya bajeti ile naomba tuiunge mkono hotuba ile kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

UTARATIBU

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardhi: Mhe. Naibu Spika, kuhusu utaratibu, nasimama na Kanuni ya 63(1), namuomba sana Mhe. Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum, Mhe. Said Soud Said aombe radhi Chama cha Mapinduzi. Kwa sababu Chama cha Mapinduzi hatufugi wezi wala majambazi na yeye atabakia kuwa mpinzani, sisi Chama cha Mapinduzi tuna kazi zetu na tutamtumbua yeyote yule akiwa CCM, *CHADEMA*, akiwa *CUF* madhali kafanya kosa tutalizungumza na tutamsema. Jambo alilolizungumza kuhusiana na kwamba Chama cha Mapinduzi tuteteane tusikandamize serikali kuzungumza ukweli tunaomba sana atuombe radhi wana CCM, hatuko hapa kutetea majambazi na wezi. Hiyo ndio kauli yangu mimi, ahsante sana.*(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Nadir Abdul-latif hivi kuna haja ya kuomba radhi kweli?

Mhe. Nadir Abdul-latof Yussuf Al-Wardi: Kwa chama haja ipo kwa sababu kakidhalilisha chama.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa mimi nataka kufanya *fair*, kwa sababu sote hapa wengi wetu ni wanachama wa Chama cha Mapinduzi, si ndio?

Wajumbe: Ndio.

Mhe. Naibu Spika: Sasa nataka nitoe hoja, wanaoona kwamba waombwe radhi na Mhe. Said Soud Said wanyooshe mikono. Wanaoona kwamba haina haja kuombwa radhi wanyooshe mikono, waliokuwa wanaona haina haja wameshinda. Tunaendelea. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana na mimi kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu *(S.W)* tukiwa ndani ya Kumi la Tatu la Mwezi wa Ramadhani ni kumi la kuachwa huru na moto. Kwa hivyo, namshukuru sana *Allah* kwamba ametuwezesha tukawa na afya njema na sisi tupo hii leo kuichangia hotuba hii ya Wizara ya Fedha na Mipango.

Mhe. Naibu Spika, sina budi kwanza nimshukuru sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa naomba utulivu, naomba sana utulivu wenu hatutoweza kupata majibu kama hatujatulia tukasikiliza Mhe. Waziri anajibu nini. Naomba sana utulivu wenu.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Mhe. Naibu Spika, naomba sana nimshukuru Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kwa hotuba yake hii na kwa muelekeo mzima wa bajeti ambao serikali yetu inatarajia kuutekeleza kwa mwaka huu wa fedha 2016/2017. Kama ilivyoelezwa mwanzo bajeti hii ni ya kwanza yenye mpango maalum unaoitwa *PBB*. Sasa mpango huu kwetu wengi ni mpya na ni mpango ambao tunatakiwa tuufahamu kwa makini kabisa. Kutokana na uwasilishaji wake naishukuru sana timu yake ambayo imekaa na imetupatia semina kwa muda usiopungua siku tatu au nne na natumaini semina ile wengi wetu tumenufaika na ndio maana hii leo tunatoa michango kadiri tunavyoweza.

Mhe. Naibu Spika, mimi nilikuwa nataka nichangie kwenye mambo mawili ambayo yaliulizwa ndani ya Wizara ya Fedha lakini yanagusa moja kwa moja Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo.

Mhe. Naibu Spika, suala la kwanza ninalotaka kulichangia ni suala zima la Uwanja wa Gombani ambao kwa namna moja au nyengine uliguswa na ulielekezwa kwa Wizara ya Fedha, kwa sababu wizaa hii ndio inayotoa fedha kwa ajili ya matumizi yote ya serikali. Nataka niwathibitishie Waheshimiwa

Wajumbe wa Baraza hili la Wawakilishi kwamba kama tulivyokiri wakati tunajibu maswali ya bajeti yetu. Uwanja wa Gombani haukumalizika kama ulivyokusudiwa kwa utengenezaji wa mwaka 2012 Disemba ambapo ulitarajiwa kumalizika Machi, 2013.

Mhe. Naibu Spika, uwanja ule haukumalizika kutokana na kukosa kutiwa *tartan* ya lami ipasavyo, ile *base* ambayo itakuja kutumika kwa kuweka *rubber* ilifika wakati ikawa na makoseo na makoseo yale nataka nithibitishe wazi baada ya ufuatiliaji wa kina Waheshimiwa Wajumbe waelewe kwamba kilichosababisha kuharibika kipande cha lami *Area D* kwenye goli na *area* ya *VIP* upande ambao wanakaa viongozi, ilikuwa ni unyeshaji ambao haukukubaliana na ile lami. Lakini nimeeleza wazi kwamba zaidi ya robo tatu ya uwanja ule ulitengenezwa kwa usahihi, sehemu zile zilizoharibika kweli zimeingiza hasara kwenye serikali na kazi kama nilivyoisema ilikuwa ni ya miezi mitatu tu.

Kutokana na matengenezo hayo Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo tayari imerekebisha marekebisho hayo na hasara kweli ilitokea, kwa sababu hasara iliyotokea pale ni vifaa vya lami vilivyokaa kwa muda mrefu, ambavyo vilitakiwa kufanyiwa kazi vikakosa kufanyiwa kazi ipasavyo. Lakini sehemu ambayo iliharibika ilikuwa ni robo na chini ya robo ya utengenezaji kwa utiaji wa lami (*base*).

Mhe. Naibu Spika, kwa hivi sasa tarehe ya leo tunazungumza uwanja ule tayari umesharekebishwa, ushafanyiwa kazi na sasa hivi wageni wa kutia lami vifaa ambavyo walipaswa kuja navyo kutokana na vile vilivyoharibika, vishafika na vimeshasafirishwa kuelekea Pemba na tunatarajia ndani ya mwezi mmoja au mmoja na nusu matarajio yetu *tartan* ya Uwanja wa Gombani itaanza kutumika ikiwa haina tatizo lolote lile. *(Makofi)*

Kwa hivyo, Waheshimiwa wasiwe na wasiwasi endapo tutabaini mfanyakazi, mhandisi, au msimamizi ameshiriki katika kuitia hasara serikali hatua tutazichukua wala hatutamvumilia mtu, wala serikali hii haina haja ya kumficha mtu ambaye anafanya kinyume na taratibu na sheria ziliopo.

Kwa muongozo huo wasiwe na wasiwasi kwa uwanja wa Gombani wapenzi wa kukimbia wajiweke tayari uwanja umekuwa hauna tatizo. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nasisitiza tena serikali hii haiko tayari kumvumilia mtu ambaye anafanya mambo kinyume na sheria na taratibu ziliopo za nchi. Sisi Wizara ya Habari tuko tayari kupokea vielelezo vyovyote ambavyo vitaonesha

kwamba hapa pameleta kasoro za kuifanyisha serikali ipate hasara; tutafuatilia, tutafanya taratibu ziliopo na tunapobaini uhakika hatua kali nawathibitishia Waheshimiwa kwamba zitachukuliwa na Baraza hili litajuzwa hatua gani zimeweza kuchukuliwa.

Sasa nizungumzie suala la ving'amuzi na utaratibu mzima wa urushaji wa matangazo ya *ZBC TV*, ambalo suala hili nalo limezungumzwa kwa kina. Limezungumzwa na Waheshimiwa wengi sana, limezungumzwa kwa hamasa, limezungumzwa mpaka mizizi ya shingo ilikuwa inatetemeka kwa aina yake.

Mhe. Naibu Spika, nataka niwathibitishie Wajumbe kama nilivyozungumza hapo awali niliwaomba sana kwamba tangu tuingie ndani ya serikali hii tulipopata uchaguzi wenye imani kabisa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Ali Mohammed Shein, tumefuatilia kwa kina suala la matangazo ya televisheni.

Suala hili linaonekana kwamba linahusiana na sehemu kubwa ya kushindwa kuhama kutoka *analogy* kuingia *digital* kazi ambayo kwa njia moja inazihusu sehemu tafauti zilizoweza kusababisha kushiriki na kuikamilisha kazi hii. Nataka niwathibitishie Waheshimiwa Wajumbe kwamba, Wizara ya Habari ni mmoja katika wadau, Wizara ya Fedha ni mmoja katika wadau, *ZMUX* ni mmoja katika wadau na *ZBC* kama Shirika ambalo tumelipitisha sisi hapa Barazani, kwa mujibu wa sheria naye ni mdau wa kuhakikisha kwamba *digital* inatumika ndani ya Zanzibar.

Kampuni ya *AGAPE* ni moja katika kampuni ambazo ziliingia mkataba na *ZMUX* kuhakikisha kwamba *digital* inafanyika. Mhe. Naibu Spika, niliwaomba sana Wajumbe wa Baraza lako tukufu hili ikiwezekana na niliwataka wakati ule kwa sababu suala hili linagusa wadau hao niliowataja Wizara ya Fedha, Wizara ya Habari pamoja na *ZBC* kama shirika ambalo liko chini ya Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo basi ilikuwa ni vyema watupe muda tufuatilie. Katika ufuatiliaji wetu nataka niwathibitishie Wajumbe kwamba, suala hili zima pale ambapo tunapingana hatukufikia maafikiano kwa mkataba ulioingiwa baina ya *AGAPE* na Wizara yetu ya Habari pamoja na Wizara ya Fedha suala hili tumelifikisha kwa mwanasheria. Mkataba upo kwa mwanasheria na mwanasheria anautizama kwa kina sisi tukiwa wafuatiliaji wa jambo lile.

Waheshimiwa Wajumbe waelewe kwamba serikali inamdai *AGAPE*, *AGAPE* anaidai serikali. Mvutano huu utawekwa sawa na mwanasheria, mwanasheria badala ya kutizama mikataba yetu atatumia vyombo vyake anavyohusika navyo

hapo yeye ataamua suala hili tulipeleke wapi, tuliwekee maamuzi gani. Waheshimiwa Wajumbe waelewe serikali kwa upande wake inaumwa sana, kwa nini suala la urushaji wa matangazo kupitia *digital* haujamalizika.

Nasema tatizo hili lilianza tangu tarehe 18 Oktoba, 2012, lakini ukweli uliopo hadi hivi leo serikali haijapata ufumbuzi lini itarusha matangazo ya *digital*. Sababu kubwa inayosababisha kutokuwa na ufumbuzi kumeonekana kwamba mkataba tulioingiliana nao ambao nimesema uko kwa mwanasheria na mwanasheria anaufanyia kazi kwa kipindi kirefu.

Mkataba huu umeonesha kwamba sisi tumepata ving'amuzi ambavyo havina ubora na ving'amuzi vile hivi sasa vingi vyao havitumiki hata mimi mwenyewe nimenunua, lakini hicho king'amuzi hivi sasa sikitumii.

Kwa hivyo, kutokana na mvutano ambao tunao mwanasheria ataweka sawa suala hili. Na nataka nilithibitishie Baraza wakituacha sisi tukilifuatilia kwa kina hili suala tutapofika pahali utaratibu wote na hatua zote tutazileta hapa Barazani. Tutaleta taratibu zote zinazohitajika, ili tuweze kuwaeleza Wajumbe tumefikia wapi juu ya suala hili. Kwa hivyo, tunataka tukiri kwamba kweli wakati mkataba ule unafikiwa Kampuni ya *AGAPE* pamoja na Kampuni ya *Lakes Digital* na Kampuni za *HUAWEI* zilishiriki katika kuingia kwenye mkataba huo na Kampuni ya *AGAPE* ilishinda kwa mujibu wa taratibu na sheria zetu tunazowezesha kuwapa *tender* zile kampuni zilizoshiriki.

Mhe. Naibu Spika, nataka niwathibitishie Wajumbe kwamba *AGAPE* tafauti na ilivyochangiwa na watu wengine, Mhe. Mohammedraza Hassanali amechangia hapa kwamba zaidi ya *eight millions US$* zimewekwa kwenye mkataba huo sio kweli. Mkataba ulikuwa na thamani kama nilivyoeleza wakati ule, mkataba ulikuwa na thamani ambazo ni US$ 3,921,000 nilieleza wakati ule.

Kwa hivyo, kuipotosha na kuwapotosha wananchi kwamba mkataba ule ulikuwa na pesa nyingi aa, tuchukue taarifa zilizokuwa sahihi na ninawaomba Wajumbe wawe watulivu wafuate taarifa, kamati yao ipo, itakuja kwenye taratibu za kuweza kuja katika maofisi yetu na kupata taarifa kwa kina, tutawapatia taarifa zote zinazohitajika, tutawapatia *document* zote zinazohitajika, ili wao wawe na taarifa kamili.

Mhe. Naibu Spika, kutokana na hali hiyo napenda sasa niwaombe tena Waheshimiwa Wajumbe, kwamba sisi binafsi tunalifuatilia kwa kina suala hili na tutalifanyia kazi na hatuna nia ya kumlinda, yeyote ambaye atakuwa kwa njia moja au nyengine kashiriki kuitia serikali kwenye jambo hili. Kutokana na

hali hiyo basi nawaomba Wajumbe wawe watulivu, wana maamuzi yao ukweli ndio huo tunawaeleza na hali halisi ndio hiyo hakuna haja ya kusema leo nakwenda kuzuwia kifungu fulani cha Wizara ya Fedha kwa sababu kuna chembe chembe za *AGAPE*. Mwanasheria anao mkataba, anapitia vipengele na atatoa utaratibu kamili.

Mhe. Naibu Spika, ahsante sana naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Naibu Spika, awali ya yoe na mimi sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uzima afya, lakini pili na mimi kwa niaba ya wananchi wenzangu wa Jimbo la Chwaka naomba niseme kwmaba tunaunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja. Tunaunga mkono bajeti hii kwa sababu tunaamini kwamba matarajio, malengo na madhumuni ya bajeti hii ni kusukuma mbele gurudumu la maendeleo kwa wananchi wetu wa Zanzibar. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, wakati wa majadiliano kuna baadhi ya mambo ambayo Waheshimiwa Wajumbe wamejaribu kuyauliza, kuyaeleza nami sina budi nikiwa ni sehemu ya serikali kutoa ufafanuzi kwa baadhi ya mambo hayo, ili tuweze kuelewana na kujenga uelewa wa pamoja katika kuwatumikia wananchi wetu wa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, miongoni mwa mambo ambayo yameulizwa hapa liliulizwa suala zima la Zanzibar kujiunga na kujitoa katika *OIC* kwa msingi wa kwamba *OIC* inayo uwezo wa kuisaidia Zanzibar kiuchumi. Suala likawa kwa nini Zanzibar imejiunga ama Zanzibar kwa nini ikawa imejitoa.

Mhe. Naibu Spika, suala la *OIC* ni Shirika la hiyari lenye mnasaba na mafungamano na itikadi za kidini kwa maana ya kwamba ni Shirika la Uislamu lenye mnasaba na itikadi hizo lililoanzishwa Mjini Rabat nchini Morocco mwaka 1969 lililotokana na kisa cha *Aqsa* kilichotokea nchini Israel.

Baadae mwaka uliofuata Makao Makuu yakabadilishwa yakawa Jeddah - Saudi Arabia na madhumuni makubwa ya shirika hili ni mambo mawili; kwanza ni kuendeleza utamaduni mzuri wa Dini ya Kiislamu lakini pili ni kuzisaidia nchi wanachama katika msingi mzima wa kuwasaidia kiuchumi.

Mhe. Naibu Spika, shirika hili nalo limepata mafanikio; limeanza na Wajumbe 25 hivi sasa lina Wajumbe 57 na wajumbe wengine watano waangalizi. Lakini jambo la msingi la kujiuliza ni maswali mawili; la kwanza la kujiuliza ni

kwamba je, haja au hoja ya Zanzibar kujiunga na *OIC* ipo au haipo? Majibu bila shaka hoja na haja Zanzibar kujiunga na *OIC* ipo, kwa sababu hoja na haja kubwa ilikuwa ni Zanzibar kujisaidia kiuchumi na bado tatizo la uchumi tunalo na tunaamini tungejiunga na *OIC* tungeweza kupata msaada wa kuwasaidia wananchi wetu katika harakati za kimaendeleo.

Swali la pili tujiulize hapo hapo je, hoja na haja ama sababu za Zanzibar kujiunga na kujiondoa sababu zipo au hazipo? Majibu bila shaka kwamba sababu zipo, kwamba Zanzibar ilijiunga na ikajiondoa. Tulijiunga mwaka 1992 mwaka uliofuata 1993 tukalazimika tujiondoe. Sababu kubwa ya kujiondoa ilikuwa ni tatizo la kikatiba na sitegemei kama Zanzibar tutakuwa tuko tayari tena kuingia katika mgogoro wa kuvunja Katiba ya Jamhuri ya Muungano.

Mhe. Spika, ukisoma ibara ya 4 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano imeeleza wazi mambo yepi ya Muungano na si yepi ya Muungano. Suala la mambo ya nje kwa mujibu wa katiba yetu ya mwaka 1977 ni jambo la Muungano. Hivyo, bado kipingamizi au kizuizi kilichotufanya mwaka 1993 tukatoka mpaka leo hii bado kipo. Lakini kwa kuwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi imeona na kutafakari kwa kina masuala haya tayari katika mchakato wa katiba mpya inayopendekezwa ukisoma ibara ya 76 kifungu cha 2 imetoa fursa hii ya kutosha.

Kwa hiyo, wito wangu na ombi langu kwa Waheshimiwa Wajumbe sote kwa umoja wetu ukifika wakati wa kwenda kupiga kura ya maoni ya katiba inayopendekezwa twende tukawashajihishe watu wetu wapige kura ya ndiyo, ili tuweze kupata katiba hii mpya ili tuwezekuondokana na hayo mengine ambayo tunayaeleza.

Mhe. Naibu Spika, tutakapochagua katiba kwa mujibu wa ibara hii sio tu kwamba Zanzibar tutapata nafasi ya kujiunga na *OIC,* lakini yapo mashirika mengine ambayo pia tutapata nafasi ya kujiunga, ili tuweze kuendeleza na kukuza uchumi wetu. Miongoni mwa mashirika hayo ni Shirila la *Alliance of Small Islands* na Shirika la *Indian Ocean Commission*. Hayo yote ni sehemu ya mashirika ambayo Zanzibar tunaweza tukanufaika katika harakati za kuendeleza uchumi wa nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine limeulizwa na wachangiaji wengi ambao naamini wote walikuwa na madhumuni na hamu ya kutaka kujua nalo ni suala la ujenzi wa jengo jipya la abiria yaani *Zanzibar Terminall II*. Suala hili Mhe. Naibu Spika, ni suala ambalo limechukuwa muda mrefu, takribani sasa hivi ni mwaka wa tano kwenda wa sita jengo halijakamilika na hapa nadhani ndio

sababu inayowapelekea baadhi ya Wajumbe kuwa na hamu ya kutaka kujua nini kilichopelekea mpaka jengo hili likawa halijamilika na siku zimekuwa nyingi.

Mhe. Naibu Spika, ujenzi wa jengo lile unasababu zake za msingi ambapo chimbuko la ujenzi wa jengo lile unatokana na mipango ya serikali kutoka mwaka 2004 mpaka 2009 katika mradi ule mkubwa uliofadhiliwa na *World Bank* na *AB* unaohusiana na suala zima la *Zanzibar Transport Master Plan*.

Katika mradi ule ulitoa mapendekezo mengi miongoni mwao ni ujenzi wa jengo hilo jipya, urefushaji wa barabara ya kurukia ndege, ujenzi wa maeneo ya maegesho, ujenzi maeneo ya kupitia ndege, mfumo wa utawala wa usafiri baharini, mfumo wa barabara, miradi ya barabara hizi zinazoingia mjini na miradi mingine yote.

Mhe. Naibu Spika, tumeweza kubahatika kukamilisha baadhi ya miradi kwa mfano, mradi wa kurefusha barabara ya kurukia ndege umekalimika, mradi wa maegesho ya ndege umekamilika, miradi ya barabara zinazoingia mjini unaendelea, mradi wa kubadilisha mfumo baharini umekamilika, tumepata *ZMA*, tumepata *Zanzibar Transport Act* ya mwaka 2006.

Sasa jengo hili lilipoanza kujengwa linatokana na mkataba uliongia Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mwaka 2009 na mwaka 2010 Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ikaingia mkataba ya kampuni ya ujenzi wa *Beijing Construction Engineering Group*.

Madhumuni ya kujenga jengo hili ni kutaka kijifungua kiuchumi na kuengeza idadi ya watumiaji wa ndege pamoja na uimarishaji wa huduma hizo.

Mhe. Naibu Spika, ujenzi wa jengo hili ulikusudiwa kukamilika katika kipindi cha miezi 36 na mjenzi tulikubaliana kwamba ajenge kwa mfumo wa ku-*design and Building* mfumo huo ulikuwa ni mpya kwetu na kwa mujibu wa mfumo ule wajenzi wana-*design*, serikali imetakiwa imridhie baada ya kumridhia tunaendelea na ujenzi.

Serikali kwa kuona kwamba haikuwa na watalaamu iliajiri kampuni ya *ATM* kufanya kazi kwa niaba ya serikali ya kuridhia na kupitisha michoro, ili harakati za ujenzi zianze kutekelezwa.

Mhe. Naibu Spika, ujenzi ule katika utekelezaji wake serikali ikabaini kuna mapungufu mengi na makubwa. Mwaka 2012 serikali ikaingia *addendum* ya

kwanza ambayo ilipelekea kutoka gharama kutoka milioni 70.4 mpaka milioni 82 na *addendum* hii sio tu kwa kutaka kujiridhisha kwa maana kwamba ya anasa. Hapana, kulikuwa na mambo ya msingi ambayo katika mchoro ule wa awali hayakuwemo.

Jambo la kwanza eneo la jengo lilikuwa ni dogo lilikuwa takrbani *square metre* 15,000 ikabidi katika *addendum* ile iongozwe ifikie kumi na saba mpaka kumi na nane mpaka elfu ishirini na moja.

La pili ilionekana nafasi ya mle ndani lazima ibadilishwe tena katika mfumo wa ujenzi kuna baadhi ya nafasi zikaondoshwa na baadhi ya vitu vikaondishwa.

La tatu lilikuwa ni *super structure* kwa maana kwamba ile *infrastructure* itakapokamilika, jengo haliwezi kutumika moja kwa moja kama hatukuongeza vifaa na vitendea kazi, ili litakapokamilika lianze kufanyiwa kazi.

Mhe. Naibu Spika, kwa bahati mbaya wasimamizi walionekana uwezo wao ni mdogo kampuni ya *ATM* ikashindwa kusimamia vizuri serikali ikavunja nao mkataba, serikali ikaingia mkataba ya kampuni ya *ADPI* mwaka 2013. Kama sote tutakumbuka mwaka 2013/14 jengo hili likaja na kelele kubwa sana katika Baraza hili tukufu Mhe. Naibu Spika, na lilipokuja zogo kubwa ilikuwa kwamba kwa nini jengo lisivunjwe lisitishwe.

Kampuni ya *ADPI* ilipewa kazi ya kuishauri serikali kuhusiana na dhana hiyo ya kuvunja jengo ama ushauri mwengine mzuri utakaoweza kuisaidia serikali katika ukamilishaji wa ujenzi wa jengo lile. Kwa bahati nzuri kampuni ya *ADPI* ilikuja na *alternatives* nne; *alternative* ya *A1, A2* na *B1*, B2.

Ukisoma *alternatives* tatu zilikuwa zinazungumzia kwamba utakapokamilisha jengo maegesho ya ndege, ndege zitaegeshwa kwa kuelekea upande wa Magharibu ukichukuwa *apron* itakayokuwepo baada ya kukamilika kwa jengo ndege kubwa ikiegeshwa maana yake unatengeneza *obstacle* katika *tax way* na *apron* iliyopo hivi sasa. Serikali ikaona *option* hiyo hatutoichukuwa kwa sababu tutashindwa kuegesha ndege kubwa.

Option ya pili kwamba tuchukuwe jengo lilipo tuongeze *apron* upande wa kusini lakini ndege zikiegeshwa zielekee upande wa Magharibi halkadhalika itaonekana kama itaegeshwa ndege kubwa za *air bus* hazitiweza kutoa nafasi nzuri kwa ajili ya watumiaji. Serikali ikafikia maamuzi kwamba tuende katika *option* itakayowezesha upande wa mashariki ya jengo kutumiwa na ndege

ndogo na upande wa kusini tujenge *apron* mpya ambayo itaendesha ndege kwa kuelekea upande wa Kaskazini.

Sasa Mhe. Naibu Spika, kwa mujibu wa mchoro wa awali kuna kitu kinaitwa *arrow bridge* ile mikonga. Mikonga ile ilikuwa mitatu kwa mujibu wa mkataba wetu wa awali na katika mikonga ile ingeweza kuhudumia ndege za *Boeing* 787 na *ATR* isingeweza kuhudumia ndege kubwa kama vile mataraajio yetu. Serikali ikaona hapa mikonga hii lazima iondoshwe na iwekwe mengine na kwa sababu tulikubaliana kwamba twende katika option ya kujenga *apron* upande wa kusini kwa ajili ya kuegesha ndege kubwa tukachukuwa idadi ya zaida sasa ya mikonga, kutoka mikonga *type 'c'* kwenda *type 'e'*. Unapozungumza *type 'e'* maana yake ni mikonga mikubwa ya kuweza ku- *serve* ndege kubwa mpaka *airbus*.

Mhe. Naibu Spika, la pili lilionekana ni kwamba upande huu wa kusini tutakapojenga *apron* mana yake hili ni jambo la ziada halimo katika mkataba na *apron* ile imegharimu takribani dola milioni ishirini na mbili. Kwa hivyo, gharama zaidi zitaongezeka.

Jambo jengine lilionekana lina nafasi ya lile jengo tunatoka jengo letu lililojengwa mwaka 1974 linalotumia watu laki tano kwa kujibana wanapita laki saba, tunaona itakuwa si busara, kujenga jengo jipya tutakalolimaliza kwa hudumia watu miliona moja. Baada ya kuongeza eneo hili kutoka *square metre* kumi na tano mpaka *square metre* ishirini na tano, sasa tuna uwezo wa kuwahudumia watu milioni moja na nukta sita.

Sasa kwa mujibu wa ule mkataba tulipaswa mara tu baada ya kutiliana mkataba tuanze kufanya nao malipo na asilimia kumi na tano tayari tukalipa mwaka ule ule mwaka 2010 na mwaka 2011 tukatakiwa kulipa awamu ya pili, 2012 kwa mujibu wa mkataba wakati tunataka kutekeleza ulipaji malipo yakasitishwa na sababu ya kusitisha malipo ilikuwa ni utendaji wa kazi sisi wenyewe serikalini ulikuwa haujaturidhisha na ndipo tulipofanya mabadiliko ya msimamizi kumuondoa *ATM* kuja na *ADPI* .

Sasa Mhe. Naibu Spika, naomba nilieleze tu Baraza lako tukufu kwamba kusita kwa jengo lile hakutokani tu na utashi wa serikali. Lakini zipo sababu za msingi zikiwepo hizo za kifundi ambazo kwa sehemu kubwa sana serikali imeweza kuzifanyia kazi na hivi sasa serikali iko vizuri kutaka kuona mradi huu unakamilika.

Mhe. Naibu Spika, jambo la pili ambalo limepelekea mradi huu kusita mikataba ile miwili ya *addendum*. *Addendum* ya kwanza na *addendum* ya pili ilikuwa ni makubaliano baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na mjenzi. Lakini sote tunajua kwamba fedha za kutekeleza mradi huu hazitoki serikalini moja kwa moja. Fedha za kutekeleza mradi huu zinatoka katika mkopo katika Bank ya *Exim* ya China.

Kwa hiyo, sehemu ya pili sasa lazima muende katika makubaliano baina ya Serikali ya Zanzibar, kwa mfumo wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano kama dhamana na muende na Benki ambayo ndio wanaotukopesha.

Kwa hiyo, majadiliano baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Benki ya *Exim* ya China ndio ambayo yamepelekea mpaka sasa hivi fedha zikawa hazijapatikana na ndiko kulikopelekea sasa hivi mradi ukawa umesita katika utekelezaji wake.

Imani yangu kwamba Mhe. Waziri wa Fedha atakapokuja kufanya majumuisho atachukuwa nafasi nzuri sana ya kutueleza hatua gani katika upatikanaji wa fedha ambapo jitihada za serikali zimechukuliwa na wapi ambapo tumefikia, ili tuweze kukamilisha ujenzi wa jengo hili.

Mhe. Naibu Spika, jengo hili likikamilika litakuwa na uwezo wa kutoa huduma kama viwanja vyengine vya kimataifa vilivyopo duniani na miongoni mwa mahitaji hayo ndiyo yaliyopelekea tukaona jengo hili ni bora tuchelewe kulikoni kulikamilisha kwa haraka lakini faida na malengo tuliyoyakusudia yakawa yameshindwa kufikia.

Kwa hiyo, niwaombe tu Waheshimiwa Wajumbe kwamba jambo hili sote tunalitaka na sote tunatamani ingekuwa jana kama jengo hili limekamilika. Lakini kutokana na mambo hayo mawili; kwanza suala la kiufundi na pili kutokana na kuchelewa upatikanaji wa fedha hatukuwa na nafasi wala hatukuwa na sababu ya kuweza kulikamilisha jengo hili kama vile ambavyo tumetarajia pale mwanzo.

Tukumbuke kwamba mkopo wa awali ulikuwa dola milioni 70.4, tumeengeza sasa hivi tuko dola milioni 124, yote hii ni kwa ajili ya kutaka kupata uwanja ama jengo ambalo litakidhi mahitaji na matakwa ya kisheria kwa mujibu wa taratibu za *IATA*, kwa mujibu wa taratibu za *AKOA***.** Lakini pia jengo ambalo litaweza ku- *focus* angalau miaka 30 mbele katika matumizi yake.

Mhe. Naibu Spika, naomba nimalizie kwa kurejea tena kauli yangu kwamba mimi mwenyewe binafsi pamoja na wananchi wangu ninaowawakilishi wa Jimbo la Chokwa tunaunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja. Mhe. Naibu Spika, nakushukuru. (*Makofi*)

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nataka pia niwashukuru Mawaziri wenzangu na Manaibu Manaibu Mawaziri walionitangulia kwa kutoa ufafanuzi mzuri kuhusu hoja iliyo mbele yetu.

Pia nichukuwe fursa hii kumpongeza Waziri wa Fedha kwa kuwasilisha hotuba yake vizuri na naamini atakapokuja kutoa majumuisho atazidi kueleza kwa kina yale yote Waheshimiwa Wajumbe waliyoyataka kuyasikia.

Nichukuwe fursa hii kuwapongeza sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili tukufu kwa kazi kubwa na nzuri wanayoifanya katika kuishauri serikali yetu na kutoa maoni yao ambayo wanayo fursa ya kikatiba ya kufanya hivyo.

Kwa hiyo, wale wote waliochangia na waliokuwa hawakupata nafasi ya kuchangia tunawapongeza kwa sababu tumeona umakini wao na kazi kubwa wanayoifanya katika kuhakikisha tunashirikiana tunajenga nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, naelewa pia dhana ya Wajumbe wetu katika kupambana na ubadhirifu, katika kupambana na rushwa na dhamira yao njema ya kutaka mabadiliko ya maendeleo katika nchi yetu. Naelewa fika kwamba wanahitaji maendeleo ya haraka na kwa bahati nzuri dhana ambayo wanayo ndio dhana na dhamira ya serikali hiyo hiyo, kupambana na vitendo vyote vya ubadhirifu kujenga nidhamu katika serikali, kujenga uadilifu katika serikali na kuleta mabadiliko makubwa ya kimaendeleo katika nchi yetu.

Kwa hivyo, Waheshimiwa Wajumbe na Serikali tunazungumza lugha moja. Nia yetu ni kutoa huduma bora kwa wananchi, naelewa Waheshimiwa mlizungumzia sana suala la *terminal II*, mlizungumzia sana suala la *Digital* la *ZBC* maarufu *AGAPE* na kadhalika na katika kuzungumzia huko mlikuwa na nia njema ya kutaka kuona jengo letu lile lipo tayari linafanya kazi na *terminall II* na kuona *TV* yetu iko tayari inatoa huduma vizuri.

Nataka niwashukuru sana Mhe. Waziri wa Habari kwa maelezo yake mazuri kuhusu *AGAPE* na vile vile nimshukuru sana Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais kwa maelezo yake mazuri ambayo ameeleza kuhusu *terminal II.*

Naamini sana Waheshimiwa Wajumbe watakuwa wameelewa vizuri na kwa kina suala ambalo limeelezwa na walitaka wao mpaka kufikia kuundwa kwa kamati teule. Naamini kwa sasa kwa maelezo hayo Waheshimiwa Wajumbe watakubaliana na mimi kwamba maelezo yametosha sana. Lakini pia niwaeleze Waheshimiwa Wajumbe kwamba ni vizuri tukawa tunasubira sana katika kutenda mambo yetu na katika kuleta hoja zetu na subira yenyewe inakuja katika kufanya utafiti zaidi. Mimi nakubaliana na nyie kabisa kwamba pale penye mapungufu, pale penye udhaifu, pale penye uzembe hatua zichukuliwe.

Lakini jambo zuri sana la kupata maamuzi yaliyo sahihi ni kufanya utafiti wa kina na kwa kuwa baada ya kuakhirisha Baraza Kamati zetu za kudumu za Baraza la Wawakilishi zitapata nafasi kubwa ya kutembelea sekta husika, ili kuweza kujiridhisha haya mambo ambayo tumeyasikia kwa kuonana na wadau husika, ili kuyapata mambo kwa upana wake.

Kwa hivyo, ilikuwa ni vyema kwa Waheshimiwa Wajumbe kabla ya kufikia hatua za kuunda Kamati Teule ni vizuri sana twende kwa sekta husika tupate maelezo, kwa sababu maelezo yote ambayo yatatoka hapa hayatatoka kwa kina zaidi kama pale waziri na wataalamu wake watakapokaa mkawauliza wakaeleza kinaga ubaga.

Bahati nzuri mara hii kwa mujibu wa ratiba yetu inavyoonesha mwezi wa Septemba tunakutana tena hapa. Kwa hiyo, mtakuwa na nafasi ya kutosha ya kwenda katika wizara husika kuuliza zaidi kupata maelezo ya kina kwa msingi wa kupata majibu sahihi na sisi katika serikali kama alivyosema waziri hapa hatuna haja wala hatuna nia ya kumficha mbadhirifu yeyote yule au mzembe yeyote yule au mtu yeyote anaekwenda kinyume na utaratibu.

Sisi tunaungana na nyinyi sana katika kuyafichua maovu, lakini lazima tuyafiyafichukue maovu kwa njia zilizokuwepo na kwa kutenda haki kwa kila muhusika. Ni njia pekee ya kufanya hivyo ni kufanya utafiti wa kina. Kwa hivyo Waheshimiwa Wajumbe kwa sababu ipo nafasi kubwa sana ya kwenda kupitia Kamati zetu, na kama yupo Mjumbe hayupo kwenye Kamati husika basi anayo haki ya kuomba Kamati na kuwa mshiriki kwenye Kamati hiyo na kuwa Mjumbe mualikwa, ili akapata taarifa za kutosha na pale ndipo atakapokuwa na usahihi wa hoja ambazo atazileta hapa.

Mhe. Naibu Spika, na hapa tunapokuja na taarifa zilizokamilika, taarifa zenye mashiko vizuri, serikali siku zote huwa haikatai ushauri ambao Wajumbe wanautoa. Hivyo ningewaomba sana Waheshimiwa Wajumbe twendeni tukafanye kazi kwenye Kamati zetu, bado hatukupata fursa katika muda

tulioanza wa Baraza wa kina wa kutosha kupitia sekta zetu. Tutakapoondoka hapa tukenda kupitia katika sekta zetu, ndiyo tutaona mapungufu gani yapo katika sekta, yale yanayohitaji kurekebishwa wakati wa kushauriana au kwenye sekta yanachukuliwa hatua na yale ambayo yatahitaji kuja kuzungumzwa hapa, tunayaleta hapa tunayazungumza, tunayazungumza kitu kimoja, kati ya Wajumbe na Serikali.

Mhe. Naibu Spika, na siku zote uendeshaji mzuri wa nchi unahitaji mashirikiano makubwa kati ya Serikali na Wajumbe wa Baraza letu Tukufu. Siku zote Serikali yenu hii ni sikivu na ipo tayari kwa kiasi kikubwa kushirikiana na nyinyi ili tuweze kufanya mambo yetu vizuri na kwa pamoja. Kwa hivyo Waheshimiwa Wajumbe niwaambie tu kwamba tunapofanya maamuzi ya haraka haraka, wakati mwengine huwa hayajakamilika kufikia hatua ambazo tungependa zifikie. Unapoleta hoja hoja ikawa na udhaifu hoja yako na ikapata majibu sahihi katika Serikali, wananchi huko wanatusikiliza ambao walituchagua, wanakuona Mjumbe hukufanya kazi yako vizuri ya kutathmini na utafiti wa kutosha. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, matokeo yake mara nyengine inaweza kukupa tofauti kati ya wapiga kura wako na wewe mwenyewe. Hivyo ni vizuri sana kufanya utafiti wa kina na tumeona hapa na nyinyi wenyewe ni mashahidi, wapo wenzetu katika kipindi kilichopita walikuwa wanakuja kwa haraka haraka na hoja za haraka haraka bila ya kufanya utafiti wa kina, na matokeo yake leo hawamo humu ndani. Kwa hivyo mimi ushauri wangu Ndugu Wajumbe tufanye utafiti wa kina, tukutane na sekta husika ili ukija na hoja hapa inakuwa pia ni rahisi kwa serikali kukubali hoja yenyewe na kushirikiana kufanya kazi kwa pamoja.

Mhe. Naibu Spika, Waheshimiwa kama walivyoeleza Mawaziri walionitangulia na mimi ni mmoja ninashukuru Mwenyezi Mungu na ninamshukuru Rais wangu, kwa kuwa nilikuwepo katika awamu ya Kwanza ya Rais Dkt. Ali Mohamed Shein, na kazi moja kubwa ambayo Serikali yetu ilikuwa imefanya ni masuala haya mawili. Moja lilihusu *terminal II* na moja lilohusu suala la *AGAPE*.

Mhe. Naibu Spika, Serikali kwa kipindi cha ziada ya miaka mitatu ilishughulika na jambo hili kwa kina sana, ili kuhakikisha lifikie hatua nzuri. Na ndiyo maana Mhe.Waziri wa Nchi (OR)BLM kalieleza kwa kina sana. Waheshimiwa kwa hali ilivyokuwa, kwa sababu alieleza hapa kwamba jengo lile la *terminal II*, pahala lilipo lilikuwa limo ndani ya mita 60 kutoka kwenye *runway*, kwenye sehemu ya kurukia ndege. Na ilitakiwa ujenzi ule uwe nje ya mita 60 na matokeo yake linapokuwa ndani ya mita 60, ni yale ambayo

aliyaeleza Mhe. Waziri wa Nchi (OR) BLM kwamba zile ndege kubwa hazingeweza kutua moja kwa moja zikaweza kufunga kwenye jengo letu na tukatumia *bridge* ile kuingia ndani moja kwa moja.

Mhe. Naibu Spika, na ndiyo maana Serikali kwa utulivu mkubwa ikatafuta kila namna ya hekma na kutafuta washauri waelekezi, ili kufikia hatua ambayo tumefikia. Vyenginevyo katika hatua ya awali lilikuja mpaka shauri ya kuvunja lile jengo.

Sasa ukitazama shauri hiyo lilikuwa na athari na ndugu zetu wa Jamhuri ya Watu China. Msaada ambao wametupa wa kutukopesha, leo waje waone jengo tumeanza kulijenga halafu tunalipiga michi linakuwa chini. Uhusiano wetu wa kidiplomasia ungekuwa na mtihani kidogo lakini pia hata wananchi wetu wasingeona kama huo ni uamuzi wa busara.

Kwa hivyo maelezo ya aliyotoa Mhe. Waziri wa Nchi (OR) BLM ni maelezo ya kina na nia ya Serikali ni kufanya tuwe na jengo bora linatimiza vigezo, ili ndege kubwa na ndege ndogo ziweze kutua vizuri na tuweze kutoa huduma bora. Kwa hivyo kulikuwa na kazi kubwa ya kiufundi ambayo ilihitaji irekebishwe. Kwa msingi huo ndiyo maana marekebisho hayo ikasababisha kuongezeka kwa matumizi na ikasababisha kuchelewa kumalizika. Kwa sababu ilituchukua miaka miwili kusimamisha ujenzi usiendelee kwa ajili ya kutafakari jambo hili.

Mhe. Naibu Spika, sasa ni sisi binadamu ndani ya Serikali lakini dhamira yetu ilikuwa njema ya kuhakikisha kwamba tunapata jengo zuri, tunatoa huduma bora kwa maslahi yetu ya sasa na maslahi ya vizazi vijavyo. Inawezekana kabisa Waheshimiwa Wajumbe mukaona katika hatua zote hizo bado zipo kasoro kwa watendaji ama kwa viongozi.

Jambo hilo linaweza likawa limetokea lakini njia nzuri na sahihi ya kupata kujua udhaifu upo wapi ni kwenda kwenye sekta husika, mukapata taarifa za ziada na pale mutakapokuja na taarifa za kina za ziada zinazoonesha mapungufu, ninataka niwahakikishie Serikali itaunga mkono na nyinyi, ili jambo hilo twende nalo sambamba nalo na kuchukua hatua zinazofaa. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, hivyo ushauri wangu kwa sasa tusubiri mwende kwenye sekta husika mukutane na Mawaziri husika na timu yake ya wataalamu, ili kupata taarifa za ziada na tufanye maamuzi yenye msingi kwa ajili ya maslahi ya nchi yetu. Wala serikali haina nia ya kumpigia kifua yeyote au kumtetea mtu

yeyote. Nia yetu ni kuweka usafi, uadilifu na maendeleo kwa wananchi wote. Hiyo ndiyo dhamira yetu sote. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, kuhusu suala la *AGAPE*. Waheshimiwa katika eneo hili serikali imefanya kazi kubwa sana. Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo amelieleza kwa kina na ninampongeza sana namna alivyolieleza, lakini tujue tu kwamba serikali ya awali ilipopata suala hili la kutaka kuzima mitambo ya *analogue* kuingia katika *digital*, makampuni yale yaliyojitokeza kutaka ku-*supply* mashine hizo na mitambo hiyo na vifaa vyengine vinavyohitajika, gharama za awali zilikuwa ni Dola milioni ishirini na nane. Maana yake ni zaidi ya bilioni hamsini na sita.

Mhe. Naibu Spika, kwa jitihada za serikali kwa busara zake na uangalifu wa hali ya juu. Ndipo tulipoangukia kwa *AGAPE* tukafanya hii kazi mpaka hivi leo haijafika hata Dola milioni tatu. Maana matumizi yote ya mradi mzima huu mpaka sasa ni bilioni tano nukta tano. Sasa maana yake nini. Tumeweza kuokoa zaidi ya bilioni hamsini katika mradi huu. Yote hiyo ni busara, ustahamilivu na umakini wa kutafuta suluhu iliyo sahihi. Ninataka niwahakikishie hapa palipobaki patafikia napo suluhu nzuri, kwa sababu nimependa sana utendaji wa Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo namna anavyoshirikiana na watendaji wake katika kupata uvumbuzi wa tatizo hili.

Tumpeni muda na ninaamini mutapokwenda wizarani, yeye akiwa na watendaji mutayapata mambo kwa kina zaidi. Tunapopata mambo kwa kina ndiyo tunapofanya maamuzi sahihi kwa maslahi ya nchi yetu. (*Makofi*)

Kwa hivyo jitihada zote zinazofanywa na serikali zilifanywa kwa nia njema. Ninataka niwahakikishie mtambo ule wa *AGAPE* ni mzuri, una ubora, unatimiza vigezo vyote. Yapo matatizo madogo madogo katika *connection* hizi na suala kubwa ni namna ya kuunganisha ile mitambo ile na huu mkonga wa taifa, ili mawimbi yale yaweze kurushwa vizuri na kuweza kuona vizuri katika TV zetu na ving'amuzi vyetu. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, palipobaki ni safari ndogo sana Waheshimiwa. Mimi ninachowaombeni na ninawanasihi tuipitishe bajeti yetu hii ya Wizara ya Fedha na Mipango. Bajeti hii ya Wizara ya Fedha na Mipango ni Wizara ya Fedha, siyo bajeti ile ya taifa.

Ukweli pale mwanzo alipowasilisha bajeti ya taifa ndiyo tulikuwa na nafasi nzuri ya kuyaeleza ya *AGAPE*, ya kuyaeleza ya *terminal II* na mengine kwa

sababu ile ilikuwa ni bajeti ya taifa. Hii ni Wizara wanawasilisha matumizi ya wizara yao. Lakini tunapoyazungumza yenye mapungufu ni haki ya Mjumbe na sisi Serikali tunayasikia, tunazidi kuyafanyia kazi na tunakubali kwamba kila ushirikiano tunaoutoa kwa Wajumbe ili tupate matumaini mema, tupate uamuzi mzuri, ili tuweze kuwahudumia vizuri zaidi wananchi wetu.

Kwa hivyo niwaombeni sana Waheshimiwa Wajumbe tuhakikishe kwamba tunaipitisha bajeti yetu hii na hayo mengine yote kwanza twende kwenye sekta husika kuhakikisha kwamba tunafanya kwa wajibu huu, ili yale mapungufu tuyaone kwa kina na mutakuja kushauri hapa, ninawahakikishieni Waheshimiwa Wajumbe hatua zitachukuliwa dhidi ya wale wote ambao wamekwenda kinyume na taratibu na sheria. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, na nyote munaelewa uadilifu wa Rais wetu, umakini wa Rais wetu namna ambavyo anahitaji Mawaziri wake, utendaji ndani ya serikali wawe waadilifu, makini, wafanye kazi zao vizuri, tuache kufanya kazi kwa mazoea. Mimi ninakubaliana na nyinyi sana na ushauri wenu na ninakuhakikishieni ndani ya serikali siku zote tunaheshimu mashauri yenu, tutaendelea kuyafanyia kazi.

Mhe. Naibu Spika, ninawatakia kila la kheri lakini ninawaombeni sana muipitishe bajeti hii. (*Makofi*)

Baada ya hayo Mhe. Naibu Spika, na mimi ninaiunga mkono kwa asilimia mia moja hoja hii ya Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, na sote pamoja tuunge mkono hoja hii, ili tumpe nafasi Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango akafanye kazi, kama alivyosema Mhe. Said Soud Said Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum kwamba Waziri wa Fedha na Mipango ni mpya, anahitaji kufanya kazi, ameonesha umakini mkubwa katika utendaji wake wa kazi, ninaamini nyote mutafurahi wakati anapotekeleza wajibu wake. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, ninawashukuru sana. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Makamu wa Pili wa Rais. Sasa nimwite Waziri wa Fedha na Mipango kwa ajili ya kufanya majumuisho. Mhe. Waziri karibu.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Naibu Spika, awali ya yote ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia neema ya uhai na uzima na kutuwezesha kukutana leo hii kuendelea kujadili mambo muhimu kwa taifa letu.

Naomba kuchukua fursa hii pia kukushukuru sana wewe Mhe. Naibu Spika, kwa namna unavyoliendesha Baraza letu kwa umakini na umahiri mkubwa.

Pia ninamshukuru Mhe. Spika, mwenyewe na Wenyeviti wa Baraza kwa kuliendesha Baraza hili kwa ufanisi unaostahiki.(*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, ninawashukuru sana Wajumbe wa Baraza kwa michango yao mbali mbali waliyoitoa wakati wakichangia hotuba ya wizara yangu. Ni imani yangu kwamba michango yote iliyotolewa na masuala yaliyoulizwa nia yake ni kujenga kwa kuamsha ari ya kufanya kazi kwa bidii na uadilifu jambo ambalo sote ndiyo dhamira yetu.

Naomba kupokea kwa niaba ya Mhe. Rais Dkt. Ali Mohamed Shein pongezi zote zilizotolewa kwake kwa kutekeleza vyema sera na mipango ya serikali, lakini pia kwa kusimamia utekelezaji wa ilani ya Chama cha Mapinduzi.(*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, ninazipokea pongezi zilizotolewa wizara yetu kwa moyo mkunjufu, ninasema ahsanteni sana. Mhe. Naibu Spika, hoja nyingi zimetolewa na Waheshimiwa Wajumbe nyengine zikitaka ufafanuzi wa kina. Ninawashukuru Waheshimiwa Wajumbe waliotoa au waliotaka ufafanuzi kwa maeneo mbali mbali bila ya kuonesha nia ya kuzuia kifungu. Karibu Waheshimiwa Wajumbe wote isipokuwa Mjumbe mmoja waliunga mkono hoja ya wizara yangu kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

Hivyo kwa mujibu wa Kanuni ya 98 ya Baraza la Wawakilishi Toleo ya 2012 fasili ya 6 (c) mpaka (g). Hakuna Mheshimiwa Mjumbe yeyote isipokuwa Mheshimiwa huyo mmoja atakayeweza kupunguza fungu lolote kwa vile hakuonesha nia yake hiyo wakati wa kuchangia hoja.

Mhe. Naibu Spika, hoja nyingi zilizotolewa na Waheshimiwa Wajumbe ikiwemo hoja ya *AGAPE*, ujenzi wa jengo la abiria katika Uwanja wa Ndege Abeid Amani Karume, pia Zanzibar kujiunga *OIC*. Zipo nje ya hoja nilizowasilisha katika Baraza hili. Hivyo mambo hayo hayamo katika hotuba yangu na hakuna fungu lolote linalohusika na makadirio ya matumizi ya wizara yangu kwa maeneo hayo.

Aidha, mambo haya yameshazungumzwa sana hapa Barazani na kutolewa maelezo ya kina na sekta husika. Iwapo Waheshimiwa Wajumbe bado walikuwa na hoja ya kutaka maelezo zaidi walikuwa na nafasi hiyo ya kuhoji sekta husika wakati walipokuwa wakiwasilisha hotuba zao. Lakini vile vile

walikuwa na nafasi ya kuhoji wakati nilipowasilisha hotuba ya Serikali. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, hata hivyo kutokana na uwajibikaji wa pamoja katika serikali, nitaendelea kutoa ufafanuzi katika maeneo mbali mbali kadri ya uwezo wangu. Ninawashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri waliojibu hoja na Waheshimiwa Manaibu Mawaziri waliosaidia kujibu hoja mbali mbali za Waheshimiwa Wajumbe, na ninaamini Wajumbe wataridhika na maelezo na ufafanuzi huo uliotolewa na Waheshimiwa Mawaziri, kwa sababu maelezo yalitolewa kwa uwazi na ufasaha mkubwa.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo maneno ya utangalizi, sasa naomba kuwatambua Waheshimiwa Wajumbe waliochangia hotuba ya wizara yangu ambao wamefikia 37. Wajumbe hao ni:-

1. Mhe. Yussuf Hassan Iddi
2. Mhe. Suleiman Sarahan Said
3. Mhe. Abdalla Ali Kombo
4. Mhe. Ali Suleiman Ali
5. Mhe. Jaku Hashim Ayoub
6. Mhe. Omar Seif Abeid
7. Mhe. Mussa Foum Mussa
8. Mhe. Simai Mohammed Said
9. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy
10. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohammedali
11. Mhe. Shamata Shaame Hamad
12. Mhe. Abdalla Maulid Diwani
13. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi
14. Mhe. Hamza Hassan Juma
15. Mhe. Hassan Khamis Hafidh
16. Mhe. Shehe Hamad Mattar
17. Mhe. Said Omar Said
18. Mhe. Miraji Khamis Mussa
19. Mhe. Ali Salum Haji
20. Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali
21. Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji
22. Mhe. Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum)
23. Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira
24. Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo
25. Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na;

26.Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na mteuliwa wa Rais

Mhe. Naibu Spika, naomba pia kuwatambua. Naomba kusahihisha ni Mhe. Simai Mohammed Said.

Mhe. Naibu Spika, pia naomba kuwatambua Waheshimiwa Wajumbe waliochangia kwa maandishi kama ifuatavyo:

1.Mhe. Dk. Mwinyihaji Makame
2.Mhe. Mtumwa Peya Yussuf
3.Mhe. Asha Abdalla Mussa
4.Mhe. Mihayo Juma N'hunga
5.Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo
6.Mhe. Masoud Abrahman Masoud
7.Mhe. Bahati Khamis Kombo
8.Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto
9.Mhe. Naibu Waziri wa Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora
10.Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa
11.Mhe. Nassor Salim Al Jazira

Mhe. Naibu Spika, baada ya utangulizi huo sasa naomba kutoa maelezo kwa hoja mbali mbali zilizotolewa na Waheshimiwa Wajumbe kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Mjumbe wa kwanza ni Mhe. Suleiman Sarahan, ambaye alitaka itolewe elimu kwa walipa kodi na alieleza kwamba walipa kodi hawana elimu na hawajui umuhimu wa kodi.

Mhe. Naibu Spika, elimu kwa wananchi juu ya kulipa kodi inatolewa, inaendelea kutolewa na itaendela kutolewa, kwa vile tunajua kwamba elimu itaweza kuongeza uwajibika katika suala zima la kulipa kodi.

Pia, alizungumza suala la kwamba *ZRB* inakataa kuchukua nusu nusu ya kodi inayodai kwa wateja wake. Hili ni kweli suala hili liko hivyo na ni kwa sababu kwamba tukiamua kuchukua nusu nusu walipa kodi wasiokuwa waaminifu wanatumia mwanya huo wa kutokulipa yale malipo yaliyobakia. Kwa hivyo, kama *condition* inabidi alipe malipo yote kamili.

Huo ndio msisitizo ambao unafanyika hadi sasa ili kuhakikishwa kwamba mapato yote yanayotakiwa kukusanywa na serikali yanakusanywa kwa ukamilifu wake.

Vile vile, aliulizia kuhusiana na vifaa vichakavu vinachelewa sana kutolewa katika taasisi zetu. Pia niseme kwamba upo utaratibu wa vifaa vichakavu kuondolewa na utaratibu huo uko kwa mujibu wa sheria ya manunuzi na uondoaji wa mali za serikali.

Kwa hivyo, kwa wakati wote taasisi zinafuata utaratibu huu. Mali ambayo ni chakavu basi kwa mujibu wa sheria ile upo utaratibu wa kuziondoa katika taasisi zetu, na sheria hiyo ndio inayoongoza. Lakini kama zipo taasisi ambazo zinachelewa kufanya hivyo, basi tutahakikisha kwamba vifaa vilivyopitwa na muda viweze kuondolewa katika taasisi zetu lakini kwa kufuata utaratibu wa sheria uliopo.

Mhe. Suleiman pia alizungumza suala la madaktari waletwe hapa nchini kwa ajili ya kutibu badala ya wagonjwa kupelekwa nje. Mhe. Naibu Spika, suala hili lilizungumzwa vizuri sana na Mhe. Waziri anayehusika na sekta ya afya, na alilitolea ufafanuzi wa kina wakati alipokuwa akijibu hoja wakati alipowasilisha hotuba yake. Sababu moja alieleza kwamba bado sisi kwa upande wetu tunaendelea kujiimarisha kivifaa. Sasa wagonjwa wanapopelekwa nje baada ya kufanyiwa tathmini ya kina na bodi maalum na kuridhika, kwamba mgonjwa huyo anapaswa kwenda nje kutokana na magonjwa aliyonayo yule mgonjwa anapelekwa nje. Kule tunapata faida ya kuwepo vifaa, lakini vile vile madaktari wengi zaidi wanaweza kufanya *consultation* ili kuweza kumhudumia yule mgonjwa wetu. Lakini jitihada za serikali zinazoendelea kuchukuliwa, ni kuimarisha upatikanaji wa vifaa, kusomesha madaktari wengi zaidi, ili kuongeza uwezo wetu wa ndani wa kutibu wagonjwa wetu, na kwa yale magonjwa sugu na mazito zaidi, ndio wagonjwa wasafirishwe nje ya nchi.

Mhe. Abdalla Ali Kombo, alizungumzia suala la nyumba iliyokuwa ikitumika na viongozi huko Makunduchi, kugeuzwa kuwa Kituo cha Mafunzo ya Amali *Vocation Training*. Alituuliza mimi na Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali kama tunalijua hilo, na kima cha pesa kilichotumika na Kampuni gani ilifanya matengenezo au marekebisho ya jengo hili.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri, nakuomba utambuwe kuchangia kwa maandishi kwa Mhe. Mohammed Said Mohammed Dimwa. Anasema jina lake hakulisikia, lakini alileta kwa maandishi. Naomba utambuwe hilo.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Naibu Spika, ni kweli na naomba kumtambua Mhe. Mohammed Said Mohammed Dimwa kwamba ni mchangiaji kwa maandishi. Ni kweli karatasi ilinifika muda mchache sana kabla sijaondoka, kwa hivyo nilisahau kumuorodhesha. Namtambua mheshimiwa.

Mhe. Naibu Spika, jibu la suala la Mhe. Abdalla Ali Kombo, naomba kumjulisha kwamba suala hili tunalijua, mimi na Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali. Jengo hilo lilikuwa ni la Kamisheni ya Utalii ambalo lilirudishwa serikalini, na kuwa chini ya Wizara ya Fedha baada ya Shirika la Utalii kuvunjwa. Wizara ya Fedha na Mipango ilitoa jengo hilo kufuatia ombi la Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Makunduchi, aliyeleta serikalini la kutaka jengo hilo wapatiwe *NGO* ya Switzerland iitwayo *CAAA*. Lengo likiwa kuanzishwa kwa Kituo cha Mafunzo ya Kilimo na Utalii kwa Vijana, ili kukuza fursa za ajira kwa vijana hao.

Kwa hivyo, ni kweli jengo limetolewa na upo mkataba uliosainiwa tarehe 26 Juni, 2014, baina ya *NGO* hii na iliyokuwa Wizara ya Kazi na Utumishi wa Umma. Kwa hivyo, hilo jambo linajulikana na ni jengo ambalo lilikuwa limechakaa sana, kwa hivyo *NGO* hii ililifanyia matengenezo makubwa na makubaliano kwamba yatolewe mafunzo kwa vijana wa Makunduchi na maeneo jirani, kwa ajili ya kuweza kuwasaidia kupata ajira katika sekta ya kilimo, lakini vile vile kupata ajira katika sekta ya utalii.

Mhe. Naibu Spika, sisi tunaliona hili ni jambo jema, kwa sababu wenzetu hawa wanatusaidia kujenga uwezo wa watu wetu. Wale wanafunzi wanaosoma pale, wakimaliza wanapatiwa Diploma ya kutoka *Switzerland.* Taarifa nilizonazo ni kwamba hadi sasa kuna vijana 40 tayari wamekwishapata mafunzo haya na pia wameshasaidiwa katika masuala mazima ya kupata ajira. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Ali Suleiman Ali Shihata, alitupa ushauri wa kuongeza mapato, kuwawezesha wajasiriamali na kuzidisha usimamizi kwa uwekezaji na kuepukana na ujanja na kutotoa risiti. Vile vile alitoa ushauri juu ya *ZSSF* kushajihishwa kuwekezwa katika viwanda vya kusindika samaki. Mhe. Naibu Spika, niseme tu kwamba tunapokea ushauri wa Mhe. Ali Suleiman Ali Shihata na tutaufanyia kazi kadiri hali itakavyoturuhusu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub, yeye alizungumza suala la usalama wa fedha za wafanyakazi, zilizotumika katika ujenzi wa viwanja vya kufurahisishia watoto na *ZSSF*. Suala la *ZSSF* kuwekeza katika viwanja vya kufurahishia watoto limefanyika kibiashara, naomba kusema hivyo, baada ya kuridhika kwamba

matokeo ya tathmini iliyofanyika na kuona uwezo wa mradi huu kurudisha fedha zilizowekezwa katika kipindi kisichozidi miaka 10.

Aidha, manufaa ya viwanja hivyo kwa jamii ni makubwa sana, na mheshimiwa asiwe na wasi wasi juu ya usalama wa fedha za wafanyakazi. Lakini pia alizungumza kuhusiana na jengo la *train building*, hatima ya wamiliki waliomo ndani. Pia, alizungumzia suala la kutolewa watumiaji wa jengo hilo katika kipindi hiki cha mwezi wa Ramadhani. Niseme tu Mhe. Naibu Spika, kwamba jengo la *train building* liliopo Darajani, lilipewa *ZSSF* kwa maana ya *lease* ya mwaka 1966, tokea mwaka 2013. Lengo likiwa kuliendeleza baada ya kuonekana kwamba jengo hilo liko katika hali mbaya sana na halifai kutumika kwa makazi ya binadamu na linahatarisha usalama wa wanaokaa humo ndani, lakini pia na wapita njia.

Kwa hivyo, *concern* kubwa ya serikali ni usalama, na kwenye hili ukitizama katiba yetu kifungu cha 17 kinazungumza wazi wazi, kwamba pale linapoonekana jengo au sehemu yoyote ina uwezo wa kuhatarisha, kuna kuhatarisha usalama wa watu, Serikali lazima ichukuwe hatua, na hicho ndicho kilichofanyika. Lakini hata sheria ya kukabiliana na maafa nayo inaeleza hivyo hivyo. Kwa hivyo, suala halikuwa kuwaondosha kwa sababu ama ya kulijenga. Lakini la mwanzo hasa ilikuwa kuwaondosha kwa sababu ya usalama wa watu. Yanapotokea maafa jengo kuporomoka, au kuanguka basi inayolaumika ni serikali kwa kutochukua hatua kwa wakati muafaka.

Kwa hivyo, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe, wakubaliane na hili, Mhe. Jaku Hashim akubaliane na hili kwamba pale wananchi walitolewa kwa usalama wao na usalama wa watu wengine wanaopita katika majengo yale. Tumesikia katika nchi za jirani majumba yanavyoporomoka na kufidikiza watu na watu kupoteza maisha yao.

Mhe. Naibu Spika, nieleze kwamba tunatambua kuwa wapo wamiliki watano katika jengo lile, na wamiliki watano hawa wamefuatwa na kuzungumzwa, na utaratibu wa kulipwa fidia upo wazi, watalipwa fidia maduka baada ya lile jengo kukamilika. Lakini na maeneo yao kwa mujibu wa gharama za matengenezo, lakini na thamani iliyokuwepo kabla ya kutengenezwa jengo hilo. Kwa hivyo, hili naomba tusiwe na wasi wasi, limefanyika kwa nia njema sana.

Mhe. Naibu Spika, pia Mhe. Jaku Hashim alizungumzia kuhusu kusuasua kwa ujenzi wa ukuta wa Forodhani. Mhe. Naibu Spika, mradi wa ujenzi wa ukuta wa Forodhani umekusudia kujenga ukuta wa bahari wa mita 340, kutoka

bustani ya Forodhani hadi Mkahawa wa *Mercury*, ambao utazidishwa kwa upande wa baharini kwa kiasi cha mita tano kutoka ukuta uliopo hivi sasa. Barabara ya eneo hilo pia itakarabatiwa na kutakuwa na eneo la watembea kwa miguu na vyombo vya maringi mawili, na eneo la kupumzikia kwa upande wa baharini. Mkandarasi aliyeshinda zabuni ya kazi hii anaitwa *Seyani Brothers and Call Limited* ya Dar es Salaam, na mkataba ulisainiwa tarehe 8 April, 2015 kwa gharama ya shilingi bilioni 7.2. Muda wa kazi ulikuwa ni miezi 18, Mkandarasi alikabidhiwa kazi tarehe 22 April, 2015 na inatarajiwa kukamilika Oktoba, 2016. Hii ni tarehe iliyotarajiwa kukamilika kazi hiyo.

Kutokana na mkataba wa mradi huu bado haujamaliza siku zake, kwa maana ulitarajiwa kukamilika Oktoba, 2016. Mradi hadi sasa umetekelezwa kwa asilimia 47, na mkandarasi huyu tayari ameshalipwa shilingi bilioni 3.3, sawa na asilimia 45 ya gharama. Mhe. Naibu Spika, kutokana na changamoto mbali mbali zilizojitokeza wakati wa utekelezaji, mradi huu sasa unatarajiwa kumalizika mnamo mwezi wa Januari, 2017. Changamoto zilizojitokeza ni pamoja na mkandarasi kuchelewa kuleta vifaa vya kufanyiakazi, pamoja na wafanyakazi muhimu kwa sababu sehemu ile ni nyeti, sehemu ya bahari, sehemu ya maji inahitaji wataalamu maalum.

La pili, kuchelewa kupata majibu ya uchunguzi wa vifaa vya ujenzi, vikiwemo mchanga, saruji inayotumika pale, kuna saruji maalum ya *marine cement* inayotumika kwenye bahari, kokoto pia zinatakiwa kuchunguzwa, nondo na *concrete* zote ziende kwenye uchunguzi. Uchunguzi huu unafanywa na taasisi zenye kutambulika kimataifa, kama *TBS* au Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, hao ndio wanaoweza kufanya uchunguzi wa vifaa hivyo.

Mhe. Naibu Spika, pia uchunguzi mara nyingi sana huwa unachukua muda mrefu, kwa hivyo hiyo nayo ilisababisha kuchelewa kuendelea kwa kazi hii. Lakini pia kunyesha mvua kubwa katika kipindi cha hivi karibuni na zipo sababu nyengine zinazohusiana na kwamba wakati wa uchimbaji wa msingi, kule chini ya bahari kulijitokeza maji mengi yakawa yanakwamisha juhudi za kufanyakazi. Vile vile tusisahau marudio ya uchaguzi nayo kwa kiasi fulani yalisitisha kuendelea kwa kazi za ujenzi huo.

Mhe. Naibu Spika, kutokana na changamoto hizo sasa juhudi mbali mbali zinachukuliwa kwa madhumuni ya kupunguza ucheleweshaji huo. Juhudi hizo ni pamoja na kuongeza vitendea kazi, wafanyakazi kuwaongeza muda wa kazi na kufanyakazi wakati wa usiku na kuanza ujenzi wa upande wa pili wa ukuta, kwa maana kule kwenye Mkahawa wa *Mercury*. Kwa hivyo, tunatarajia kwamba kazi hii itakamilika mnamo mwezi wa Januari, 2017.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Omar Seif Abeid yeye alieleza haja ya bandari kupatiwa vifaa, ili kuondokana na mrundikano wa makontena. Hili pia lilielezwa na Mhe. Jaku Hashim na Mhe. Simai Mohammed, pia walitaka kujua miradi yenye manufaa ichukuliwe hatua, pia walitaka kujua lini mashine za *EFD* zitaanza kufanyakazi.

Mhe. Naibu Spika, suala la kupatikana kwa vifaa vya bandari lipo katika hatua za utekelezaji, na tuna matumaini kwamba hivi karibuni bandari itapata vifaa, ambavyo vitasaidia sana kuondosha tatizo la mrundikano wa makontena pale bandarini. Ushauri wa Mhe. Omar Seif tunauchukua wa kuhakikisha kwamba tuna- *focus* kwenye ile miradi ambayo inatija. Lakini suala hili la mashine za *EFD*, nakumbuka nililieleza kwa kina katika hotuba yangu, hotuba ya serikali na tumekusudia kununua mashine 1,000 kwa majaribio na zitatumika katika mwaka wa fedha ujao wa 2016/2017.

Mhe. Mussa Foum Mussa, yeye alizungumzia kuhusu Hoteli ya Kiweni iliopo Shamiani Mwambe na Hoteli ya Kuji iliopo Kisiwa cha Kuji Shehia ya Mtangani. Alisema kwamba maendeleo yake hayaonekani katika hoteli hizi, pia alitaka kujua iwapo *ZIPA* wanafahamu mwenendo wa hoteli hizo.

Mhe. Naibu Spika, *ZIPA* wanazielewa vizuri hoteli hizi, awali lililokuwa Shirika la Utalii la Serikali, ndilo lililotaka kuendeleza Hoteli ya Kuji kwa kuingia ubia na mwekezaji kutoka Island. Suala hili halikuwezekana kutokana na kuvunjwa kwa Shirika la Utalii. Mwekezaji huyu baadae alitaka kuliendeleza eneo hilo pekee na *ZIPA* ilimtaka ashirikiane na jamii katika uwekezaji huo. Alitakiwa kutayarisha *concept note*, lakini hadi sasa *concept note* hiyo hajaiwasilisha.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu suala la uwekezaji wa Hoteli ya Kiweni Mwambe. Hoteli hii awali ilikuwa ikimilikiwa na Kampuni ya *Pemba Resource Limited*, iliyokuwa inamilikiwa na wazalendo kwa asilimia 20, na wazalendo hawa ni vikundi vya akina mama. Kikundi kimoja ni cha Mkoani ambacho kilikuwa kinamiliki hisa ya asilimia 10 na kikundi changine cha Kiwani ambacho ni cha wanawake hivyo hivyo, kilikuwa kinamiliki hisa ya asilimia 10, na Kampuni ya Norway ilikuwa inamiliki asilimia 80.

Mhe. Naibu Spika, wazalendo hawa ambao ni vikundi vya kinamama kama nilivyosema vilishirikiana na Kampuni hii ya Norway katika kuwekeza. Mkataba wao ulikuwa unaelezea kwamba watapatiwa gawiwo la asilimia 20. Lakini pia mkataba huo ulieleza kama mradi huu utakuwa na hasara, basi

vikundi hivyo havitahusika na kufidia hasara hiyo. Tayari walikuwa wakipata shilingi 150,000 kila mwaka, lakini mradi huu ulifilisiwa na hivyo ulibadilisha umiliki wake na kwenda kwa Kampuni ya Eliwana Afrika ya Afrika ya Kusini, nayo hii ikanyang'anywa pia lies. Sasa kuna Kampuni nyengine pale inaitwa *Pemba Lodge* ambayo imepewa sehemu ya eneo lile.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Simai Mohammed Said, yeye aliulizia kuhusu barabara ya Mwanakwerekwe Fuoni. Naomba barabara hii nisiitolee maelezo, kwa sababu Mhe. Naibu Waziri anayehusika na masuala ya ujenzi, ameshaizungumza kwa kina sana. Kuhusu kiasi gani cha fedha kimepatikana kutokana na Mkataba na Zantel ya matumizi ya mkonga.

Mhe. Naibu Spika, naomba kumjulisha Mhe. Simai Mohammed Said kwamba Kampuni ya Zantel inamilikiwa na kwa pamoja, kwa sasa baina ya Kampuni ya Milcom ambayo ina *share* ya asilimia 85 na SMZ asilimia 85, na kabla ya hapo *Etisalat* ndio waliokuwa wanamilikia asilimia 85 za Milcom.

Mhe. Naibu Spika, ni kweli Kampuni ya Zantel iliingia mkataba na SMZ kwa ajili ya kutumia mkonga wa mawasiliano *Fiber Optic Light Ball* makubaliano hayo yalitiwa saini Tarehe 15 Februari, 2013 na makubaliano hayo yalihusisha kugawana matumizi ya mkonga huo, kwa maana ya *Capacity* baina ya Serikali na *ZANTEL* na matumizi ya ziada yaweze kuuzwa kwa Makampuni mengine ya Mawasiliano. Kwa hivyo ilikuwa *ZANTEL* iwe na matumizi SMZ iwe na matumizi na yale ya ziada ndio yauzwe kwa makampuni mengine.

Mgawano wa mapato yanayotokana na hayo mauzo ya ziada ilikuwa basi mgawano huo uwe kwa asilimia 70% SMZ na 30% kwa kampuni ya *ZANTEL*, kwa bahati mbaya sana kampuni ya *ZANTEL* ilipata kipindi kigumu na nadhani zote tunaelewa na ile miundombinu ambayo ilikuwa iwekezwe na kampuni hii haikuweza kuekezwa na kwa namna hiyo hawakuweza kuuza ile ziada ya matumizi ya *Capacity*. Sasa kwa kipindi chote hicho jibu ni kwamba, hatujaweza kupata mapato kutokana na kwamba mauzo ya *Capacity* hayakufanyika.

Lakini hivi sasa zipo dalili nzuri sana baada ya kuwepo mmiliki mpya wa *MILCOM* na dalili hizo zinaonyesha kwamba kwa mara ya mwanzo *ZANTEL* imeweza kupata faida, kwa hivyo tuna matarajio makubwa sana katika kipindi kifupi kijacho basi sasa mwelekeo utaelekea kule ambako tumekusudia mwanzo.

Kuhusu suala la kurundikana Makontena Bandarini, Mhe. Naibu Spika, nikubaliane na Mhe. Said kwamba kwa muda sasa kumekuwepo na tatizo la

mrundikano wa makontena hapo Bandarini, na kusababisha usumbufu mkubwa kwa wenye mali na hata kwa wale wamiliki wa meli. Suala hili linashughulikiwa kwa kutafuta eneo litakalotumika kuweka baadhi ya makontena kwa dharura na hatua muafaka zitachukuliwa kuondosha kabisa tatizo hilo, maamuzi ya kutokulitumia eneo la Bwawani na uwanja wa Malindi ni maamuzi yaliyofanywa na Serikali yenyewe na sio muwekezaji.

Pia, hapa kuna suala zima ambalo inabidi tuwanasihi wenzetu wafanya biashara kuacha kutumia bandari ile kama ni *storage* ya mizigo yao, ile mizigo ambayo inaweza kutoka basi watusaidie itoke na hasa wafanya biashara wa saruji wanaweka pale na kuchukua kidogo kidogo, nadhani wanaohusika *Zanzibar Port Authority* watalishughulikia suala hili na vifaa vinatarajiwa kuwasili, lakini vile vile kutafuta eneo la dharura la kuweka makontena hayo suala hili linashughulikiwa na naamini kwamba litapata ufumbuzi si muda mrefu kutoka sasa.

Mhe. Naibu Spika, suala la *ZIPA* kujipanga *ZRB* kutoa semina kwa wajumbe na Wajumbe kufahamishwa kuhusu *IFIN* hili tunalipokea na tutalizingatia na hatua zinazostahiki zitachukuliwa.

Suala la ujenzi wa Jengo la Abiria la Uwanja wa Ndege wa Abeid Amani Karume suala hili lilizungumzwa na Waheshimiwa wengi wakiwemo Mhe. Nadir Abdullatif , Mhe. Hamza Hassa Juma, Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi, Mhe. Mohammedraza Hassanali, Mhe. Abdalla Maulid Diwani na wengine walilizungumza suala hili kwa kina, lakini nashukuru sana Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi amelitolea ufafanuzi mzuri sana ulioongezewa na Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais, kwa hivyo sina haja ya kulieleza kwa undani sana.

Lakini niseme tu kwamba naomba ieleweke kwamba tunapozungumza *Tarminol II* ina maana hatuzungumzi lile jengo peke yake tunazungumzia eneo la *apron*, tunazungumzia pia eneo la *landside Packing*. Kwa hivyo yote kwa umoja ndio yanazungumzwa kwamba ni mradi wa *Terminol II* na mambo yote haya yanachukua fedha nyingi sana, kutengeneza *apron* ni fedha nyingi sana kuna wakati fulani tulitengeneza *parking na runway* ilichukua karibu dola milioni 58.

Kwa hivyo, uwekaji wa lami katika uwanja wa ndege ni jambo ambalo linachukua pesa nyingi sana kwa hivyo hilo lieleweke, lakini pia mradi huu kutokana na yale mapungufu aliyoyazungumza Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ilibadilisha *scope* nzima ya ule

mradi sio ile ile tuliyoanza nayo ambayo ilikuwa ya dola 70.4 milioni *Scope* imebadilika na *Scope* imebadilika kutizama kazi zinazotakiwa kufanywa ni kubwa, lile jengo lenyewe limeongezwa *size* yake ili kutoa nafasi zaidi kwa huduma za Uwanja. Lakini Vile vile na hilo eneo limeongezeka kwa zaidi ya asilimia 30, mwanzoni lilikuwa mira za mraba 15,600 zimeongezeka hadi kufikia mita za mraba 25.000 na hiyo katika kuimarisha jengo lile na kulifanya liwe jengo la kisasa.

Lakini pia eneo la *apron* nalo limeongezeka hadi kufikia mita za mraba 14,000 na *parking* huku ya nje *landside parking* nayo imeongezeka kutoka mita za Mraba 4,570 hadi elfu 7,245 nukta 4.3 kuna ongezeko za mita za mraba elfu 2,675 nukta 4.3 kwa hivyo *scope* imeongezeka, kulikuwa na *euro bridge* mbili upande wa mashariki, sasa kuna *euro bridge* nne imeelezwa hapa mbili zitakuwa kusini ya uwanja ambazo zitatua ndege kubwa kama ilivyozungumzwa na Mhe. Waziri Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Kwa hiyo, *Original Contract Sun* ni sahihi ilikuwa Dola za Kimarekani milioni 70.4 lakini *addendum one* number 0ne hii ilikuwa peke yake inachukua dola za Kimarekani milioni 11.82 na *addendum one* ya pili ilichukua dola za Kimarekani 46.518 kwa hivyo ni sahihi kwamba sasa jengo lile baada ya kufanyika hayo yote na kubadilika kwa *Scope* itakuwa inagharimu jumla ya dola za Kimarekani milioni 128.747.

Hapa ningeomba niseme kitu kimoja hadi sasa hivi fedha zilizotoka ni dola za Kimarekani milioni 35 tu, kazi ile na fedha zilizolipwa ni dola za Kimarekani milioni 35 tu, na utoaji wa fedha, hizi naomba hapa nieleze vizuri ni kwamba si kwamba *Exim Bank* wanaleta fedha hapa, fedha zinalipwa na *Exim Bank* wenyewe huko huko, baada ya kuwasilisha *Certificate of Payment*. Kwa hivyo hapa kinachopelekwa ni *Certificate of Payment, Exim Bank* wanamlipa mkandarasi au wanamlipa mshauri elekezi.

Kwa hivyo, tunapozungumza kwenda kutafuta majipu hatutaweza kuyaona hapa, kwa sababu pesa hazikuja hapa kama watu walikuwa nazo mikononi na wakaanza kuzifanyia mchezo huo unaofikiriwa kuchezwa. Lakini mapungufu yote haya niseme ni Serikali yenyewe ndio iliyoyaweka wazi na baada ya kuona kwamba jengo ambalo lilikuwemo katika ile o*riginal design* lisingekuwa na tija kwa nchi yetu. Kwa hivyo hali ya mambo yanayojulikana naomba sana Waheshimiwa wajumbe waridhike na maelezo hayo.

Hivi karibuni mimi mwenyewe nilifanya mazungumzo na ujumbe kutoka *Exim Bank* na wako tayari kuendelea kutusaidia kwa maana kutoa mkopo katika kima kinachofikia dola za Kimarekani milioni 27. Lakini kulikuwa na *Condition* ya malipo ya riba pamoja na malipo ya *Commitment* ambayo yote haya yanatakiwa kulipwa na SMT, kwa sababu SMT ndio mkopaji kwenye mradi, *borrower* ni SMT, taarifa niliyonayo kwamba fedha hizo tayari zimeshalipwa na tunafanya mawasiliano hivi karibuni ili kuona kwamba hizo dola za kimarekani milioni 27 zinaingia ili shughuli za ujenzi zinaweza kuendelea.

Mhe. Naibu Spika, kulikuwa na suala la wawekezaji kukutana na *ZIPA* kuwalea wawekezaji wa ndani niseme hili ni jambo ambalo tunalifanyia kazi ni jambo zuri na sisi tutaendelea kukutana nao, ni wenzetu ni *partner* katika maendeleo yetu, kwa hivyo hilo ni shauri zuri na tunalichukua.

Suala la kuwa na uhakika wa kupata umeme utakaokidhi mahitaji kutokana na kuongezeka kwa wawekezaji na hasa Mhe. Simai alizungumzia suala la mji mpya wa Fumba, bandari na *airport* ni kweli Serikali inalitambua hili na ndio maana sasa hivi kunaendelea utafiti wa kutafuta nishati mbadala inayotokana na nguvu za jua, mawimbi ya bahari, upepo, taka taka. Kazi hiyo inafanywa na *European Union* ndio wanaofanya *study* hiyo, mara baada ya kumalizika *study* hiyo basi tutawasilisha Serikalini na hatua zinazostahiki kwa mujibu wa mapendekezo yatakayotoka basi yatafanyiwa kazi.

Mhe. Naibu Spika, pia lilikuwepo suala la deni la taifa linawekwa wapi na kwa sarafu gani ikiwa ni shilingi ni kwa nini tunaweka kwa shilingi. Mhe. Naibu Spika, sijui kama nimelifahamu vizuri suala hili lakini naomba nilijibu kama ifutavyo.

Naomba kumjulisha Mhe. Simai Mohammed Said kwamba hatuna *account* ya madeni na utaratibu ni kwamba tunapokopa huwa tunakopa kwa jambo fulani na matumizi yanafanywa kama nilivyosema pale mwanzo yanafanywa moja kwa moja na wale wanaotukopesha, ikiwa tumekopa kutoka Benki ya Dunia, wao ndio wanaofanya *Direct Payment* ikiwa *ADB* hivyo hivyo, ikiwa *BADEA* hao ndio wanaofanya malipo moja kwa moja. Kwa hivyo sisi huwa hatuna *account* ya madeni.

Kuhusiana na *Currency* ipi inategemeana na mkopo unatoka wapi, tunaweza kukopa kwa Dola za Kimarekani, tunaweza kukopa kwa Pound, Japanese Yen, tunaweza kukopa hata kwa China RMB, kwa hivyo *Currency* ni hiyo. Lakini tunapotoa ripoti zetu tunatoa ripoti kwa shilingi ya Tanzania baada ya kuifanyia

conversion kutegemeana na *exchange rate* ya wakati huo. Kwa hivyo hiyo ndio hali halisi na hayo ndio majibu ambayo naweza kumpatia Mhe. Simai kwa wakati huu.

Sheria ya Manunuzi ina kasoro ni kweli tumezibaini na tayari sheria hii imeshafanyiwa marekebisho na iko katika hatua ya kupelekwa kwa Kamati ya Makatibu Wakuu kwa ajili ya kupitia ule mchakato wa kwenda Serikalini, na kuweza kuletwa hapa Baraza kwa hatua zinazostahiki.

Suala la *AGAPE,* naomba hili nisilieleze limetolewa ufafanuzi mzuri sana na Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo kwa hivyo sioni haja naomba Wajumbe watakuwa wameridhika sana na majibu ya Mhe. Waziri.

Mhe. Nadir Abdullatif alizungumzia kuhusiana na *Terminal II Building na AGAPE* na barabara ya Mwanakwerekwe ambayo yote yameshatolewa maelezo.

Mhe. Mohammedraza pia alizungumzia *Terminal II Building na AGAPE* nalo limeshatolewa maelezo ya kina na suala la *OIC* la Mhe. Mohammedraza limezungumzwa vizuri sana na Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, ni suala ambalo kama tutapitisha katiba inayopendekezwa, basi Zanzibar nayo itakuwa na fursa hiyo ya kujiunga na hizi jumuiya mbali mbali za Kimataifa.

Suala la mgao wa madawati ya BOT pia lilizungumzwa na Mhe. Abdalla Maulid Diwani tuseme tu kwamba BOT imetenga jumla ya Shs. bilioni nne (4) kwa ajili ya madawati, na tayari bilioni mbili (2) zimeshatengwa kwa ajili ya matumizi ya Mikoa sita na Zanzibar ikiwemo, kwamba Zanzibar itakuwa ya saba. Na bilioni mbili hizi wamezipeleka kwenye maeneo ambayo.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri naomba kidogo ukae nataka kuwakaribisha wageni halfu baadae utaendelea. Waheshimiwa Wajumbe naomba tutambue uwepo wa wageni ambao ni Wajumbe wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi NEC.Wajumbe hao ni:

1. Mhe. Jaji Darmian Z. Lubuva ambae ni Mwenyekiti.
2. Mhe. Jaji Mkuu Mstaafu wa Zanzibar
   Mhe. Hamid Mahmoud Naibu Mwenyekiti
3. Mhe. Jaji Mstaafu Mery H. C. S. Loguway Mjumbe
4. Mhe. Jaji Mstaafu John Mkwaza Mjumbe
5. Mhe. Prof. Amon Chaligha Mjumbe

6.	Mhe. Mchanga Mjaka	Mjumbe
7.	Mhe. Hasina A. Omar	Mjumbe
8.	Ndg. Kairima Ramadhan	Mkurugenzi wa Uchaguzi
9.	Ndg. Clemence Nanyaro	Afisa wa Habari

Waheshimiwa Wageni wetu tunawakaribisha sana sana na ni fahari yetu kuwa nanyi leo hapa kwa siku ya leo karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe pia tuna wageni wa Mhe. Rashid Ali Juma Muwakilishi wa Amani pia Waziri wa Utalii, Habari, Utamaduni na Michezo na ni Wachezaji wa timu ya mpira wa miguu chini ya umri wa miaka 20 kutoka Wilaya ya Mjini, naomba msimame msalimie Waheshimiwa. Ahsanteni sana, na hawa leo wanaondoka kuelekea Arusha kwa ajili ya mashindano ya Rolling Stone *(Makofi).*

Kwa hivyo, tunatakutakieni kila la kheri katika mashindano haya karibuni sana mnaweza kukaa*(Makofi)*

Mhe. Waziri tunaendelea.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Suala la mgao wa madawati ya *BOT* kama nilivyoeleza ni kwamba *BoT* ilitenga Shilingi bilioni 4 kwa ajili ya madawati nchi nzima, tayari bilioni mbili zimetengwa kwa ajili ya Mikoa saba ikiwemo Zanzibar na ilitengwa kwa kutolewa kwenye maeneo ambayo *BOT* ina *branch* zake. Kwa hivyo Mkoa wa mwanzo ni Mkoa wa Dar-es-Salaam ambao ndio *Head Office*, lakini pia Mkoa wa Arusha, Dodoma, Mbeya, Mwanza, Mtwara na hapa Zanzibar.

Kwa hivyo, bilioni mbili zitagawanywa katika maeneo hayo. Mgao halisi utakavyokuwa bado tunafuatilia taarifa hiyo bado hatujaipata.

Bilioni mbili nyengine zilizobakia zimeachiwa Serikali yenyewe kufanya maamuzi na itafanya maamuzi kutegemeana na hali ya mahitaji katika maeneo hayo, kwa hivyo nako hapo hatujajua Zanzibar katika maeneo yepi yataweza kunufaika na hizo bilioni mbili ambazo zimeachiwa Serikali yenyewe kufanya maamuzi.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Shamata Shaame Hamad alizungumza kuhusu suala la kuimarisha mapato kupitia *ZRB* na Mawizara na pia aliweka msisitizo mkubwa sana wa kujenga barabara katika eneo la Micheweni, Mhe. Naibu Spika, ushauri wa Mhe. Shamata tunaupokea hasa katika suala zima la kuimarisha

mapato kupitia bodi ya *ZRB*, lakini vile vile na *TRA* na mapato ya Mawizara, nadhani nilivyowasilisha bajeti ya Serikali mliona mkazo ambao tumeuweka kwa kuimarisha mapato katika mwaka wa 2016/2017.

Kwa hivyo, kazi hiyo ipo pale pale na tunakusudia kuchukua juhudi kubwa sana kuhakikisha mapato yanaimarika katika mwaka wa fedha ujao.

Suala la ujenzi wa barabara nadhani sekta inayohusika imeshasikia kilio cha watu wa Micheweni na italifanyia kazi, lakini niseme tu kwamba Micheweni katika mradi wa *Millennium Village* ulipata fursa ya kipekee na kuna huduma ya barabara iliyopelekwa katika eneo hilo, lakini maendeleo hayatoshi ni lazima wadai maendeleo zaidi na kwa namna hiyo Wizara inayohusika imeshalisikia na italifanyia kazi suala hili.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani alizungumzia kuhusiana na suala zima la ukadiriaji wa kodi kwa bidhaa za *TRA* na kwamba *TRA* huwa inafanya upendeleo kwa kuangalia mtu na kutoza kodi kutegemeana na mtu huyo nafikiri hilo kama nimelifahamu ndivyo alivyolikusudia; niseme kwamba hili nalichukua tutakaa pamoja na wewe tutapata maelezo yako zaidi na tutalifuatilia na hatua muafaka zitachukuliwa iwapo kutakuwepo na dosari kama hizo.

Pia, alizungumzia kuhusiana na fedha za *ZSSF* kwamba hazitolewi mpaka mtu atimie umri wa miaka sitini na hili lilizungumzwa pia na Mhe. Shehe Hamad Matar.

Mhe. Naibu Spika, suala hili ni kweli na hii ni kwa mujibu wa Sheria ya *ZSSF* yenyewe, naomba tu ieleweke kwamba *ZSSF* ni *pension scheme* na sio *provident fund*. *Pension scheme* mafao hutolewa pale anapofikia umri wa kustaafu ndio mafao yake anapoyapata. *Provident fund* anaweza akayapata wakati wowote ule. Kwa sheria yetu hiyo ndio inayoielekeza *ZSSF* kufanya hivyo.

Lakini pia niseme kwamba inapotokea mahitaji maalum na kama mfanyakazi labda amepata maradhi ambayo sasa hatoweza tena kufanya kazi katika kipindi chake chote cha uhai uliobakia basi upo utaratibu wa mtu huyo kupata fedha zake. Lakini kwa wengine kwa sababu wanazo fursa za kupata ajira katika maeneo mengine na kwa sababu suala hili limewekwa maalum kusaidia kuondoa makali ya umaskini pale watu wanapostaafu basi naomba Waheshimiwa Wajumbe, wakubaliane na hili na kwamba ni suala la kisheria na

hatuna njia ya kulifanya lakini wananchi waeleweshwe kuhusiana na mfuko huu.

Lakini pia Mhe. Abdalla Maulid Diwani, alizungumza kuhusiana na kuku wa *perdue* na alieleza kwamba wanadhoofisha wafugaji wadogo wadogo. Mhe. Naibu Spika, suala hili tunahitaji kuliangalia kwa makini sana, kinachotokea hivi sasa ni kwamba uzalishaji wetu wa kuku wa ndani ni wa kiwango cha chini sana kukidhi mahitaji. Lakini vile vile suala la gharama za uzalishaji ni kubwa, chakula ni ghali, madawa ni ghali, kwa hivyo, gharama zetu pia ni kubwa. Kwa hivyo, kuingiza kuku wa *perdue* kutokana na upungufu huo kunawasaidia walaji. Lakini kwa upande mwengine soko la wazalishaji wa ndani linakabiliwa na ushindani na hivyo kuwaumiza wafugaji wetu.

Tayari wizara inayohusika na ufugaji imeshakaa na wawekezaji wanaoleta kuku wa *perdue* na tayari wawekezaji hawa wameonesha nia ya kuanzisha kiwanda cha kusarifu kuku hapa nchini ambacho kitaweza kutoa fursa ya ajira lakini pia kitaweza kutoa soko kwa wafugaji wetu. Lakini bado wizara ambayo tutakaa pamoja tutashirikiana nao ili kuona hatua gani zaidi tunaweza tukazichukua ili kuwasaidia wafugaji wetu wadogo wadogo waweze nao kuingia katika soko la ndani ya Zanzibar, lakini pia watupie hatua ya kuweza kuingia hata katika soko nje ya Zanzibar.

Hilo tutalifanyia kazi na zipo mbinu nyingi ikiwemo, kutoa taaluma kwa wafugaji wetu juu ya kutengeneza chakula kuna *homemade ration* ambazo wanaweza kuzitengeneza, malighafi zote zipo madagaa yapo, pumba zinapatikana. Kwa hivyo, wao wenyewe wanaweza kutengeneza *home made ration* na wakapunguza gharama ya chakula na wakaongeza uwezo wao wa ushindani katika soko.

Mhe. Naibu Spika, shamba la mipira la Kichwele na Kitope, suala hili pia liligusiwa na Mhe. Asha Abdalla Mussa wa Kitope, ni kweli mashamba haya yalikodishwa kwa kampuni ya *Agrotex* na ni kweli karibu miaka 4 sasa kampuni hii imeshindwa kuyaendesha mashamba haya na ni kweli Kampuni hii ina madeni mengi, ina madeni ya wafanyakazi, lakini pia inadaiwa na *PBZ*, inadaiwa na *ZSSF*, lakini sisi serikali tunawadai jumla ya dola za Kimarekani laki nne kutokana na kodi ya miaka minne. Kila mwaka ni kodi ya dola laki moja, kwa hivyo, wana madeni mengi.

Kwa hivyo, tunawaomba walioathirika hasa wananchi wazidi kustahamili wakati serikali inaendelea kulifatilia suala hili. Mwenye dhima ya kulipa deni hili ni muekezaji mwenyewe *Agrotex*, yeye ndio mwenye dhima ya kutulipa

sisi serikali, kulipa *ZSSF*, kulipa deni la *PBZ*, lakini pia na kulipa wananchi. Kwa hivyo, tutalifatilia kuona muekezaji huyu analipa madeni yake kwa haraka iwezekanavyo.

Pia, lilizungumzwa suala la tofauti baina ya Bodi ya Rufaa na Mahakama ya Rufaa, Mhe. Naibu Spika, niseme hivi vyote ni vyombo vya Mahakama ambavyo vimeanzishwa kusikiliza rufaa za kodi. Bodi ya Rufaa husikiliza malalamiko ya wafanyabiashara na huwa wanamlalamikia Kamishna ama wa *ZRB* au Kamishna wa *TRA* na anaeongoza bodi hii ni Hakimu. Lakini kwa upande mwengine kuna Mahakama kwa maana ya *Tribunal* ambayo sasa inasikiliza wote; inamsikiliza Kamishna wa Kodi, lakini pia inasikiliza malalamiko ya wale wafanyabiashara, nayo hii inaongozwa na Jaji ambaye anateuliwa na Jaji Mkuu.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Hamza Hassan Juma, alitaka kujua kuhusiana na mapato ya *TRA* kama yamepatikana na niseme tu kwamba ni hivi juzi zimeingizwa zile pesa nilizosema bilioni 12.5, kwa hivyo, tayari zimeingizwa na tunashukuru sana Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutuingizia fedha hizi, lakini pia tunafuatilia kuona ile bakaa nayo pia inapatikana, kwa hivyo, hizi fedha tayari zimepatikana. Barabara ya meli tano hadi Denjani na kuongeza kilomita hadi Mzambarau Takao, nadhani hii ilitolewa ufafanuzi na Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, kwa hivyo, naomba myakubali maelezo yaliyotolewa kwamba ni maelezo sahihi yanayotoka serikalini.

Mhe. Naibu Spika, kuhusiana na misamaha ya madeni na kiasi gani kimesamehewa, suala hili ni la jumla sana, pamoja na kwamba tulikuwa na siku mbili, lakini sasa kutokana na ujumla wake kwa sababu haiku-s*pecify* ni madeni ya sekta ipi na madeni yako mengi sana. Kwa hivyo, tunaomba Mheshimiwa, atukubalie kwamba atupe muda kidogo tulifanyie kazi hili na tutamjulisha, tutampatia maelezo na takwimu zinazohusika kwa maandishi.

Mradi wa chelezo uliotaka kufanywa na Mzanzibari umefikiwa wapi. Mhe. Spika, naomba kumjulisha Mhe. Mjumbe, kwamba mradi huu bado haujapitishwa na *ZIPA* na hivyo haujapatiwa kibali hadi sasa. Tatizo ni kwamba mradi huu ulipaswa kuwepo katika eneo la *industry sector* na unapoombewa ni eneo la utalii kwa maana ya *tourist zone*. Sasa kupewa kibali katika eneo hilo ama waziri anayehusika na masuala ya ardhi abadilishe matumizi ya eneo hilo ambalo litakuwa ni tatizo kubwa kwa sababu maamuzi ya kulitumia eneo hilo kama ni eneo la utalii yameshafanywa.

Sasa hizi ni taratibu na mipango tuliyojiwekea sisi wenyewe na imewekwa mipango hii kwa ajili ya kujenga nidhamu katika uwekezaji, hatuwezi tukaekeza kila mahala na kila mtu anavyotaka sehemu ya utalii tukawa na viwanda, sehemu ya viwanda kukawa na utalii, hilo ni suala ambalo ni nidhamu ya uwekezaji la limewekea utaratibu huo kwamba tuna *tourist zone* na tuna sehemu nyengine ya uwekezaji kwa maana *special economic zone*, haya yote yamewekwa maalum kwa sababu hiyo.

Lakini pamoja na hilo ni kwamba watu wanaohusika na mazingira wenyewe wamesema kwamba mradi huo haufai kuwepo hapo eneo linaloombewa. Kwa hivyo, hiyo ndio taarifa ya watu wa mazingira na kama taarifa ndio hizo basi *ZIPA* hawatoweza kutoa kibali kwa mwekezaji huyu. Lakini tuseme tu muekezaji huyu tayari ameshapatiwa kibali kwa mradi wake mwengine katika eneo lililokaribiana na sehemu ile. Kwa hivyo, si suala la kwamba tunamu-*attack* muekezaji Mzanzibari ambaye ni muekezaji mzalendo, lakini ni suala la utaratibu pale alipoomba katika eneo stahiki kibali chake tayari ameshapatiwa.

Kuhusiana na muekezaji wa *Pemiroyal* kwamba hajalipa fidia kwa wananchi wa maeneo ya Nungwi, naomba niseme Mhe. Naibu Spika, kwamba mimi mwenyewe bahati nzuri nilipata nafasi ya kulitembelea eneo la Nungwi na nilitembelea katika maeneo yote, eneo lile la hekta 411 ambazo tayari muekezaji ameshapewa kibali katika eneo hilo, lakini muekezaji huyo anadai ziada sasa ya hekta karibu 225 ili atimize hekta 640. Kwa hivyo, hilo ni eneo la ziada, lakini pia ameonesha dhamira ya kuomba hekta elfu na thamanini elfu katika eneo hilo hilo. Lakini ninachosema kwamba serikali imempa eneo la hekta mia nne kumi na moja na katika eneo hili taarifa nilizonazo kwamba tayari ameshalipa fidia wananchi wa hapo, yapo matatizo madogo sana yanayowahusu wananchi wenyewe lakini sio muekezaji. Pia, muekezaji huyu mimi nimezungumza nae na amesema kwamba iwapo atatokea mtu mwenye *genuine claim* katika eneo la hekta mia nne kumi na moja basi yuko tayari kulipa fidia hiyo.

Fidia kwa maeneo ya Fumba Mhe. Naibu Spika, fidia kwa wananchi wa maeneo ya uwekezaji Fumba yaliyokwisha kubalika tayari yamelipwa, eneo lililobakia ni eneo lililobadilishwa barabara. Kuna sehemu imebadilishwa barabara ambayo wananchi wake wanastahiki kulipwa lakini pia kuna sehemu ambayo imefanyiwa tathmini hivi karibuni. Tumepata taarifa kwamba muekezaji tayari ametenga jumla ya shilingi milioni mia saba kwa ajili ya kulipa fidia hiyo na matayarisho yapo karibu yatakamilika kulipwa fidia hizo wananchi wanaohusika hivi karibuni.

Mhe. Spika, kuhusu *PBZ* kukataa kukopesha Shirika la Bandari. Mhe. Spika, niseme tu kwamba Sheria ya Benki Kuu inaweka ukomo kwa benki za kibiashara kukopesha kwa mkopaji mmoja, kwa maana *single borrower* wa ndani ana kima ambacho Benki ya Biashara inaweza kumkopesha na kima hicho kisizidi asilimia kumi ya mtaji wa Benki inayohusika. Kwa hivyo, 10% ya mtaji wa benki ndicho kima ambacho anaweza kumkopesha mkopeshaji mmoja *single borrower*. Sasa Shirika la Bandari ombi lake lilikuwa ni zaidi ya mara mbili ya kile kima ambacho kinaruhusika na benki kuu. Kutokana na sababu hiyo *PBZ* ilishindwa kuwakopesha lakini pia ilisaidia kuunganisha Shirika la Bandari na *ZSSF* na mkopo huo wamepatiwa na *ZSSF*. Kwa hivyo, nadhani hapa kwenye hili halina tatizo lolote, lakini tatizo la kisheria kwa mujibu taratibu za Benki Kuu na ukomo huo ndio ulisababisha *PBZ* ishindwe kutoa mkopo huo.

Suala la *ZUSP* kulipa fidia kwa wananchi watakaoathirika na maradi wa ujenzi wa misingi ya maji ya mvua, hili nililisema wakati nilipowasilisha Bajeti ya Serikali na msimamo uko vile vile, kwamba hivi karibuni wakati ule nilisema tunatarajia pengine ndani ya mwezi wa Julai, fidia hii itatolewa kwa wale watakaohusika na ujenzi huo.

Kuna malipo ya madeni hasa ya walimu lakini na wastaafu kwa ujumla. Suala la madeni ya walimu tayari tumekubaliana na Waziri anayehusika na Wizara ya Elimu kukaa pamoja na kulifanyia kazi suala hili. Lakini taarifa nilizonazo kwamba Wizara tayari imeshaanza kulipa madeni ya walimu hasa yale madeni ya likizo zao, tumeshaana kutokana na *OC* zao.

Lakini tumekubaliana mara baada ya bajeti hii tukae pamoja sasa tutizame utaratibu gani tutautumia kuhakikisha madeni yote haya tunayalipa katika mwaka wa fedha huu. Na hili nililisema katika Hotuba ya Bajeti ya Serikali kwamba, moja ya kipaumbele ni kulipa mafao ya wastaafu, lakini vile vile kulipa madeni ya walimu ikiwemo na fedha zao za likizo, hilo tulishalitolea ufafanuzi mzuri. Lakini niseme tu katika madeni ya wastaafu katika miezi miwili hii tayari tumeshalipa bilioni nne katika miezi miwili hii na hii leo tutaingiza bilioni 5.4 kwa ajili ya kulipwa wastaafu hawa, lakini pia tutalipa katika kipindi cha karibuni sana bilioni 1.1 kuwalipa wale maofisa wa Usalama wa Taifa waliostaafu.

Kwa hivyo, tutakuwa tumelipa jumla ya bilioni 12.5 na matarajio yetu kufanya vizuri zaidi kuhakikisha tunamaliza madeni haya ili yasizidi kuwaletea usumbufu wananchi wetu. Kwa hivyo, huo ndio msimamo wa serikali na hizo

ndizo juhudi za serikali za kuhakikisha kwamba wananchi wetu wanapata mafao yao stahiki.

Mhe. Naibu Spika, kuhusiana na kauli ya Waziri wa Fedha wa SMT ya kutaka Taasisi za Umma kukata Bima zao kwa Shirika la Bima la Taifa, suala hili Mhe. Waziri wa Fedha wa SMT tayari ametoa tamko la ufafanuzi kupitia televisheni ya *TBC* na kusema kwamba mashirika ya Bima ya Serikali ni Shirika la Bima la Zanzibar pamoja na Shirika la Bima la Taifa. Na ma-*agency* wote sasa hivi wanayo taarifa hii na wametoa pongezi kubwa sana kwa juhudi iliyochukuliwa, kwa hivyo, tatizo sasa hili halipo.

Suala la Mkataba wa *DP* Shapriya hili limetolewa maelezo mazuri sana ninamshukuru Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kwa maelezo yake.

TRA ni chombo cha muungano kwa nini hadi leo Zanzibar kuna Naibu Kamishna. Hoja ya Mhe. Mjumbe, tumeisikia na mimi mwenyewe ninaikubali niseme hivyo na tutaifatilia katika vyombo husika kuona hadhi inayostahiki ya *TRA* Zanzibar inapatikana kwa mujibu wa sheria za nchi na taratibu.

Lakini pia Mhe. Hamza, aliuliza kwa nini katika kipindi chote Zanzibar haijapata kutoa Gavana wa *BoT*. Suala la uteuzi wa Gavana ni mamlaka ya Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na mamlaka hayo yapo kwa mujibu wa Katiba.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh, aliuliza suala la mfuko wa wafanyakazi kwamba wafanyakazi wanakatwa lakini fedha haziwafikii wafanyakazi hao. Naomba niseme kwamba suala hili ninalichukua, maana yake nimelisikia hapa na nitalifatilia kujua ukweli wake na hatua stahiki tutazichukua iwapo kutawepo na ujanja wowote katika fedha hizi. Lakini suala lake la *Terminal II* na *AGAPE* limeshatolewa ufafanuzi wa kina, lakini pia alisema iundwe taasisi nyengine itakayosaidia kukusanya mapato *ZRB*, hili nalo tunalichukua na tutalifanyia kazi kwa kadri hali itakavyokua, ni wazo zuri tunalichukua tatalitafakari kwa kina kuona faida itakayotokana na kuwa na taasisi hiyo nyengine na ikionekana faida ipo sisi haja yetu kupata faida, kama faida ipo basi wazo hili tutalifanyia kazi.

Bima kwa wanaogongwa na daladala Mhe. Spika, niseme tu kwamba Bima ya *third party* inahusisha watakaopata ajali ama wakiwa abiria ama wanaokwenda kwa miguu pamoja na uharibufu unaotokea wa mali. Malipo hayo yanalipwa kwa mujibu wa utaratibu uliopo. Kwa hivyo, mara baada ya kutokea tokeo hilo

tathmini inafanywa ili kujua kwamba huyo aliyepatwa na tatizo hilo anastahiki kulipwa fidia ama la. Lakini *third party* ina-*covers* wote hawa watembea kwa miguu, walio abiria lakini pia na mali iliyohusika.

Jengo la Wizara ya Fedha Pemba, je, mkandarasi atarudisha fedha suala hili pia liliulizwa na Mhe. Shehe Hamad Matar, aliliuliza pia suala hili. Mhe. Naibu Spika, mara baada ya kuonekana mkandarasi ameshindwa kuendeleza ujenzi, wizara ililifikisha suala hili kwa msuluhishi *arbitrator* kwa mujibu wa mkataba. Msuluhishi alitoa maamuzi ya mkandarasi tarehe 23 *April*, 2014 kulipa gharama zote za ujenzi huo na kulipomoa jengo hilo kwa gharama zake. Mkandarasi alikata rufaa Mahakama Kuu kupinga uamuzi wa msuluhishi ila shauri hili lilitupiliwa mbali kutokana na mkandarasi kunakili vifungu visivyokuwa halali.

Hivi sasa wizara imo katika hatua za kukaza hukumu kwa maana ya *drol-order* na hata hivyo tuna changamoto ya kwamba mkandarasi huyu hana *asset* yoyote hapa Zanzibar na wala hatujui *asset* yake kwa upande wa Tanzania Bara na hivi sasa anaishi Mombasa, tunamfuatilia huko aliko kupitia Ofisi yetu ya Ubalozi na Mahakama Kuu ya Kenya. Kwa hivyo, suala hili halijala bado linafatiliwa tunatumia taratibu za kisheria ili kuhakikisha kwamba haki ya serikali yetu, haki ya wananchi wa Zanzibar inapatikana kutokana na mkandarasi huyu kutofanya kazi yake kwa umakini.

Mhe. Naibu Spika, deni la shilingi milioni 600 inayodaiwa Wizara ya Fedha na Mipango na Chuo cha Usimamizi wa Fedha, ni kweli deni hili tunalifahamu, tayari tunafanya jitihada za kulipa deni hilo kama tunavyofanya jitihada kulipa yale madeni mengine.

Mhe. Shehe Hamad Matar, jengo la Wizara ya Katiba na Sheria limefikia wapi. Mhe. Naibu Spika, jengo hili limemalizika, jambo lililokuwa limebakia ni marekebisho ya umeme, ambayo marekebisho haya yalikuwa yanafanya pia ile *lift* isiweze kufanya kazi vizuri, lakini pia na ma-*air condition* katika lile jengo zisifanye vizuri. Lakini hivi karibuni mkandarasi huyu ambaye ni *CRGE* amelipwa ile *certificate* yake ya mwisho.

Kwa hivyo, *last payment certificate* imeshalipwa na nadhani karibuni kama hajaanza basi atakuja kurekebisha hali hiyo ili suala la *lift* liweze kufanyakazi vizuri, *air condition* ziweze kufanya kazi vizuri na atabakiwa na malipo yake ya mwisho ambayo yamezuiliwa kwa mujibu wa mkataba *retension* ili tumalize kipindi chote cha *default liability period*.

Washika fedha nao wawe wanahamishwa kama wahasibu, wazo tunalipokea na tutalifanyia kazi, mafunzo ya uhasibu na wakaguzi wa Pemba, alitaka kujua ni wangapi wamepata mafunzo hayo. Mafunzo kwa wahasibu na wakaguzi wa Pemba yametolewa kwa wahasibu na wakaguzi 35.

Pia, Mhe. Naibu Spika, Mhe. Shehe, alitaka kujua mishahara ya wafanyakazi wa mashirika ya umma na wafanyakazi wa serikali ni tofauti. Hili lilitolewa ufafanuzi sana na Mheshimiwa anayeshughulikia masuala ya Utumishi wa Umma Sheria na Katiba alilitolea ufafanuzi mzuri alisema kwamba huko nyuma mashirika haya yalikuwa yakijipangia wenyewe mishahara yao. Suala hili sasa linarekebishwa na serikali, kuna udhibiti, kwa hiyo, wa tofauti iliyokuwa imejitokeza tunajaribu katika serikali kuiondoa taratibu ili kuondosha hii tofauti kubwa iliyopo baina ya wafanyakazi wa mashirika na wafanyakazi wa serikali.

Katika Shirika la Bima kuna fedha za maendeleo, je, ni maendeleo gani hayo Mhe. Shehe, alitaka kujua.

Mhe. Naibu Spika, fedha hizo ni kwa ajili ya ujenzi wa ofisi Pemba ambayo itachukua karibu milioni 500,000,000 lakini pia wanataka kulifanyia matengenezo jengo liliopo karibu na Ubalozi wa Misri, ndio watachukua karibu shilingi milioni 100,000,000, wanataka kununua gari kwa ofisi ya Dar-es-Salaam na ununuzi wa *software* za kufanyia kazi lakini na vifaa mbali mbali ikiwemo *generator*. Kwa hiyo, fedha hizo zimetengwa kwa ajili hiyo.

Ulipaji wa madeni ya wastaafu hili nimeshalieleza na jitihada mmeshaziona kwamba, kabla hata kuanza mwaka wa fedha 2016/2017 basi serikali imeshachukua juhudi kubwa sana ya kulitatua tatizo hilo.

Pia, kulikuwa na maelezo ya Mhe. Miraji Khamis Mussa, hoteli ngapi zilihaulishwa katika kipindi cha 2014/2016. Mhe. Waziri, anayehusika na Wizara ya Ardhi amelitolea ufafanuzi mzuri sana na kwa kina, naomba tuchukue maelezo yale kama ndio maelezo tuliyotoa kujibu hoja iliyowasilishwa hapa.

Kodi za *ATM* zilizopo katika nyumba za watu binafsi, hili lilizungumzwa na Mhe. Miraji, kodi inalipwa na wakodishaji nyumba hizo, kwa maana *tax on rental income*. Kwa hivyo, hii inakusanywa na *ZRB*, hakuna matatizo, wote wanajuulikana, wote wako kwenye orodha na kodi yao inalipwa kawaida.

Madeni ya wanafunzi wanaosoma *Zanzibar University*. Ni kwamba tumeshazungumza na chuo kuhusiana na madeni haya tutakutana naye na tutaweka utaratibu mzuri wa kulisawazisha deni hili kama tunavyosawazisha madeni mengine kwa kadri hali yetu itakavyoruhusu.

Je, ni kweli *ZIFA* inataka kuunganishwa na *SUZA*. Jibu ni kweli, hayo ndio maamuzi ya serikali, maamuzi haya yalifikiwa kutokana na mapendekezo ya kamati iliyoundwa na Mhe. Rais, kuangalia suala hili la uwezekano wa kuunganisha taasisi mbali na Chuo chetu Kikuu cha Taifa (*Zanzibar State University*) na lengo lake ni kukijengea uwezo chuo chetu lakini pia kuvisaidia hivi vyuo kutoa elimu bora lakini pia vyeti vyao kuwa na hadhi inayotambulika zaidi.

Fedha za Gombani ilisemwa hapa kwamba zimeliwa. Mhe. Waziri wa Habari tayari ameshalitoa ufafanuzi.

Fedha za Bodi ya Wakandarasi nayo imetolewa ufafanuzi. Mhe. Ali Salum, alisema kwamba wafanyakazi wa kada ya uhasibu wawe wanabadilisha. Tayari nimeshalisema kwamba tunalichukua na tutalifanyia kazi.

Wafanyakazi wa *ZRB* kupanga na wenye mahoteli nalo hili tutalifuatilia. Moja ya kazi ambazo nimekusudia kuzifanya kwa karibu zaidi na viongozi wenzangu katika wizara ni kuhakikisha kwamba hili tunalifuatilia na kama yapo mambo haya basi tunayakomesha kwa muda mfupi sana.

Wizara kusomesha wafanyakazi wao badala ya kupeleka katika Mfuko wa Elimu ya Juu na kusababisha kwamba fedha hizo kutokulipwa katika ule mfumo wa mzunguko.

Mhe. Spika, naomba kumjuilisha Mhe. Mjumbe, kwamba mfuko ulianzishwa kwa madhumuni ya kuwapatia mikopo vijana wa *undergraduate* na sio ambao wameajiriwa. Wale wa *undergraduate* na ambao hawajaajiriwa ndio walikuwa wasaidiwe na mfuko huo, na kwamba mkopo huo warudishe pale ambapo watakuwa wamepata ajira zao. Hivyo, wizara zinazosomesha wafanyakazi wao ndivyo hasa inavyotakiwa, na naziomba wizara zote ziendelee na juhudi hiyo wasomeshe kwa mujibu wa matakwa ya wizara zao. Zile *fields* zinazotakiwa na wizara zao wasaidie kuwasomesha na kupunguza mzigo katika mfuko huu ambao umekusudiwa kusomesha wale vijana ambao bado hawajapata fursa za ajira.

Kuingiziwa mfanyakazi wa *ZRB* na mfanyabiashara shilingi milioni 400,000,000 na alitaka pia Mhe. Ali Salum, *accounts* za wafanyakazi wa *ZRB* zichunguzwe, *accounts* zao ndani na *accounts* zao za nje. Niseme tu kwamba vyombo vinavyohusika na masuala ya kuchunguza tuhuma vipo vyombo hivyo, na naamini vimeshasikia na vitafuatilia masuala hayo ikiwemo tatizo la baadhi ya wafanyakazi wa *ZRB* kutokuwa waaminifu katika kutekeleza majukumu yao.

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini, kusoma bajeti siku moja na nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kusoma bajeti siku moja na nchi nyengine za Afrika Mashariki ni jambo linalowezekana, lakini tufahamu tu kwamba jambo hili halitakuwa na athari yoyote kwetu, kwani nchi zinazosoma bajeti kwa siku moja ni nchi zile ambazo zinafuata *Common Standard Tarrif*. Utayarishaji wa bajeti na mipango kutumia zaidi *top down* na sio *bottom up approach,* hili nalo pia lilizungumzwa na Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame.

Katika kutayarisha mipango ya bajeti zetu njia zote mbili hutumika kwa maana *top down* na *bottom up approach*. Wananchi wanashirikishwa kikamilifu katika uaandaji wa mipango ya kitaifa kama MKUZA na pia ushiriki wao upo kupitia kwa wawakilishi wao. Kwa hivyo, sisi humu ndani pia ndio tunaowawakilisha wananchi katika maeneo yetu.

Lakini vile vile tuelewe kwamba yako masuala ya kimkakati kwa maana *strategy issue,* hizi ni lazima zianze juu, ziende chini. *Strategy issue* lazima zitumie *top down approach,* lakini kwa upande mwengine mawazo ya wananchi ama ya moja kwa moja au kupitia kwa wawakilishi wao basi nayo yafike serikalini na mawazo hayo yanazingatiwa kama tulivyozingatia katika uandaaji wa MKUZA II. Mawazo ya wananchi yalikusanywa na ndio yanayofanya kazi kwa sababu MKUZA II pamoja na *vision 2020* ndio dira zinazoongoza mipango ya sekta na mipango ya kitaifa.

Lakini niseme tu kwamba mkakati wa MKUZA kwa maana ya MKUZA *success strategy*, unaofuatia MKUZA II. Tunatarajia utakamilika katika robo ya kwanza ya mwaka wa fedha wa 2016/2017.

Mhe. Naibu Spika, lipo suala jengine ambalo lilizungumzwa ni suala la Mradi wa Kuimarisha Utawala Bora (*Institutional Support and Good Governance Phase III*). Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame, alitaka uhamishiwe sekta husika na Wizara ya Fedha ibaki na usimamizi wa fedha.

Mhe. Naibu Spika, naomba kueleza kwamba miradi yote inapoandaliwa huwa inazingatia pia suala zima la uendeshaji na usimamizi wa miradi hiyo, na kufanyika tathmini ya *price* na wafadhili wa mradi huo. Utaratibu uliopo sasa wa mradi huu ndio hasa uliokubalika na wafadhili wenyewe kutokana na madhumuni ya mradi huu na kazi zake. Kwa hivyo, tathmini iliyofanyika iliona kwamba ile *institutional arrangement* ya kutekeleza mradi huu basi uwepo mradi huo ndani ya Wizara ya Fedha.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine lilikuwa ni kuongeza uwekaji wa *ATM* katika maeneo mbali mbali ili kuongeza huduma za kibenki, katika maeneo hayo na suala hili lilizungumzwa na Mhe. Yussuf Hassan Iddi, lakini pia lilizungumzwa na Mhe. Nadir Abdul-latif.

Mhe. Naibu Spika, *PBZ* ina mpango wa kuweka *ATM* 14 katika maeneo mbali mbali, lakini *ATM* 10 zinabadilisha *ATM* zilizopo sasa hivi ili ziwe na uwezo wa kutumia *visa card* na *master card*. Lakini vile vile *ATM* 4 zilizobakia basi zimepangwa ziwepo katika maeneo ya Mpirani, eneo la Kibweni KMKM, eneo la hospitali ya Kivunge, lakini na moja itawekwa katika eneo hili la Baraza la Wawakilishi ili kuweza kutoa huduma kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili na wafanyakazi waliopo hapa.

Lakini pia *ATM* za Benki ya Kiislamu hivi sasa zinatumika katika *ATM* zote, lakini pia *Islamic Bank* yetu sasa ina uwezo mteja akatumia hata simu yake ya mkononi kuweza kupata huduma za kifedha.

Mhe. Naibu Spika, naomba nitoe sahihisho dogo katika maelezo yangu ya kile kituo cha Mafunzo ya Amali pale Makunduchi. Nilisema kwamba vijana 40 wamepata mafunzo pale, badala ni vijana 40 wameshaajiriwa na kituo kile. Kwa hivyo, hilo ni faraja kubwa kwa vijana wa Makunduchi na maeneo ya jirani. Lakini vile vile niseme kwamba kwa wale ambao sikuwagusa moja kwa moja katika maelezo yangu haya, basi wachukulie kwamba nimefanya hivyo kua sio kuyadharau maoni yao, lakini maoni yote yaliyotolewa nimeyachukua, nimeya-*record* vizuri na tutayafanyia kazi ipasavyo.

Mhe. Naibu Spika, kwa mara nyengine naomba kukushukuru wewe, lakini niwashukuru pia wachangiaji wote, niwashukuru Waheshimiwa Mawaziri waliosaidia kujibu hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wajumbe, lakini pia niwashukuru hata wale ambao hawakupata fursa ya kuchangia iwe kwa kusema moja kwa moja kwa maandishi, kwa sababu naamini kwamba wamekubaliana na hoja niliyoitoa kwa asilimia mia moja. Nawashukuru wote na Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, Mhe. Waziri, ameshatoa hoja na kama Kanuni zetu zinavyotuelekeza tupige kura sasa tukubaliane wale ambao wanakubaliana…

MUONGOZO

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, mimi naitwa Hassan Khamis Hafidh, Mwakilishi wa wananchi Jimbo la Welezo, nimekuja hapa kuwatetea wakwezi na wakulima wa nchi hii. Katika siku nimefurahi Mhe. Naibu Spika, leo Mhe. Waziri wa Fedha ametoa majibu mazuri sana, lakini kuna mambo amekiri juzi nilitoa hoja kutumia Kanuni ya 120, katika hilo tukawa tunasikiliza majibu. Hoja moja niliyoisema kuhusu wizi wa pesa za Mfuko wa Wafanyakazi ambao nitatoa mfano. Kwa mfano, pesa zilikatwa katika mishahara ya wafanyakazi na zikaingizwa katika mifuko yao halafu zikatolewa. Mhe. Naibu Spika, mimi nimefanya utafiti na utafiti wangu umebaini ndani ya serikali hii inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi kuna watu ndani ya serikali hii hawaitakii mema serikali, ndio wanaofanya hujuma hizo kutaka kuiangusha Serikali ya Chama cha Mapinduzi.

Mhe. Naibu Spika, kwa heshima kubwa na taadhima kubwa kama tutaendelea kuwaachia wezi hao *Wallahi* watatufikisha pahali kuna siku pabaya. Nitatoa mfano jana nilikuwa nipo Mnazi Mmoja Hospitali…

Mhe. Naibu Spika: Hoja yako umeshasema kifungu gani, kwa Kanuni gani, sasa toa hoja.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Kwa hiyo, namuomba Waziri wa Fedha tu anipe maelekezo kwa sababu kasema hii hoja ya hawa wezi ameisikia hapa, nampenda sasa kaka yangu, sote ni wapya, hebu atujuze zaidi kama kaisikia hapa, hizi pesa zimeibiwa, wenyewe wanadai masikini ya Mungu, sifichi wanatisha mpaka kutaka kwenda Mahakamani kuishitaki Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi na sisi chama hiki ndio kilichotuleta humu.

Kwa hivyo, namuomba ajaribu kutujuza zaidi kwa sababu tuna hoja ya kuunda Kamati Teule juu ya suala hili la upotevu wa mishahara, ajaribu kutujuza zaidi suala hili kalisikia na kuna watu tayari wameshasimamishwa kazi dhidi ya suala hili. Je, Mhe. Waziri wa Fedha, naomba maelezo zaidi dhidi ya suala hili.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, Mhe. Waziri, amejitahidi sana kujibu masuala, amejitahidi sana na kwa kweli tunastahiki kumpongeza amejibu *almost* masuala yote. Sasa kama kuna kifungu kidogo ambacho hukuridhika nacho tunakwenda kwenye Kamati ya Matumizi, hapo ndio tutaweza sasa kumuuliza tena masuala, lakini sio sasa hivi Mheshimiwa, sasa hivi nauliza hoja kama imekubalika, sijui umenifahamu Mheshimiwa, sasa tukubali hoja tuingie ndani ya kamati, tukiingia ndani ya kamati kuna kifungu hujaridhika nacho Mheshimiwa, atakitolea maelezo.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Sawa Mhe. Naibu Spika, naomba tuendelee nasubiri kwenye vifungu.

UTARATIBU

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Naibu Spika,…

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Jaku, nilivyosema sijui kama umenielewa, sijui kama hiyo hoja inakuja sawa sawa na hiyo, lakini ninachokisema kwanza twende kwenye kamati halafu baadae kwenye kamati kama kuna kifungu bado hujaridhika nacho kutokana na maelezo ya Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, bana kwenye kifungu, tusianze kupeana shida sasa hivi.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, mimi wala siko huko, ungenisikiliza kwanza ninachokizungumza, watu wanasema; "mtu hakatai wito hukataa analoitiwa"…

Mhe. Naibu Spika: Sijakufamu bado.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, mimi wala siko huko, kuna msemo unasema na Kanuni zetu hazikatazi, "mtu hakatai wito hukataa analoitiwa", ungenisikiliza kwanza hoja yangu halafu ukanijibu Mhe. Naibu Spika, kwa heshima kabisa.

Mimi nikumbushe tu binadamu kuna kusahau na kupitikiwa Mhe. Hamza, ali-*raise point* moja muhimu sana hii leo, ndio nataka kukumbusha tumefikia wapi kuhusu Mswada wa Mnazi wa Mmoja, huu mswada ni muhimu na ni nzuri. Lakini…

Mhe. Naibu Spika: Nimeshasema nitautolea maelezo, sasa usiingilie kazi yangu, mimi najua nini nafanya, eeh, Mhe. Jaku.

Waheshimiwa Wajumbe, sasa nikuulizeni anayekubaliana na hoja ya Mhe. Waziri, anyooshe mikono, anayekataa, wanaokubali wameshinda.(*Makofi*)

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa Baraza limejadili na kukubali hotuba ya bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango, sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili kuvipitisha vifungu vya matumizi vya wizara yangu.

MUONGOZO

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nataka muongozo kwa Mwanasheria Mkuu atusaidie, unajua haya mafungu tunavyoyapitisha tunajua msimamizi mkuu anakuwa Katibu Mkuu wa Wizara, lakini mafungu haya Wizara ya Fedha naona msimamizi anakuwa ni Naibu Katibu Mkuu kama zile taasisi mfano kama mafungu ya Idara za SMZ unajua Makamishna, lakini hii hebu tusaidie Mhe. Mwenyekiti, unajua kuna vitu vyengine hivi tunataka ili tumjue dhamana tunayopitisha haya mafungu tunakuja kumkamata nani. Ufafanuzi tu kwa Mhe. Mwanasheria Mkuu.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kama ambavyo amesema Mhe. Hamza, mara nyingi tunapopitisha haya mafungu tunapitisha pia na msimamizi wake wa mafungu haya. Kwa mfano, tulipopitisha fungu la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali msimamizi wake ni Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Pia, tunapopitisha fungu la Wizara ya Fedha imewekwa msimamizi wake ni Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, kwa nini tunafanya hivyo? Kwa sababu Sheria ya fedha za umma zinatoa idhini kwa Katibu Mkuu Wizara ya Fedha kuteua Maafisa *Mas-uul* wa kila fungu.

Sasa kwenye fungu la Wizara ya Fedha, Katibu Mkuu aliyemteua asimamie fungu hilo ni Naibu Katibu Mkuu, hawezi akajiteua yeye mwenyewe kusimamia fungu lake. Sasa hayo ni matakwa ya kisheria ambayo ameyafanya Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na ni jambo la kawaida, na ni jambo la kisheria. Nakushukuru.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, napiga *salute*.

KAMATI YA MATUMIZI

FUNGU F 01 WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO

Kifungu F0102

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya mwanzo na kuonesha *concern* kidogo. Kwenye hotuba ya Mhe. Waziri, katika kitabu chake katika ukurasa wa 34 anaeleza mamlaka ya uwekezaji wa vitega uchumi Zanzibar. Pesa ambazo amezitaka kwa muda huu ni asilimia mia, lakini matumizi asilimia mia, lakini hoja yangu iko hapa.

Mhe. Mwenyekiti, kila baada ya mkutano kama huu waziri anatakiwa alete ripoti kwa sheria ambayo imepitishwa hapa Barazani, ili tujadili tuone basi matumizi yake anayapanga vipi, lakini vile vile na *auditing reporting* yake ya matumizi iwe imeletwa hapa. Nataka kujua

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa, unatambua kwamba haya ni mapato?

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Ndiyo tuko kwenye mapato na mimi nasema mapato hapa.

Mhe. Mwenyekiti: Sawa endelea.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Nataka kujua tu ile sheria ambayo inamtaka waziri alete hapa mapato yake na kuijadili, ameileta hapa, ameshawahi kuileta kwa sababu sijaiona hapa, lakini na huku anataka mapato haya asilimia mia, lakini vile vile anataka kutumia asilimia mia, nataka kujua haya mapato na hii sheria...

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa, hebu tuambie hiyo sheria yenyewe, sheria gani unayoitaka wewe iletwe inayoeleza kwamba mapato yaletwe hapa, taarifa ya mapato iletwe hapa, sheria gari?

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Ni Sheria ya 2002, Sheria Nam. 1 ya Kifungu cha 27.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa, hebu rudia ili Waheshimiwa Mawaziri, itaje kwa ukamilifu kabisa, sheria gani na jina na mwaka.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, ni Sheria Nam. 4 ya mwaka 2002, Kifungu cha 27, kinamtaka Mhe. Waziri, anayehusika na mambo ya fedha au yeyote alete ripoti ya mwaka hapa tuijadili kabla ya kuweka mapato haya ya mamlaka hii, hatuyaoni au tunapigwa changa la macho hofu yangu, au nisome hiyo sheria yenyewe vile vile?

Mhe. Mwenyekiti: Mimi nilikuwa nataka uniambie jina la hiyo sheria kwa sababu hujalisema jina la sheria kwanza.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Sheria Nam. 4 ya mwaka 2002.

Mhe. Mwenyekiti: Haya Mhe. Dimwa, umeshafahamika utajibiwa na Mwanasheria Mkuu.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, ninavyoona tuko kwenye Mapato ya Idara ya Mipango, Sera na Utafiti. Sasa hoja ya Mhe. Dimwa, ambayo imewekwa kwa mujibu wa sheria aliyoitaja iko kwenye mashirika ya umma, mashirika ya serikali ambayo yanaongozwa na Sheria Nam. 2 ya mwaka 2002. Sasa hapa sioni kama kuna hoja ya mashirika ya serikali, hapa tuko kwenye Idara ya Sera, Mipango na Utafiti, sasa labda angesubiri tufike huko kwenye ambayo anayoitaka kusema ili sasa asimame halafu na sisi tupate kumjibu.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, Mhe. Dimwa, subiri Mhe. Waziri, anataka kuongeza majibu.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri yaliyotolewa na Mhe. Mwanasheria Mkuu, naomba kumueleza Mohammed Said Dimwa, kwamba hotuba yangu niliyoiwasilisha ndiyo taarifa yenyewe ya utekelezaji wa mapato hayo.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, nimemuelewa sana Mhe. Waziri, hotuba hii haina vigezo vya kusema, hapa anasema tu nitatumia kiasi fulani, lakini na makadirio yangu asilimia mia kwa mia zinatumika, ukiniambia hotuba hii tu, hii sio hotuba hapa ya kuzungumza, sio ripoti unayoleta hapa ya matumizi, tuletewe ripoti tuijadili Barazani, siyo hii, hii siyo ripoti hapa, hii *page* mbili nini tunafanya.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa, lakini ushauri alioutoa Mwanasheria Mkuu umeusikia.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, nimjibu nani mmoja nichukue ya Mwanasheria Mkuu nichukuwe ya waziri.

Mhe. Mwenyekiti: Hata hivyo Mwanasheria Mkuu amesema kwamba usubiri mpaka kifungu kinachohusika ndiyo uulize. Kwa hiyo, sisi tunaendelea kwanza.

Kifungu	F0102	Idara ya Mipango, Sera na Utafiti	7,632,600,000
Kifungu	F0103	Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali	58,000,000,000
Kifungu	F0104	Idara ya Fedha za Nje	326,100,000,000
Kifungu	F0105	Idara ya Uhakiki Mali na Mtaji wa Umma	0
Kifungu	F0111	Bodi ya Mapato Zanzibar	237,000,437,000
Kifungu	F0112	Idara ya Forodha	

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi hii.Miongoni mwa waliochangia suala la uingizwaji wa kuku na samaki nchini alikuwa Mhe. Abdalla pamoja na mimi nililizungumzia vile vile. Suala hili nimelizungumzia kwa kuona kwamba tulipiga kelele sana kuhusu uingizwaji wa kuku na kuua soko la wafugaji wa ndani, leo tukaambiwa serikali itakwenda, itakaa ili na tulipendekeza kwamba iwekwe kodi ambayo itawasababisha na wananchi wetu waweze kuuza kuku wao. Suala hili halikushughulikiwa, lakini leo sasa hivi tayari tumeletwa mapato ambayo ya uingizwaji wa kuku nchini, hapa nazuia fungu ambalo linashikilia masuala ya forodha.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nilisikiliza maelezo ya Mhe. Waziri, lakini mimi hayakunitosheleza kwa sababu. Sababu zangu ni kwamba yeye amesema kwamba uzalishaji wetu wa kuku ndani hautoshelezi soko na vigezo vinavyochukuliwa na serikali soko katika hoteli za kitalii. Mimi katika suala la hoteli za kitalii sina matatizo kwa sababu ule ni uwekezaji, lakini hawa kuku na sasa hivi wameingia na samaki wanauwa mpaka soko la ndani.

Mhe. Mwenyekiti, kuna muwekezaji mmoja amejenga mabanda karibu ya milioni mia tatu, leo hakuna kuku hata mmoja, hawezi akashindana na hili soko, ndio maana tukasema iwekwe kodi ambayo kwa hawa kuku wanaoingizwa waweze kushindana na soko la ndani, lakini sasa hivi hii kodi ambayo inayolipishwa inaua wafugaji wetu wa ndani, sasa hili suala Mhe. Mwenyekiti, bado maelezo ya waziri hayajanitosheleza, labda anieleze vya kutosha zaidi ili niweze kuridhika.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema wakati nikitoa ufafanuzi wa hoja hii. Nilisema kwamba suala hili tutakaa tuliangalie, lakini hapa sasa hivi tunapitisha vifungu vya mapato na tayari tukumbuke kwamba Mswada wa Sheria wa Mapato kwa maana ya *Finance Bill* na mapato haya yote yamo, tumeshauzingatia na tumeshaukubali.

Mhe. Mwenyekiti, nilichokisema katika maelezo yangu na naomba nikirudie hicho, kwamba suala lililozungumzwa na Waheshimiwa Wajumbe, hapa linafaa kuangaliwa na kuzingatiwa kwa kina hiyo *statement* niliyoizungumza na nikasema kwamba tutakaa na wizara inayohusika. Kwa sababu masuala ya *industry* ya kuku ni mengi, tukizungumzia uzalishaji mdogo unaweza ukatokana na vifaranga vyenyewe, yaani *quality* ya vifaranga, lakini inaweza kutokana na chakula chenyewe *quality* ya chakula chenyewe, gharama za madawa, sasa haya yote yanahitaji kwa upana wake ili kuweza kuona ni jinsi gani tunaweza kumsaidia mfugaji. Kuku anaweza kufa kutokana na vifaranga vibovu na ni tatizo kuku wanakufa na isiwe sababu ya kodi, kwa hiyo hilo nalo linahitaji kutizamwa kwa upana wake.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Hamza, akubaliane na mimi kwamba atupe muda tukakae, tulifanyie kazi, tulifakari na pale tutakapoona kuna haja ya kufanya hivyo kwa maana ya kuingia kwenye kodi basi serikali itafanya maamuzi, sekta zinazohusika ziko tutakaa tutalizingatia serikali na kuona jinsi gani tunaweza kuwapunguzia usumbufu wazalishaji wetu wadogo wadogo. Lakini kwa sasa hivi suala la kodi ya kuku wanatozwa *import duty* ya 25% na *trade levy* ya 5%, hizi ndio tunazotoza, sasa kama kuna haja ya kuongezwa hizo tutakaa tuzingatie ili kulilinda soko la ndani.

Mhe. Mwenyekiti, lakini nako kuna athari yake kama uzalishaji bado mdogo, sasa haya yanahitaji kuzingatia ili kuona *balance,* usije ukaongeza makodi uka-*restrict import* halafu ndani uka-*create shortage* kubwa sana ambayo pia itakuja kulalamikiwa na wananchi.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri, kwa kuwa ni mpya katika wizara hii naweza nikakubali na kwa sababu. Niliwahi ku-*raise* hoja hii na Mhe. Waziri wa Fedha, kipindi kilichopita alipiga maneno matamu kweli kweli hapa na tukaona kwamba watakwenda kukaa ili kuliangalia upya, tokea kipindi kile kodi hii imebakia ile ile na matokeo yake wale wafugaji waliokuwa wana tamaa serikali italiangalia, sasa hivi wamekata tamaa kabisa na mabanda yako makavu. Nadhani sasa hivi Mheshimiwa, mabanda yale sijui kama hayafugwi chui, maana yake kuku hawana.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nilikuwa namuomba Mhe. Waziri, katika hicho kikao chenu mtakachokaa, unajua tatizo serikali wanakaa wao, hawakai na wadau. Mimi naomba Mhe.Waziri, naomba hicho kikao chenu kiwe *tripartite* kwamba baina ya wadau wafugaji wa kuku na hawa wadau ambao niliokwambia tayari mabanda yao ni matupu na wakati wowote wanaweza wakaingiza chui pamoja na serikali pamoja na hiyo mamlaka ya mapato ili wale kuweza kutoa ushauri wao wakaweza kusaidia.

Mhe. Mwenyekiti, hili wenzetu wa Tanzania Bara wamelifanya na sasa hivi hakuna kuku anayeingia Tanzania Bara na wafugaji kule sasa hivi wanafuga kuku wazuri tena wakubwa kuliko hilo paja nono. Sasa sisi hapa tukishapita hapa ngoma ikeshapita, hakuna utekelezaji, lakini ninamuamini sana Dkt. Khalid na ni kijana ambaye tunamuamini ataweza kufanya hii kazi na mimi basi Mheshimiwa, kabla ya bajeti inayokuja nisije nikamzuia tena basi aje anishirikishe kwenye japo kikao kimoja na ninaposema anishirikishe yeye mwenyewe anajua, sizungumzii mambo yale mengine.(*Makofi*)

Lakini alau ionekane ile jitihada yangu ya kuwasaidia wafugaji kuingia na wao ndani ya soko na wakawezeshwa na serikali. Ahsante Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Tunaendelea baada ya hayo, tunaendelea.

Kifungu	F0102	Idara ya Forodha TRA	114,844,783,000
Kifungu	F0103	Idara ya Kodi za Ndani TRA	73,951,217,000
Kifungu	F0114	Idara ya Mitaji ya Umma	

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, napenda nisimamie tena hoja yangu hii kuwa ripoti hii inasema Kifungu (c); *'The audit report of those financial statements.'* Mimi sijawahi kuiona katika Baraza hili na hakuna ripoti inayoletwa na serikali hapa kwenye mashirika tukaijadili na sheria hii imepitisha Baraza lako, sijapitisha mimi na nina khofu sana Baraza hili litakosa nguvu ya kuisimamia serikali.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba nimjibu Mwakilishi wa Jimbo la Mpendae kuhusu hoja hii ya ripoti. Jamani lazima tuelewe kwamba kila kitu kina utaratibu wake, sheria haiendi, sheria ipo lakini na sheria pia inaongozwa na kanuni inaongozwa na utaratibu na miongozo mbali mbali. Ndani ya Baraza hili kuna utaratibu wake na utaratibu wa Baraza katika kuwasilisha *annual report* ni utekeleza wa maamuzi ambao sisi kama mawaziri tunautoa kila kabla ya bajeti na ndio maana tunatoa nini tumetekeleza kwa mwaka ule tumepata kiasi gani na

tumefikia wapi. Sasa ile ni ripoti ya mwaka ya utekelezaji wa majukumu. Naomba Mhe. Dimwa, uweze kuelewa hilo na naomba uunge mkono hoja ili tuweze kuendelea, nakuomba sana.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru nimemuelewa sana Mhe. Waziri, na hoja yake dhaifu sana. Siwezi kupokea hoja dhaifu kama hiyo, kwa sababu hapa tunachotakiwa kujadili, tusipigane machanga ya macho, mashirika haya Mhe. Miraji, kasema kule kuna *lease* ngapi zinatokea, kuna *tax holiday,* kwa nini tusiweze kujadili, serikali inaogopa nini tusijadili.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nilikuwa naomba Mhe. Mohammed Said Dimwa, animalizie ile sheria inasemaje, lakini kama anazungumzia *audit report, CAG* huwa anaandika ripoti kwa taasisi zote ziliopo na ripoti hii inawasilishwa hapa, lakini ripoti hiyo hiyo pia inapewa *PAC* kuifanyia kazi na ripoti hiyo pia inakuja serikalini nayo tunaifanyia kazi na kuja kutoa majibu yake hapa Barazani.

Sasa kama ni *audit report, CAG* anafanya kazi, kama ni kuleta *estimate* zao kuhusu taarifa za mapato na matumizi hapa Barazani kama ndivyo alivyokusudia Mheshimiwa, ni kwamba hizi taasisi au haya mashirika hayako kwenye *votes* hizi tunazozizungumza hapa, hapa tunazungumza *votes* ambazo zinazungumzwa ndani ya *budget estimate,* hawa wana utaratibu wao mwengine wa kupitisha bajeti zao kwa maana ya mapato na matumizi ambayo yanapitishwa na waziri anayehusika, bodi zao kwanza na waziri anayehusika anaangalia matumizi na mapato hayo, hayaji hapa Barazani. Sasa sijui moja wapo analolizungumza Mhe. Mjumbe, ni lipi katika hayo mawili.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, ningemuomba Mhe. Waziri, aende kwenye sheria hii *sub section of audit report* na ripoti ya 27 ili kuona sheria hizi zinatungwa hapa na serikali na zinapitishwa na Baraza lako, lakini sheria hizi lazima tuziwekee meno ya kuweza kujua, lakini kwa sababu hii ni hoja yangu ya tatu na mimi sitaki kwenda kwenye kura, nataka serikali ielewe, ijue ituletee tujadili, kwa nini tusijadili. Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Kifungu F0114	Idara ya Mitaji ya Umma	6,000,000,000
Kifungu F01015	Idara ya Uhakiki Mali	390,000,000
JUMLA KUU		**824,355,600,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapa juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Kifungu PF0101 Programu Kuu ya Usimamizi wa Bajeti na…

(Hapa Waheshimiwa walisimama kutaka kuhoji kifungu hicho kilichotajwa)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa, bado.

Kifungu PF0101 Programu Kuu ya Usimamizi wa Bajeti na Fedha za Umma
Kifungu SF01

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana, wakati nilipokuwa nachangia kwa maandishi nilitaka kujua kuhusiana na malipo ya walimu yale, mbali na majibu ya Mhe. Waziri, lakini kuna fedha ambazo walimu walikatwa kimakosa. Sasa hakutoa maelezo sahihi kuhusiana na fedha zile ambazo walikatwa kimakosa vipi watalipwa na lini wataanza kulipwa pesa zao hizi.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mjumbe, kwamba nilivyosema pale nilisema kwamba tutakaa na waziri na tumeshapanga baada ya bajeti hii kupita tukae tutizame yale madeni yote yaliyoko kwa walimu, madeni yote yaliyoko ndani ya sekta ya elimu ili tuyafanyie mpango wa kuyalipa madeni haya. *Commitment* hii tumeshaichukua kwamba ni *priority* kulipa madeni ya wafanyakazi wetu, kwa sababu wanafanya kazi kwa ajili ya kukidhi mahitaji yao na maisha yao. Serikali hili imeshaliona na ndio maana tumeweka kipaumbele kulipa madeni ya walimu bila ya kuainisha ni deni la namna gani.

Kwa hivyo, kama kuna mikato tutaijua kutoka kwenye sekta na utaratibu wa kuyalipa madeni hayo yaliyokatwa kwa makosa basi yatafanyiwa kazi. Mheshimiwa, naomba aridhike kwamba hili tutalifanyie kazi atupe muda na iko nafasi huko mbele ya kuja kutuuliza jinsi gani tulivyolitekeleza.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Mwenyekiti, nimeridhika tuendelee.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, kifungu ni Usimamizi wa Bajeti ya Fedha za Umma, nilipokuwa nachangia nilizungumzia *AGAPE*, ingawaje Mhe. Waziri, ametoa majibu mazuri, lakini hoja yangu inasimama pale kwamba pesa zote zinazotolewa kwenye taasisi zinatoka Wizara ya Fedha na *AGAPE*, kuna ushahidi mwingi kwamba hii *project* imeitia hasara serikali na inaendelea kuitia hasara. Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo, amekiri, sasa hapa hoja ni pesa. Namuomba Mhe. Waziri wa Fedha

na Mipango, bado tunasimamia kwamba pesa hapa zimetumika vibaya anijibu kwa sababu pesa zinatoka Wizara ya Fedha hazitoki kwengine. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana, kwanza nimpongeze Mhe. Mwakilishi wa jimbo la Welezo kwa jitihada zake na uchungu wake dhidi ya wananchi kuwatafutia yale maovu ambayo yanaithakili serikali na sisi kututaka tuyaweke sawa, hususan msimamo wake wa kuwatetea wakwezi na wakulima ambao sisi ndio wametuzaa. Kwa sababu na sisi tunatoka katika hiyo mifupa ya wakwezi na wakulima, ningefarijika sana na kwa vile suala hili liko ndani ya Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo, mmoja katika wadau, Mhe. Hassan Khamis, angenipatia ushahidi tukakaa tukaufuatilia pamoja na yeye ili tukaweka wazi, bayana, hadharani huyu mwizi na huyu sio mwizi tukaelewa hili suala linakwendaje.

Kwa hivyo, ningemuomba kwa sababu mwenzangu anafanya *research*, anafanya utafiti, ina maana tayari anao na mwisho wa utafiti unakuwa na *result* kujua *result* hizi zimetafutiwa, zimepata uhakika, zimefanyiwa *analysis*, zimefanyiwa *evaluation*. Kwa hivyo, akitupa na tukishirikiana na yeye pamoja, mimi nashukuru tuko karibu sana na mpiga kura wangu huyu, kwa hivyo, aniletee kwa njia zote mbili; yoyote atayoiona rahisi tutashirikiana naye pamoja tulifanyie kazi kwa kina. Naomba Mhe. Hassan, tukae pamoja, tushirikiane, atuletee hizo taarifa ili tuzifanyie kazi, tukisha tutoe majibu. Ahsante sana.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, nampongeza sana Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo kaka yangu, lakini yeye mwenyewe katika maelezo yake hapa leo amekiri kwamba kwenye *AGAPE* kuna matatizo na nina-*quote* maneno yake. "King'amuzi cha *AGAPE* mimi situmii", maana yake nini, kwamba hapa kuna matatizo, Mhe. *VP2* pia amekiri. Sasa naomba kusema hivi, shilingi bilioni nane zilizotumika kunako *AGAPE* na kufeli zingetumika hospitali tungepata maendeleo makubwa.

Naomba suala hili serikali ilipe kauli mahususi na inayofaa, sio maneno ya kisiasa tunakwendaje, kwa sababu lina *public interest*, wananchi wote wanaizungumza *AGAPE* na vijana wanakwambia hivyo tunapitwa na Said Salum Bakhresa! Tunapitwa na *Coconut!* Ni aibu, miradi kama hii ya serikali kila siku haiendelei, inafeli kutokana na imani za watu wengine kutaka kuiba. Nilisema *statement* yangu ndani ya serikali hii kuna watu ambao hawaitakii mema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa, lakini huu sio wakati wa kutoa hotuba, unajua hayo.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Ahsante, kwa hivyo, naomba serikali inipe maneno dhidi ya suala hili. Mwenyewe Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo kakiri na yeye hatumii king'amuzi naomba kuwasilisha.

Mhe. Mwenyekiti: Tuendelee, tunaendelea.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Aaa, nataka kauli, Mhe. Mwenyekiti, naheshimu kiti chako lakini nataka kauli.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, kwanza suala ambalo analizungumza halimo kwenye vifungu au kasma, haimo kabisa kwenye eneo hili. Sasa ningemuomba tu mawazo yake, fikra tumeshazisikia waziri anayehusika na sekta ameshasikia na ameshamuahidi kwamba watakaa pamoja watalifuatilia akubali hilo, atuache tuendelee.

Lakini la pili, lile suala la kusema kwamba pengine zile fedha zilizotumika kwa *AGAPE* zingetumika hospitali. Ningependa kumfahamisha au kumueleza kwamba, mambo yote haya ni muhimu katika nchi na yote yanahitaji fedha. Maana yake tusingeweza tukasema kwamba basi serikali iingie katika *digital*, tubaki kwenye *analogue* wakati ulimwengu mzima umeshaingia kwenye *digital*, isingewezekana kwamba serikali isifanye jitihada za kununua ving'amuzi na televisheni yetu ingekuwa wapi. Kwa hiyo, hilo nalo ni jambo la muhimu na hospitali vile vile ni muhimu, lakini na maeneo mengine yote ni muhimu.

Kwa hivyo, tuondokane na dhana hiyo kwamba hizi pesa kuna upotevu, matumizi yaliyofanywa kwamba si matumizi mazuri, ni matumizi mazuri na yalilenga kabisa katika kuisaidia nchi yetu kiuchumi na kijamii. Kwa sababu hiki ni chombo cha kitaifa lazima kisikike, kauli za serikali lazima zisikike kupitia kwenye chombo chake, ni suala muhimu sana.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru sana kwa maelezo mazuri ya Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, hata na mimi nataka nchi ya Zanzibar iwe katika *digital*, lakini bado hatupo katika *digital* kwa sababu king'amuzi ya *ZBC* sicho kinachotumika Zanzibar badala yake vinatumia vyengine. Kwa nini, kwa sababu ya kufeli *project* hii. Sasa...

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Hassan Khamis, nikuombe kidogo, tuachie tuendelee. Umepata majibu mazuri sana kutoka kwa Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo na hayo yanatuonesha kwamba iko nia safi kabisa ya serikali kulifuatilia suala hili. Kwa hiyo, naomba utuachie tuendelee kwa sababu utakalolisema ndio hilo hilo litajirudia, kwa hiyo, itakuwa hata haileti maana. Tuachie tuendelee ili hizo kazi nyengine tuje tumalize. Mhe. Hassan, naomba sana usikilize kiti changu, nakuomba sana, majibu yanatosha uliyoyapata, si dhani kama kuna ziada ya majibu. *(Makofi)*

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, leo ni Ramadhani ya 21 nazungumza haya kwa sababu sio ya kujifanya najua kusema au vipi, ni uchungu wa masuala kama haya ya *project* za serikali. Sasa juzi nilitaka kutumia kifungu cha 120, lakini kwa sababu umeniomba sana na wewe ni Naibu Spika na sasa ni Mwenyekiti kwa mara ya kwanza naomba nikuheshimu kuliko siku zote nikubali tuendelee.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kunijaalia uzima, lakini mimi pia nilichangia suala la *Airport* na nashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri kama watatu walinijibu vizuri. Lakini tukienda kwenye mali ya umma hizi fedha zilizotumika kwenye kujenga *Airport.* Mhe. Simai Mohammed, aliwahi kuzungumza kuwa ni uzembe, huu kweli ni uzembe na unakubalika kuitwa uzembe. *US$* 128 milioni kwa *Airport* ile Mhe. Waziri wa Fedha, lile jengo la *Dubai Tallest building in the world*, jumba refu duniani kwa *square metre* hata *Airport* haijafikia, lile jumba halijafikia *amount* ya pesa iliyojengewa *Airport* ya Zanzibar kwa *square metre*.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, namuomba sana fedha za umma kwa vyovyote najua *Airport* iko kwenye mawasiliano, lakini ukija *terms of payment* masuala ya benki, masuala ya mikopo inamuhusu Waziri wa Fedha na Mipango na ni fedha za wananchi ambazo ni fedha za umma. Mimi ningeomba sana ubadhirifu huu uchunguzwe, awe makini na fedha zilizotumika kwenye *Airport* ile haiwezekani. ni fedha nyingi sana, *US$* 128 milioni unajenga Mabaraza ya Wawakilishi kama haya 300, unao uwezo huo kwa fedha hizo.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa, ulipata nafasi ya kuzungumza hayo kipindi kile cha mchango, sasa toa hoja tu.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardi: Naomba Mhe. Waziri, anijibu kwa sababu sitaki nipige buti wala kuzuia kifungu, sina lengo hilo, lakini anikubalie tu kama hili suala lililofanyika ni uzembe. Kwa sababu suala ambalo si uzembe

binadamu hawezi kuunda kitu kimoja tu, yaani kumuumba binadamu, ila Mwenyezi Mungu mwenyewe ndiye anaweza akamuumba, lakini kwa suala la *Airport* kukosewa zaidi ya mara nne, vipimo sijui vimekwenda vibaya, sijui kipimo kimerudishwa nyuma.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa, sijui unanielewa, hiki sio kipindi cha kuchangia kama una swali unataka kuuliza au una hoja utoe hoja yako, maelezo marefu umeshapata nafasi hiyo ukayatoa.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Ahsante, mimi swali langu ni mainjinia gani na vigezo gani walitumia mwanzo mpaka yakatokea matatizo yote zaidi ya mara nne kutokea tatizo hili.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, naamini Mhe. Nadir Abdul-latif, wakati ambao tulikuwa tunatoa michango yetu kwa madhumuni ya kujibu baadhi ya hoja ama alikuwa hayumo au hakutaka kusikiliza kwa makini. Kwa sababu maelezo haya nadhani wangeyaweka wazi wenzetu, hofu yao au tatizo lao liko wapi, maana mradi huu una sehemu mbili kwa tatu.

Sehemu ya kwanza, inahusiana na suala la mkopo wenyewe, Sehemu ya pili, inahusiana na utekelezaji wake na Sehemu ya tatu, namna ya utekelezaji wa mradi ulivyosimama. Sasa tatizo liko wapi, kama Sehemu ya kwanza, tumekopa shilingi 70.4 milioni tukaona katika utekelezaji wake jengo halitokidhi vigezo na mkataba wetu tulikubaliana kwamba wajenzi wa-*design* halafu sisi turidhie pajengwe. Serikali ikaajiri mtu wa kutusaidia kuthibitisha michoro tukagundua kuna mapungufu, tukaingia nyongeza ya mkataba baina yetu sisi na mjenzi. Nyongeza ya kwanza na nyongeza ya pili, kilichokwama na kilichopelekea mradi kusimama sasa hivi sio suala la kiufundi ni suala la upatikanaji wa fedha. Fedha mara ya kwanza tumelipa shilingi 21 milioni mwaka 2010 kwa mujibu wa mkataba, tukalipa mara ya pili shilingi 14 milioni mwaka 2011 mwezi Novemba kwa mujibu wa mkataba, mara ya tatu mwezi Mei, 2015 wakapeleka maombi ya shilingi 17 milioni zikazuwiwa, kwa sababu watoaji wa fedha walikuwa hawajaridhika na ajenda mbili ambazo sisi wajengewa na mkandarasi upande wa utoaji wa fedha wakasema hapana tujiridhishe.

Sasa tukisema uzembe, mimi siamini kama kulikuwa kuna uzembe. Kwa sababu hadithi ya jengo sote tunaijua ilivyokuwa. Jengo limeanza kujengwa kwa mujibu wa michoro ya *World Bank* na hatukuwa na uwezo wa kulipa *compensation*, tungelijenga upande wa Magharibi lakini sote tunajua, tumekuja

kuhamisha makaburi ya watu juzi katika kupitisha *apron* na *taxiway*, hatukuwa na uwezo wa kulipa *compensation* wakati huo. Baada ya wenzetu kuja kuona kuna makosa kwamba mita 60 *tail* itasababisha *obstacle* wenzetu wataalamu wa *IDPI* wakatushauri, kwamba tuondoshe *apron* kubwa ya ndege za *type E* tuyaondoshe upande wa Mashariki tuweke upande wa Kusini. Sasa tunapozungumza uzembe hizi jitihada za serikali hazionekani?

Suala la hizi gharama kuongezeka tusijichanganye, ukichukua eneo la *square metre* 25 ukigawanya kwa hivyo kweli utaona jengo liko ghali, lakini hapa tunachokizungumza gharama hizi ni *infrastructure with superstructure*, kwa maana ya kwamba lile jengo lenyewe na vifaa vyake. Lakini katika hilo jengo lenyewe kuna fedha zimeongezeka kwa mujibu wa mchoro tulioubadilisha, tunazungumza *apron* ya Kusini, *apron* peke yake imetugharimu *US$* 22 milioni ambazo hizi imebidi ziongezewe katika huo mkopo. Sasa tunapokaa tukisema kwamba ah, shilingi 128 milioni kwa *square metre* 25 pesa nyingi, ni kweli, lakini hizo *square metre* 25 zipi, tusichukue *square metre* 25 za jengo, hapana, mradi huu na vingine vimeongezeka, ukichukua *apron*, ukichukua zile *eurobridge* ambazo zilikuwa zinatoka *type C* kwenda *type E* gharama yake *eurobridge* moja ni *1.4 million dollar*, hizo ndio zilikuwa *included*.

Mhe. Mwenyekiti, tunaposema uzembe, mimi nadhani sio lugha nzuri kabisa, kuna jitihada kubwa sana ya serikali na mradi kusimama kwake si kutaka kwetu sisi ni *policy* ya nchi yenyewe, kwa maana ya kwamba *export and import Bank* ya China imebadilisha sera na sheria husika, hawawezi kutupa fedha mpaka wajiridhishe wao wenyewe, wamebadilisha utawala, wamebasilisha sera, wamebasilisha mfumo. *(Makofi)*

Mkopo wetu wa kwanza ulikuwa *soft loan*, mkopo wetu wa pili umekwenda katika *concessional*, masharti yamebadilika. Kwa hivyo, tunapozungumza hili suala la huu mradi tusione tu labda watu wazembe hawataki, hapana, ziko jitihada kubwa ambazo zimepelekea huu mradi kufika hapa ulipo na kumalizika kwake.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nikuombe tu, sijaamini kabisa kama mradi huu umefika hapa kwa sababu ya uzembe. Mradi huu umesimama zaidi ya miezi 18, serikali wanahangaika, tumeshakwenda China zaidi ya mara nne katika kuzungumza na wenzetu wa *Exim Bank* ili tupate ruhusa ya kutumia fedha hizi tukamilishe. Wenzetu hawa wamejenga toka mwaka 2012 mpaka leo hawajalipwa Kampuni ya *BCEG*, tungewafikiria wao wanaishi vipi na kufanya kazi zao pale, wao wamezuwiwa malipo yao na hao hao *Exim Bank* kwa sababu ya kujiridhisha na taratibu na mabadiliko ya sheria walizozifanya.

Sasa sisi tunaona hivyo, hawa wenzetu wanaojenga wanaishi vipi, lazima na sisi tujiulize hawa wanatudai wamefanya kazi na tumeridhika kutoka 2012 mpaka *certificate* yao waliyotupa mwezi Novemba, 2015 wamekamilisha kazi, hatuwezi kuwalipa shilingi 17 milioni kwa sababu zimezuwiwa kwa mujibu wa taratibu na sheria za *Exim Bank,* sasa uzembe uko wapi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani sote tuna uchungu, hatuna kwengine kwa kwenda, hili lazima tukubali limetokea na limetokea kwa matakwa yetu sisi wenyewe, lingejengwa jengo kwa shilingi 70.4 milioni lingekwisha, lakini je, lingemridhisha nani? Ndio hapo tulipofanya mabadiliko kupitia serikali, jengo kwa mfumo ule lisingekuwa jengo lenye tija lingekuwa jengo lipo na lisingetumika na lisingekuwa na faida yoyote, tungelaumiana maradufu, ndio serikali tukafikia maamuzi ya kufanya hayo mabadiliko ambayo tunayaona leo ni ghali kwa kutaka sisi. Mambo yako mengi sana, Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Mwenyekiti, majibu mengi mimi mwenyewe mpaka mengine nimeyasahau, maana yake kaeleza muda mrefu sana. Lakini ninachotaka kusema kwanza tumpongeze sana Mhe. Rais wetu Dokta Ali Mohammed Shein na Makamu wa Pili wa Rais kwa ustaarabu wao na mwenendo wao mzuri. Mimi naweza kusema tena ni uzembe, sisemi serikali yangu, sisemi Chama changu kilichofanya, huwezi kusema ramani ishachorwa unataka kujenga kitu halafu unakuja kuambiwa kimekosewa hasa ujenzi wenyewe kama ule hata mita 200 haufiki kwa upana umekosewa, zaidi ya *US$* 70 milioni ni *around One Hundred and Fourty Billions Shillings (140 billion)* halafu leo tusiseme uzembe kwa watu watano, sita waliosababisha. Mimi nitaita uzembe, waliosababisha ni wazembe, sisemi serikali yangu, serikali yangu inataka mambo mazuri, viongozi wetu wanataka mambo mazuri. Lakini huu ni uzembe, fedha hata tukisema dola milioni ishirini, basi ni bilioni hamsini, kama kitu kimekosewa cha bilioni hamsini tukiite nini, tuite ujinga au uzembe. Mimi nanichotaka kusema uzembe umefanyika...

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa, angalia sana lugha unayotumia, angalia sana, unasema husemi serikali yako uzembe. Lakini ukae ukijua unazungumza na serikali, hivyo, unavyosema unainyooshea kidogo serikali. Sasa angalia sana lugha unayotumia, hayo maneno mengine naomba sana jitahidi usiyatumie. Najua una hasira, lakini jitahidi sana usitumie lugha ambayo haipendezi.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Wal- Wardy: Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na mambo yako mazuri, lakini mimi nime-*mention* watu waliosababisha hili. Lakini sasa mimi ningemuomba sana Mhe. Waziri wa Fedha, miradi inakuja na

mambo yanakwenda awe makini sana. Vitu kama hivi mwaka 2017/18 tutakuwa hatufahamiani humu ndani. Kwa sababu fedha za watu za umma zimetumika vibaya na tunaona. Mimi nitaishia hapa, sitaki kwenda kwengine hata kujibiwa wala kwenda kwengine mbele, lakini maneno yangu ndio haya.

Kifungu SF010101 Programu ndogo ya usimamizi wa Hazina 28,837,234,000

Kifungu S

Mhe. Simai Mohammed Said(Mpakabasi): Ahsante Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri aliyoyatoa mazuri aliyoyatoa Mhe. Waziri wa Fedha na mimi nilikuwa nataka niulize suala dogo ni kwamba amezungumza suala la *Fiber optic* na amesema kwamba Kampuni ya *Zantel* iliingia kwenye misikosuko katika muda wa miaka mitatu na serikali ilishindwa kuweza kukusanya.

Kwanza, nimpongeze kwa majibu aliyoyatoa kwamba tayari mkataba umeshafungwa. Lakini Mhe. Mwenyekiti, haiingii kichwani kwangu mimi kwamba kwa muda wa miaka mitatu Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imefunga mkataba ya Kampuni ya *Zantel* ambao wanatumia hii *Fiber optic* ambayo ya kwanza inayotoka baharini kutoka Dar-es-Salaam kuja hapa Zanzibar. Lakini pia hii *Fiber optic* ambayo iliyoekezwa na kuzunguka ndani ya nchi kwa kutumia zaidi ya bilioni dola ishirini ambazo tayari hii Kampuni wanatumia kufanya biashara.

Lakini juu ya hapo katika hiyo hiyo Bodi ya *Zantel* tuna Wawakilishi wa Serikali ambao ni Makatibu Wakuu wetu na Kampuni hiyo hiyo ya *Zantel* hisa zake ambazo wanazozungumza katika huko nje walipotaka kununuliwa hiyo Kampuni ya *Zantel* miaka ya nyuma pamoja na *Vodacom.* na hiyo *Tigo* na kampuni nyengine walikaa kuuza kampuni kwa sababu tayari wao walikuwa wanatengeneza pesa. Sasa leo tunaambiwa Kampuni ya *Zantel* ilikuwa mambo yao sio mazuri.

Nataka kufahamu kwa muda wa miaka mitatu katika siku zote hizi nne tangu nilipoleta hoja yangu siku ya Alhamis mchana nilipochangia. Nilitaka kujua ni kiasi gani cha fedha Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imeikosa, kama hana hizo taarifa basi tujue ni kiasi gani fedha za Zanzibar hazijapokelewa, hilo ndilo suala langu.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, naomba pia niseme kama nilivyosema wakati najibu lile suala lililopita. Ni kwamba tunagusa

vifungu hivi ambavyo havimo hayo masuala yayayozungumzwa. Kwa sababu masuala ya *Fiber optic* hapa haijazungumzwa. Kwa hivyo, anagusa kifungu kingine.

Lakini pamoja na hayo nilieleza pale wakati natoa majibu yangu kwamba bado hatujaweza kufaidika kutokana na mkataba ulioingia *Zantel* na SMZ na kutokana na sababu kwamba ilikuwa kukamilishwe zile *infrastructures,* ni jukumu moja la *Zantel* wakamilishe ile *infrastructure* kwa maana ya *loop* ya Dar- es-Salaam Unguja kupitia *Sub-marine table*, lakini pia Dar-es-Salaam - Tanga na kuunganisha ile Tanga *Sub-marine*, inayokwenda Pemba lakini na kwa kutumia *Micro wave* iliyoopo Unguja kwenda Pemba, hiyo haikufanyika.

Lakini kutokana na hiyo *infrastructure* haikukamilika na tulichotakiwa kufanya ndani ya mkataba ule kugawana matumizi kama ile *infrastructure* ingekamilika na matumizi hayo ilikuwa tupate sisi SMZ kwa maana ya taasisi zetu ziunganishwe. Lakini vile vile ilikuwa wao *Zantel* wanufaike lakini ziada ya hapo ndio uizwe. Sasa ile ziada ndio iliokuwa igawanywe kwamba ni mapato ya kugawanywa baina ya SMZ na *Zantel*.

Sasa hayo hakuwepo, kwa hivyo, hakuna kitu ambacho tunaweza tukamjibu kwamba kuna mapato ya kiasi gani yangekosekana kwa sababu kwanza pia tulikuwa hatujui ni zaida gani ambayo ingekuwepo ya kuuza kwa hizo Kampini za Mawasiliano. Naomba kujibu hilo.

Mhe. Simai Mohammed Said(Mpakabasi): Ahsante Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mwenyekiti, ukisoma katika Hotuba ya Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango 2013/14 kwenye ukurasa wa 74 amesema kabisa kwamba;

"Mkataba wa *Zantel* umetiwa saini tokea mwezi wa Februari mwaka huu na kwa sasa matayarisho ya mwisho ya utekelezaji yamekamilika"

Mhe. Mwenyekiti, naomba nirudie tena hii ni mwaka 2013, lakini hata hivyo serikali imeekeza hii *Fiber optic* ambayo ilikuja ikaomba hizi fedha na ikenda ikakopa zaidi ya bilioni arubaini, wamesema kiasi cha milioni ishirini dolla. Ilipokuja hapa Wizara ya Katiba na Sheria tukazungumza hapa kwenye suala la *E-government* na tukaondoka hapa saa 4:30 usiku na serikali ilisema bado kuna mpango wataendelea kuhakikisha kwamba hili suala la *component* la *E-government* itakamilika.

Lakini katika hii *Fiber optic* kuna *components* mbili, asilimia 10 ilikuwa iende ambayo watatumia serikali, asilimia 90 ilikuwa serikali itafanya biashara kwa

kutumia mkataba na kampuni ya *Zantel*. Leo serikali inakiri kwamba kwa muda wa miaka mitatu hawajapokea fedha hata shilingi moja, wanasema kuna mambo hayajakamilika, sawa. Lakini pia Kampuni ya *Zantel* inatumia hii *Fiber optic* kuuza *bandwidth* kwa Kampuni ambazo za *ISP (Internet Service Providers),* sitaki kutaja majina yao, nitakuwa ninatuhumu watu ambao wanawalipa *Zantel,* lakini *Zantel* hawawalipi serikali na hizi kampuni zipo, sitaki kutaja majina yao.

Lakini kuna kampuni nyengine ambazo pia ni za *Network* wanatumia hii *Fiber optic*. Lakini tumezungumza hapa kwamba Taasisi za Serikali zilikuwa zipatiwe hizi *Internet.* Mhe. Mwenyekiti, Mashirika ya Serikali mpaka leo wanatumia kampuni za binafsi kwenye *internet*. Hasa...

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa, lete hoja yako.

Mhe. Simai Mohammed Said (Mpakabasi): Mhe. Mwenyekiti, swali ni kwamba kama Mhe. Waziri, ikiwa hataki kunambia kwamba ni fedha kiasi gani hawajapokea basi atwambie fedha kiasi gani basi tumekosa, ni kiasi gani lazima kwamba kila mwaka bajeti wanaweka na mwaka jana waliweka bajeti ya bilioni nane.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa, umemaliza.

Mhe. Simai Mohammed Said(Mpakabasi): Kidogo bado samahani Mhe. Mwenyekiti, bado sijamaliza.

Mhe. Mwenyekiti: Si ushauliza swali.

Mhe. Simai Mohammed Said(Mpakabasi): Naomba unifahamu kila mwaka serikali inawakaguzi wake inapita katika taasisi zake, inajua ni kiasi gani cha fedha zinapatikana, mikataba kiasi gani inatakiwa ifanyiwe kazi, ni kwamba huu mkataba huu mkataba wa mwaka 2013/14/15/16 tuko hapa hatujui basi kiasi gani, hata shilingi moja hatujui jamani!

Mhe. Mwenyekiti: Umemaliza haya. Mhe. Waziri, jibu.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, majibu yangu yatakuwa hayana tafauti na yale niliyosema mwanzo. Na hapa naomba tutafautishe kwa sababu kwanza hii Kampuni ya *Zantel* na sisi Serikali SMZ ina hisa zake asilimia 15 na wenzetu sasa hivi *Mil. com* wana hisa asilimia 85.

Kwa hivyo, kama zipo faida tunagawana pia kwa faida hiyo hiyo ya asilimia thamanini na tano na kama kuna hasara basi ni hivyo hivyo.

Alilolizungumza Mhe. Simai Mohammed Said, ni ule mkataba ambao tumefunga na Kampuni ya *Zantel* kwa ajili ya kutumia mkonga wa mawasilisono *'Fiber Optic Network'* hiyo ndiyo tunayoizungumza na kwa mujibu wa mkataba kwenye *Annex* kuna mambo ambayo ndani ya mkataba huu yalipaswa yatolewe na SMZ. Lakini vile vile na kuna *obligation* za kampuni hii na moja ya *obligation* ya kampuni hii ndio hiyo sasa *infrastructure*, lakini vile vile kuweka ***LAN Connectivity*** ya mawizara na Taasisi za Serikali 84, hiyo ilikuwemo na ndani yake sasa ndio tungeweza na sisi kufaidika kwa maana ya *E-government* ndio sehemu ya matumizi ya serikali na wao *Zantel* wangelinufaika kwa upande wa matumizi yanayotokana na mkonga huu.

Lakini ile ziada tungeweza kuuuza, lakini hicho kitu hakijafanyika na kama hakijafanyika hakuna *capacity* inayoweza kuuzwa kwa kampuni binafsi hakuna mapato. Sasa hata tukisema vyengine vyovyote bado suala litakuwa Mhe. Mwenyekiti, hakuna mapato tuliyokusanya kutokana na matatizo haya.

Lakini niseme tu kwamba hivi sasa ziko dalili nzuri sana za kuimarika kwa utendaji wa Kampuni ya *Zantel* na tunakusudia kukaa pamoja kuutizama upya mkataba huu na vile vile tutatizima sasa kipi kinachoweza kufanyika katika hatua za hivi karibuni. Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mhe. Simai Mohammed Said(Mpakabasi), ni mara ya mwisho nakupa nafasi.

Mhe. Simai Mohammed Said(Mpakabasi): Mhe. Mwenyekiti, tungekuwa tushamalizana, lakini majibu bado sipati, tatizo leo ni wiki ya pili.

Mhe. Mwenyekiti, mimi tatizo langu natafuta pesa, hizi fedha ni kiasi gani lakini bado naambiwa fedha hakuna. Sasa kutokana na kwamba majibu yanayotoka serikalini ni kwamba mkataba umefungwa na Kampuni ya *Zantel* kwa muda wa miaka mitatu. Serikali imetumia dola milioni ishirini hakuna *return* wanazozipata kutoka *Fiber optic* kwa kutumia kwenye *E-government*, hakuna *return* zilizokuweko katika taasisi za kutosha kupata hiyo huduma ya *internet*.

Lakini pia hakuna fedha ambayo Kampuni ya *Zantel* inatumia *Fiber optic* ya wananchi iliyotumika zaidi ya milioni ishirini. Sasa mimi nilikuwa na suala

moja kwa Mhe. Waziri, kwa kuwa serikali imeshaamua kutoa huduma za bure kwa kutumia hii *Fiber optic* na mimi ningeomba kwamba Wajumbe wa Baraza wote wapatiwe *Internet* ya bure majumbani kwao na kwa wananchi wao wote kwa pamoja.

Sasa naomba Mhe. Waziri, je, atatutekelezea kwa hilo kwa pamoja.

Mhe. Mwenyekiti: Hiyo ni *opinion* yako wewe, usihusishe na wengine.

Mhe. Simai Mohammed Said(Mpakabasi): Sasa Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa hatujui kiasi gani cha fedha tunapata kwa hiyo huduma na tayari kuna Kampuni za *internet* zinatumia hii *Fiber optic* na wana-*advertise* katika mitandao yao kwamba sisi kampuni fulani *so and so*, tumeungana na *Fiber optic* hii kutoka Dar-es-Salaam mpaka hapa halafu tunauza kiasi fulani tutakuletea hii *speed* kadhaa. Je, utatulipa kiasi gani wanauza dola 40 - 50 hawa ni kwenye *retail.*

Sasa ina maana *Zantel* anafaidika kwenye mfumo huu, lakini serikali kwa vile haitaki kupata fedha zake mimi sina maneno tuendeleeni.

Kifungu SF010102	Programu ndogo ya Usimamizi wa Hesabu za ndani	720, 881,000
Kifungu SF010103	Programu ndogo ya Usimamizi wa Bajeti ya Serikali	23,123,476,000

Kifungu SF010104

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia nilieleza namna ya fedha za umma zinavyopotea wakati wengine bila ya sababu za msingi na nilijaribu kuzungumzia hoja ya hii miradi ambayo inayofanywa na serikali ambayo maamuzi yake hayako katika taasisi moja na pamoja Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, alieleza kwamba wizara yake hii kuna baadhi ya hoja tulizozizungumza ziko katika wizara nyengine. Lakini pia tujue kwamba hizi wizara nyengine wao wanasimamia tu miradi lakini fedha zinatoka Wizara ya Fedha.

Sasa katika eneo hili nilizungumza kuhusu ujenzi wa hizi barabara na nikatoa mfano zile zinazosimamiwa na Mfuko wa barabara na pamoja na kwamba Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu, alitoa ufafanuzi lakini nilikuwa namuomba sana Mhe. Waziri wa Fedha, ile hoja yangu akajaribu kufanya

utafiti ni kiasi gani za fedha ambazo zimelitumika zingelikuwa kama kungekuwa na mashirikiano mazuri zisingeweza kupotea kiasi kama hicho.

Sasa hapa nilizungumza hukusu suala la mjenzi aliekuwa amejenga barabara ya Wete-Gando na Wete-Konde, kule Mhe. Mwenyekiti, kuna fedha ambazo zinapotea bure bure na hapa Mhe. Mwenyekiti, ule mradi unafadhiliwa na fedha za nje ni *BADEA* na ndio hapa fungu hili kuratibu kushughulikia fedha za nje. Lakini hizi fedha za nje huwezi ukazipata bila ya kwanza kutumia fedha za ndani ambazo moja kwa moja hazitoki Wizara ya Mindombinu ila zinatoka Wizara ya Fedha.

Sasa leo kuna madeni ambayo zaidi ya miaka mitatu au miaka mitano hayajalipwa na leo tunapiotisha bajeti hii. Mhe. Waziri, juzi alizungumzia kwamba anafanya utafiti na kujua na kujiridhisha kama hizo fedha ziko halali ataweza kulipa. Sasa labda kwa kuwa zaidi ya wiki alivyojibu hili suala, sijui utafiti wake umefikia wapi ili tujue kwamba hizi fedha zitalipwa lini ili kuzuia kuongezeka tena na riba. Kwa sababu hizi fedha zinalipwa zina riba ili kuzuia hii riba isije ikaongezeka, naomba maelezo.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Mhe. Hamza Hassan Juma, alizungumza suala hilo na nilisema kutokana na zile barabara ambazo amezisema za Wete-Gando na Wete-Gonde ni kweli yapo madai hapa ya yule mkandarasi lakini kuna historia kubwa sitaki kuisema historia hiyo yote hapa.

Katika madai hayo sisi Wizara ya Fedha yako madai ambayo tunahisi ambayo yanapaswa kulipwa. Lakini yako mengine tunahisi yanahitaji kufanyiwa uchambuzi(uhakiki) zaidi na ndilo tulililoliomba na kazi hiyo tunafanya. Mimi mwenyewe binafsi nimepata kuzungumza nae mmiliki wa kampuni hii hivi karibuni tu nimepata maelezo yake. Lakini pia tunataka kukaa na wizara inayohusika na masuala ya ujenzi nayo kuona nao upande wao wana maelezo yepi. Tutakaa pamoja na watendaji wangu ili kuona kwenye yale mambo ambayo tunawasi wasi basi tunatizama kwa kina kwa pamoja na tunakubaliana.

Lakini niseme kwamba pamoja na yote haya mahusiano ya mkadarasi huyu na serikali ni mazuri na ndio maana bado serikali inaendelea kumuamini na kumpa kazi nyengine. Kwa hivyo, hakuna jambo la kutia wasi wasi, ni jambo la kukaa pamoja na tutaangalia. Zipo gharama ambazo tunaziona zimesidi sana kutoka zile gharama za mwanzo na madai ya sasa hivi ambayo lazima tufanye uhakiki, maana yake yako maeneo ambayo yamezidi kutoka labda milioni tisa mpaka milioni mia nne. Sasa jambo hilo ni lazima ukae uliangalie

ulichukunguze kwa kina kabla huja-*commit* fedha za umma kwa maana ya kulipa bila ya yeye mwenyewe kujiridhisha.

Hicho ndicho tunachokifanya sasa hivi. Namuomba Mhe. Hamza Hassan Juma, akubaliane na mimi, anipe muda kazi tunaifanya na tunaifanya kwa mashirikiano na maelewano na kwa namna hiyo halitotokea tatizo lolote. Ahsante. (*Makofi*)

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema Mhe. Waziri, mimi namuamini sana na kwa kuwa huyo muhusika ameshaonana nae bila shaka hiyo kadhia itakuwa imeshafika pahala husika. Sasa labda tu nilikuwa nina ushauri kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, miongoni mwa pesa hizo kumeongeza fedha za *interest* kutokana na *delay of payment* na Mhe. Waziri, ili hiyo *delay payment* isiendelee nilikuwa namuomba tu basi hayo madai ambayo ameyaona ni *genuine*, mimi nafikiri yangelipwa kwanza ili kumpunguzia panda shuka yule *contractor* na hayo mengine ambayo yanahitaji kukaa kuyakagua mimi nafikiri wakae wayakague ili kuondoa hiyo sintofahamu.

Kwa sababu haipendezi kwamba *contractor* huyu wao kama anavyosema wana mahusiano mazuri. Kama mna mahusiano mazuri huyu mtu angekuwa anapita analalamika, kwa kweli keshafika mpaka serikalini kwa kiongozi mkuu wa shughuli za serikali bado anaendelea kuzunguka. Mimi nafikiri Mhe. Mwenyekiti, hayo malipo ambayo Mhe. Waziri, amesema wameshayaona ni *genuine* wamlipe basi hayo mengine waendelee na *negotiation* na kwa kuwa wanasema kwamba wana imani nae na wanaendelea nae basi ili na yeye asijisikie vibaya. Kwa sababu tatizo analolalamika anasema wageni wanalipwa ila mwenyeji halipwi na hao wageni kuna kazi wamefanya wameziacha wamekimbia na wameshalipwa, yeye kafanyakazi kamaliza hajalipwa, anaambiwa watu wana wasi wasi nae.

Mimi nafikiri Mhe. Mwenyekiti, umoja katika Taasisi zetu za Serikali tena hasa Wizara ya Miundombinu na Wizara ya Fedha kwa sababu hawa ni taasisi ambazo zinatumia pesa nyingi na zihitaji mashirikiano makubwa ile kuvutana kwao inaisababishia serikali hasara ambayo ilikuwa haina sababu.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa naomba tu labda hilo la ushauri wangu hayo *genuine* yafanywe nini na hayo mengine wakae kitako labda kwa taratibu za serikali Mhe. Waziri, anisaidie maelezo ili tupate kuendelea.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, naomba kueleza kwamba kwanza hakuna mvutano baina taasisi mbili. Sisi tunafanya kazi vizuri

kwa mashirikiano na kuelewana kama serikali. Lakini suala lake la kwamba kulipa hizi pesa ambazo ni *genuine*, sisi hatuna matatizo na kulipa pesa hizo. Kwa hivyo, hilo suala tunalichukua na ndiyo dhamira yetu hasa kwamba zile ambazo *genuine* basi tufanye tuandae utaratibu wa kuzilipa na zile ambazo tunakwenda kuzihakiki zaidi zifanyiwe uhakiki huo. Kwa hivyo, hilo halina tatizo.

Mhe. Mwenyekiti: Ninakushukuru Mhe. Waziri. Mhe. Hamza Hassan Juma, naona tuendelee.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa hili naomba tuendelee, tusubiri mengine huko baadae.

Kifungu FS 010104	Programu Ndogo ya Uratibu wa Raslimali za Nje	Shs.1,515,456,000/-
Kifungu PS 0102	Programu Ndogo ya Usimamizi na Uwekezaji wa...	

Mhe. Mwenyekiti: Tunaanza na Mhe. Simai Mohammed Said, tunakuja Mhe. Mussa Foum Mussa, baadae Mhe. Abdalla Maulid Diwani.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri aliyotoa Mhe. Waziri katika *summary* yake, nilikuwa na suala moja. Kwa kuwa Zanzibar sasa tumefungua milango yetu kwa ajili ya kuhakikisha kuwa wawekezaji wa ndani hasa na wa nje tunawatumia ipasavyo ili kujenga uchumi wetu. Kitengo ambacho maarufu tunakitumia sisi ni cha *Zanzibar Investment Promotion Agency (ZIPA).* Na katika majibu kama nilivyomuuliza Mhe. Waziri, ambapo matarajio ambayo tayari anayotarajia yeye na anayoyazungumza hayaendani na hali halisi.

Sasa mimi suala langu ni dogo. Suala langu la kwanza Mhe. Waziri, ninataka ahadi yako kwanza. Kwa kuwa tayari wawekezaji wa nje na wengi wa ndani wanapoteza matumaini katika kupata fursa na haki pamoja na matatizo yao, hiyo katika lengo ambalo serikali imekusudia la *One Stop Centre.*

Je, Mhe. Waziri, unanipa ahadi kwamba utalisimamia vizuri katika *restruction* ya *ZIPA* na pia kuleta matumaini kwa wawekezaji na kwamba katika muda wa miezi mitatu mpaka sita, hayo matumaini ya nje tutakapokuja kupata kikao cha Baraza kabla ya mwisho wa mwaka, tutakuwa tayari mabadiliko tunayaona.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, naomba kumueleza Mhe. Simai Mohammed Said, kuhusiana na hoja yake kwamba serikali inalielewa hili suala la *One Stop Centre* na lilikuwepo, lakini lilikubwa na changamoto kidogo. Na hivi sasa serikali kwa nguvu mpya imeunda Kamati ya Mawaziri, Kamati ambayo inaongozwa na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais na hivi karibuni tumekuwa na kikao kuzingatia suala hili.

Niahidi tu kuna kazi wamepewa wataalamu kuifanya kabla ya kikao chengine cha pili. Kwa hivyo. suala linashughulikiwa na linafanyiwa kazi katika ngazi hiyo.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, naomba Mhe. Waziri, wakati anatoa majibu tunakuwa hatumsikii vizuri, kwa sababu ninaona *microphone* yake ipo mbali na anapozungumza. Naomba kidogo angeekea mabuku hapo chini tupate kumsikia vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kama nimemsikia vizuri kwamba amekubali kuwa kuna Kamati imeundwa. Sasa katika mambo ambayo tayari wawekezaji wanapata kuna mambo madogo ambayo hayatakiwi kuleta usumbufu au sura mbaya kwa nchi yetu. Sijui masuala ya barua ya *work permit* wakipeleka, mambo madogo madogo kama haya inatakiwa yaondoke.

Mimi ninachomuomba Mhe. Waziri, kama amekubali kwamba atayashughulikia, mimi naomba tusipoteze muda tuendelee ila huko mbele matumaini hayo ambayo ananipa hapa ahadi iwe ya ukweli, kwa sababu tunamuamini yeye ni mchapaji kazi mzuri.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe.Waziri, amesema kwamba watalifanyia hilo kazi. Hivyo, muamini Mhe. Waziri.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Mwenyekiti, nimesema tuendelee nimekubali, ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Haya, naam! Mhe. Mussa.

Mhe. Mussa Foum Mussa: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, mimi nilipokuwa nikichangia nilizungumzia Hoteli ya Kiweni iliyokwisha Miani Mwambe. Na nikasema kwamba kwa mwekezaji wake wa mwanzo aliyokuwa nayo Mr. Ofen

walikuwa wananchi wa shamba lile walikuwa wanalipa dola mia moja na hamsini kwa wakati huo.

Baadae yule mtu alifilisika ikapewa mwekezaji mwengine na hapa Mhe. Waziri, kasema kapewa mwekezaji mwengine. Sasa wananchi wenye shamba lile tokea wakati huo mpaka hii leo bado hawajalipwa chochote. Sasa madai nilikuwa ninasema hivi kwamba, ikiwa kuna mwekezaji yeyote aliyepewa. Je, wale wananchi wenye shamba lile mbona sasa hawaendelei kulipwa. Na hivi sasa lile shamba limebaki tupu kwa sababu mabanda yote yamemalizika kuanguka hakuna kitu.

Je, Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri, hapa ananieleza vipi kuhusu hatma ya wale wenye shamba. Naomba majibu.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mussa Foum Mussa, suala lake kama ifuatavyo.

Kama nilivyoeleza kwenye maelezo yangu wakati ninafanya majumuisho ni kwamba kampuni ya mwanzo ilikuwepo katika eneo lile ni *Pemba Resources Limited*. Kampuni hii ndiyo iliyokuwa na makubaliano na wananchi kulipwa zile shilingi laki moja hamsini elfu kwa mwaka. Lakini kampuni hii ilifilisiwa na badala yake eneo hili hili walipewa *Elewana Africa* ambayo kampuni nyengine.Kampuni hii nyengine haikukubali makubaliano yale ya mwanzo. Wao walisema kwamba wangeweza kuwa-*retain* wale wafanyakazi waliokuwepo kwenye kampuni ile ya mwanzo, lakini pia wangetoa kitu kile kinachoitwa *social cooperative responsibility,* lakini siyo kwa masuala ya makubaliano ya ile laki moja na hamsini.

Kwa hivyo, yale makubaliano yalivunjika baada ya kampuni hiyo walitiliana mkataba nayo kuvunjika. Na kampuni hii nayo pia *lease* yao imeondolewa tulivyozungumza na sasa hivi eneo kubwa la sehemu hiyo lipo wazi, lakini kuna eneo dogo ambalo linatumika na hoteli nyingine *Pemba Lodge*. Sasa suala ni kwamba kampuni iliyokuwa na makubaliano na wale wananchi haipo tena na haifanyi kazi. Kwa hivyo, zile shilingi laki moja na hamsini hazipo tena.

Mhe. Mussa Foum Mussa: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nilivyomfahamu Mhe. Waziri, ni kwamba hilo eneo hivi sasa ina maana halina mwekezaji. Kwa hivyo, je, ni kusema kwamba wale wananchi wanarudishiwa eneo hivi sasa.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, ardhi ni mali ya serikali. Kwa hivyo, hilo eneo lilikuwa kwa mwekezaji na sasa linabaki kuwa ndani ya miliki ya serikali.

Mhe. Mussa Foum Mussa: Mhe. Mwenyekiti, tunajua hivyo kwa sababu hili shamba lilikuwa la wananchi na mulikuwa na vipando vyao vya kudumu. Na kwa wakati huo vipando hivyo vikaondolewa kwa sababu hiyo kwamba lile shamba lilikuwa linajulikana kuwa ni lao. Tunajua kwamba ardhi ni mali ya serikali, lakini mimi ninazungumza lile shamba lilikuwa la wananchi wa Shamiani baadhi yao ambao walirithi kwa wazee wao wa zamani.

Sasa ikiwa lile shamba haliendelezwi tena na wale watu waliokubaliana nao mwanzo. Kwa nini sasa wasirejeshewe shamba lao?

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, kwa kawaida utaratibu ulivyo katika uwekezaji kwamba mwekezaji anapopewa eneo mazao yaliopo pale na vitu vyote vilivyopo pale kwenye ardhi ile hulipwa fidia. Na ninaamini fidia hiyo ilitolewa kabla ya kuchukuliwa eneo. Sasa kama fidia imeshalipwa kwa wananchi, ardhi inabaki ni mali ya serikali na hilo sasa ni eneo la uwekezaji.

Kama pakitokezea mwekezaji mwengine basi serikali ina mamlaka na uwezo wa kumpatia mwekezaji mwengine eneo hilo. Kwa hivyo, haliwezi kurudi kwa wananchi hao, ndiyo utaratibu kwa sababu wameshalipwa fidia yao.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mussa Foum Mussa, la mwisho hilo.

Mhe. Mussa Foum Mussa: Mhe. Mwenyekiti, mimi ninataka niseme kwamba kuna utaratibu na hapo mwanzo ndiyo ikakubalika kuwa wale watu walikodisha shamba lao na wakawa wanalipwa mia moja na hamsini dola, kwa sababu lile shamba ni lao. Na sheria ya serikali ni kwamba watu wasiuze isipokuwa wakodishe. Ndiyo utaratibu na wao waliufuata.

Sasa hii leo hili suala halipo. Je, kile chao hawarudishiwi, lakini mimi ninadhani tusilumbane sana. Ninamuomba Mhe. Waziri, akubali kwamba hawa watu wake wa *ZIPA* na hawa watu wenye shamba hili na mimi tukutane basi hili suala lielezwe ili yapatikane mawasiliano. Kwa sababu si hivi itakuwa kuna utata kule.

Mhe. Mwenyekiti: Ninafikiri Mhe. Waziri, amelisikia hili na atalifanyia kazi. Tunaendelea.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe.Mwenyekiti, kunipatia fursa hii. Pamoja na ushawishi mkubwa sana anaotoa Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango na kunishawishi mimi niunge mkono hoja kwa sababu ile moja ninafikiri ndiyo mimi, lakini bado kidogo mpaka asilimia tatu nimezikamata.

Mhe. Mwenyekiti, nilizungumza juu ya suala zima juu ya shamba la mipira *Agro-Tec*. Shamba sasa hivi lina karibuni miaka minne ninafikiri halifanyi kazi. Kuna wananchi wetu pale wanadai pesa nyingi sana. Sijapata jibu wakati wa majumuisho yake Mhe. Waziri. Naomba ufafanuzi wake tafadhali.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, naomba kumueleza Mhe. Abdalla Maulid Diwani, kwamba wakati ninapofanya majumuisho nilitoa maelezo ya kina katika suala hili. Inawezekana Mheshimiwa, wakati ninatoa maelezo kwenye eneo hili alikuwa nje ya ukumbi lakini nilizungumza vizuri sana.

Na nikasema kwamba ni kweli *Agro-Tec* ime-*seize operation* zake karibu sasa hivi kwa miaka minne na yapo madeni ya wafanyakazi waliokuwa wakifanya kazi kwenye kampuni hii. Lakini vile vile nikasema kwamba *Agro-Tec* inadaiwa pia na taasisi mbali mbali za serikali ikiwemo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Tunawadai dola laki nne kwa sababu ya kodi ya kila mwaka ya dola laki moja.

Lakini vile vile kuna madeni ya *PBZ* ambao hawa watu wanadaiwa na *PBZ* na ninafikiri *PBZ* wenyewe wanadai karibu dola za Kimarekani hamsini elfu na ishirini na tano nukta tatu, tisa. Lakini pia wanadaiwa na wafanyakazi wa mashamba kwa upande wa Unguja wanadaiwa shilingi milioni mia moja na ishirini na sita, laki mbili na hamsini saba elfu, mia mbili hamsini na wafanyakazi wa Pemba wanadai shilingi milioni mia moja na tano, laki moja, kumi na tano, mia mbili na ishirini na tano.

Lakini wanadaiwa na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwenye ile michango ya wanachama shilingi milioni mia moja na ishirini na tatu, laki saba thalathini na tano elfu na kumi mbili. Na adhabu ya *ZSSF* kwa kuchelewa kulipa ni shilingi milioni ishirini na tatu, laki tano tisini na sita elfu, mia moja na kumi na saba.

Kwa hivyo, jumla baada ya kufanya *conversion* wanadaiwa karibu Dola za Kimarekani laki nne hamsini na nne elfu na ishirini na tano nukta tatu. Hili ndilo deni walilo nalo na tukasema kwamba wajibu wa kulipa deni hili ni wajibu wa kampuni yenyewe. Kwa sababu hata sisi tunamdai. Kwa hivyo, wao

ndiyo wenye wajibu na serikali italifanyia kazi kwa kufuatilia kwamba mwekezaji huyu analipa madeni yake kwa taasisi, lakini vile vile kwa wafanyakazi wanaodai kampuni hii. Hilo ndilo jibu nililolitoa.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kama ulitoa pale jibu ninashukuru sana na nikutake radhi kwa kusumbua kuniletea tena binafsi. Kwa sababu pengine moja au nyengine sijasikia ni kweli ilikuwa ni dharura.

Lakini ni kweli hii taasisi imefilisika na ninafikiri Wizara ya Fedha na Mipango ni watu ambao muliokuwa dhamana katika ile. Katika je, kuna *exhibit* gani ambacho cha kuweza kukamata ili wale wananchi wanaodai pesa zao wakaweza kupata. Kwa sababu wananchi wetu ni wengi ambao wafanyakazi waliofanya kazi pale zaidi ya miaka minne sasa, lakini bado hajatoa hatma.

Pamoja na majibu yake yote mazuri. Je, hawa watu ambao waliokuwa wafanyakazi wa pale wanaoidai ile kampuni wategemee nini kutoka kwako wewe kama Waziri wa Fedha.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, kwanza hatua ya mwanzo tuliyochukua ni kwanza kulirudisha shamba hili serikalini, mashamba yote yale yaliyokuwa yanahudumiwa na kampuni hii yamerudi serikalini kwenye mitaji ya umma. Hiyo ndiyo hatua ya mwanzo.

Na hatua ya pili nimesema kwamba tutalifuatilia suala hili na kwa mujibu wa taratibu za kisheria kuona tunafanya nini ili fedha zinadaiwa na kampuni ile ili ziweze kupatikana.

Mhe. Mwenyekiti, siwezi kusema hapa ni lini, lakini nimuahidi kwamba tunalifanyia kazi.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Sawa Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana Mhe. Waziri, kwa vile Dkt. Khalid Waziri wa Fedha na Mipango wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ni *doctor* ambaye ninakuamini sana na katika watu ambao ninaowaamini asilimia mia moja, mmoja ni wewe, basi ninakubali na tuendelee.

Kifungu PF 0102 Programu Kuu ya Usimamizi na Uwekezaji wa Mali za Umma Shs.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa, subirini kwanza. Hii hatujamaliza, hatujapitisha kifungu ile ambayo tumeizungumza bado hatujapitisha. Tuacheni tupitishe halafu tena ndiyo mutapiga buti.

Kifungu PF 0102 Programu Kuu ya Usimamizi na Uwekezaji wa Mali za Umma

Shs.6,606,238,000/-

Kifungu SF 010202Programu Ndogo ya Usimamizi

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Abdalla Ali Kombo na baada ya hapo ni Mhe. Hamza Hassan Juma.

Mhe. Abdalla Ali Kombo: Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima yako mimi niliwahi kuuliza suala la nyumba ya Makunduchi.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri, ninamjuulisha kuwa sitokuwa na ulimi wa ng'ombe, msimamo wangu ni kupitisha bajeti wala sitoisimamisha, msimamo wangu ni kuipitisha. Lakini na maelezo yake mazuri sana bado sijaridhika.

Ninachoomba kama kuna uwezekano hii mikataba, hii ni mali ya serikali na ni nyumba kubwa tu ambapo mpaka Marais walikuwa wanakaa. Sasa ninachokitaka mimi Mhe. Mwenyekiti, kama kuna uwezekano hii mikataba kwa sababu siyo siri, ile nyumba ipo barabarani ipo nje. Ningemuomba Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, tukaiona hii mikataba ama barua za serikali, barua halali na mwenyewe *NGO* na *NGO* ambaye ni halali.

Mhe. Mwenyekiti, *NGO* zina taratibu zake, zimesajiliwa, watu wametia saini na kila kitu. Ningependa kuona *NGO* halali na siyo idadi ya watu. Hilo ndilo suala langu na ninamuomba Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri, anijibu.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjuulisha Mhe. Abdalla Ali Kombo, kwamba mkataba huo uliofungwa nao, nitakaa naye na hata barua ambazo tumeandikiana zipo, tutakaa naye na tutalizungumza hili. Lakini ni kitu ambacho kama nilivyosema kwamba kimetoka kihalali. Wizara ya Fedha iliiruhusu wizara inayohusika na Wizara ya Kazi na Utumishi wa Umma litoe eneo hilo kufuatia maombi yaliyoletwa serikalini na Mwakilishi wa jimbo hilo na serikali kuridhia jengo hilo litolewe kwa ajili ya matumizi hayo mema ya kuwasaidia vijana kuweza kupata fursa za ajira.

Mkataba upo wazi kabisa, una *conditions* zake zinazoelekeza *NGO* iliyopatiwa jengo hilo ilitumie vipi na kufanya marekebisho katika jengo hilo. Kwa hivyo,

ni kitu cha halali na kipo wazi na nitazungumza naye na tutazidi kueleweshana nje ya Baraza, Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Abdalla Ali Kombo: Mhe. Mwenyekiti, nimemsikiliza uzuri Waziri wa Fedha na Mipango. Ningemuomba mimi na yeye wakati kiongozi au mtu yeyote amechukua hii mali, kwa hivyo, sitotizama kwamba ni waziri ama ni nani. Ningeomba na yeye awepo na *NGO* yake iwepo.

Yeye aliyechukua mali ya serikali, Waziri wa Fedha kwa niaba ya serikali na *NGO* iwepo. Mhe. Mwenyekiti, nina uzoefu wa eneo la Makunduchi, kuna viongozi wanakwambia huu ni mradi wa serikali au ni mradi wa wananchi, inafika wakati anamuonesha mpaka Rais huu ni mradi wa wananchi. Kwa macho yangu shahidi nimefunga, kumbe sio wa wananchi. Kumbe mradi unaoneshwa huu wananchi wamehusika pesa za serikali zinatumika, lakini hakuna kinachofanyika.

Mheshimiwa wasi wasi ndio maisha ya binadamu. Hii Dakhalia sijui katika nyinyi kama mnaijua. Hapana mwanafunzi anayesoma Makunduchi kulala kule. Wasiwasi wangu isije kuwa hoteli ambayo haina njia yoyote iliyopitwa ikawa wawekezaji wanalipa pesa, lakini kuna watu wanachukua mambo haya bure, serikali naomba iwe macho. Kwa mara yangu ya mwisho tuendelee lakini Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, Mkuu wa Mawaziri anayehusika na *NGO* naomba tuonane na Waziri wa Fedha.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, Mhe. Mjumbe anataka kujua lini mtaonana. Nafikiri hilo ni suala la kupanga baina yako wewe na yeye. Mhe. Mjumbe, mmekubali tuendelee. Nafikiri mtapanga Mhe. Mjumbe, pamoja na waziri.

Mhe. Abdalla Ali Kombo: Sina matatizo. Tupate muda wa kuonana na *NGO* halali na aliyechukua kasema barua zote za nyuma ziwe halali. Kama sio halali Mheshimiwa kikao kinachokuja Mwenyezi Mungu akipenda hapa patakuwa sio pazuri. *(Makofi)*

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, mimi ninasikitika sana kwamba kutokana na upya wa waziri, kwa kweli watendaji wake hawakumtendea haki, kwa sababu nilihoji ule mradi ambao mwekezaji mzalendo na majibu yake alisema kwamba ule mradi uko katika eneo la utalii, ule mradi wa chelezo.

Kwa kweli hilo suala sio kweli hata kidogo, isipokuwa na nafikiri Mhe. Waziri tutamchosha kweli, maana yake kila mtu anataka aongozane naye. Sasa

nitakiruhusu hiki kifungu kiendelee, lakini nitamuomba tu Mhe. Waziri kwa wakati wake muafaka tuje tufuatane baina ya mimi Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira na yeye Waziri wa Fedha na Mipango pamoja na *ZIPA*, pamoja na Idara ya Mazingira ili twende tukaangalie hilo eneo, kweli ni eneo la utalii, hivyo tu nilikuwa nataka hii *message* Mhe. Waziri aijue, basi tuendelee, wala sisimami.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, anataka kauli yako, kama utakubali kwenda naye.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, naomba nimuhakikishie kwamba niko tayari na nitatembelea eneo hilo na wala asione huruma. Mimi kutembelea maeneo ndio kazi ninayoipenda zaidi kuliko kukaa ofisini, kukaa kitako kunachosha.

Mhe. Mwenyekiti: Tuendelee.

Kifungu SF010202	Programu Ndogo ya Usimamizi wa Manunuzi na Uhakiki Mali za Serikali	161,345,000
Kifungu PF0104	Programu Kuu ya Mipango na Uendeshaji Sekta ya Fedha	
Kifungu SF01		

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Masoud Abrahman Masoud, baada ya hapo Mhe. Miraji Khamis Mussa, kisha Mhe. Hassan Khamis Hafidh.

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri kwa Waheshimiwa Wajumbe.

Mhe. Mwenyekiti, wakati nachangia kwa maandishi nilimuuliza Mhe. Waziri, kwa bahati nzuri kabla ya kuingia kwenye Baraza mimi nilikuwa ni Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi.

Halmashauri yetu fedha yake yote inayokusanya inapeleka Benki ya *PBZ*, na natumai Halmashauri nyingi zinapeleka kwenye benki hiyo. Kwa bahati nzuri sisi kila mwaka wastani huwa tunakusanya karibu bilioni moja kupeleka Benki ya *PBZ*. Tulikaa kwenye kikao chetu cha Baraza la Madiwani, tukaamua tukakope benki ya *PBZ* shilingi milioni 150. Wakatupa masharti waliotupa tukayatimiza yote na wakatwambia kuwa itabidi kila mwezi tuwalipe shilingi milioni tatu, kwa hizi shilingi milioni 150 kwa muda wa miaka mitano itakuwa

deni hili tutamaliza. Tulifanya makubaliano yetu haya kwa sababu serikali sisi haitupi ruzuku ya kununua magari kwa ajili ya ukusanyaji wa taka kwenye maeneo mbali mbali. Lakini kwa bahati mbaya mpaka leo Benki ya Watu wa Zanzibar haijatukopesha hizi fedha shilingi milioni 150. Kwa hivyo, ninalomuomba Mhe. Waziri atwambie, je, Benki ya Watu wa Zanzibar haitaki kwa makusudi kuikopesha Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi, au hakuna utaratibu wa Halmashauri kukopeshwa pesa na Benki ya *PBZ*.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Mhe. Masoud Abrahman Masoud aliuliza kwenye mchango wake wa maandishi, na bahati mbaya sikuweza kulitolea ufafanuzi, lakini naomba tu aelewe kwamba *PBZ* haina dhamira ya kuwakopesha mkopo Halmashauri yoyote. Inawezekana pengine utaratibu haukukamilika, na utaratibu kwa vile Halmashauri ni taasisi ya serikali, ni lazima maombi hayo pia, kwa sababu hawa wanapata ruzuku kutoka serikalini, kwa hivyo ni lazima wapate ruhusa kwanza kwa wizara husika, lakini vile vile na serikali, sio serikali kwa maana Wizara ya Fedha na Mipango nayo ijulishwe, ili kujua kwamba kuna dhima ya mkopo huu ambayo inachukuliwa na Halmashauri.

Naomba tukutane baadae tufahamishane utaratibu huo, naamini kabisa baada ya kukamilika utaratibu huo basi *PBZ* itakuwa kwenye *position* ya kuweza kutoa mkopo huo.

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: Mhe. Mwenyekiti, nimshukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri. Lakini niseme tu kuwa taratibu za kupita wizarani tumepita na Katibu Mkuu wanalielewa suala hii, na ndio maana baada ya kupata barua kutoka wizarani walitupa haya masharti na tukayakubali. Lakini kwa bahati mbaya ndio mpaka leo hatujapata mkopo huo.

Mhe. Mwenyekiti, ninaloliomba, je, inawezekana hizi Halmashauri kuweza kuhamisha *account* zao, kwa sababu wana masharti magumu *PBZ* ya kutoa mikopo ili tukahamishia kwenye benki nyengine za *NMB* au *CRDB*, kwa sababu kule tutaweza kupatiwa mkopo.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, naomba Mhe. Masoud Abrahman asifikirie kuondosha *account PBZ*, ni taasisi ya serikali. Lakini kama nilivyomueleza kwamba tutakaa tutauangalia huo utaratibu uliofanyika na tutafanya mawasiliano na benki husika ili kuona vikwazo viko wapi na tuvifanyie kazi vikwazo hivyo. Kwa hivyo, naomba niamini tukimaliza bajeti hii tutakutana na tutalifuatilia suala hilo kwa nia ya kulitatua tatizo hilo.

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri na ushauri wake. Lakini kwa sababu Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ pale katikisa kichwa, inaonekana yeye atakuwa yuko karibu zaidi kumshauri Mhe. Waziri na watu wa benki ya watu wa Zanzibar kupatiwa mkopo huo, ili Halmashauri yetu iweze kupata hizo fedha na kwenda kununua magari kwa ajili ya kubebea taka, kuweke usafi mji wetu au Manispaa yetu ya Magharibi A na B.

Mhe. Mwenyekiti tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Tunaendelea. Mhe. Miraji Khamis Mussa.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi nina swali moja dogo tu. Wakati ninachangia Chuo cha Uongozi wa Fedha Chwaka, niliwahi kumwambia tu waziri kuna baadhi ya watendaji pale wanafanya kazi wanazidi muda wa ziada ule wa utumishi uliowekwa kwa mujibu wa yale masaa ya kisheria. Ukizidisha muda unatakiwa ulipwe *over time*, sasa hazitoki kwa watendaji hawa.

Kwa hivyo, nataka atakapokuja anijibu hatma ya wafanyakazi hawa ambao wanapitiza ule muda na wanakosa stahiki zao, lakini hakunipa majibu. Kwa hivyo, naomba asimame anipe utaratibu ambao watapata haki zao hawa watumishi wa Chuo cha Fedha Chwaka.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Mhe. Miraji Khamis Mussa aliliuliza swali hilo, lakini sikupata nafasi ya kulitolea maelezo. Lakini nimueleze tu kwa mujibu wa kanuni za Utumishi wa Umma, wafanyakazi ambao hawako katika ngazi ya uteuzi wa Mhe. Rais wanapokaa na kufanyakazi baada ya masaa ya kazi ya kawaida, basi wanastahiki kulipwa *over time* zao. Kama hilo tatizo lipo na ameshanijulisha basi tutawasiliana na uongozi wa chuo ili kuona ni utaratibu gani unatumika ili kusawazisha madeni ya wafanyakazi hao kwa sababu hiyo ni haki yao.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Tunaendelea Mhe. Hassan Khamis Hafidh.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipochangia niligusia kuhusu wizi wa fedha za Mfuko wa Wafanyakazi na kidogo niligusia kuhusu mishahara hewa.

Mhe. Mwenyekiti, nakubali Mhe. Waziri wa Fedha ni waziri mpya, na nilipotoa mchango wangu nilisema kwamba ndani ya serikali hii kuna watendaji ambao hawaitakii mema Serikali hii ya Mapinduzi inayoongozwa na CCM. Kwa kauli ya kujiamini kabisa, *with full confidence*, napenda kumwambia Mhe. Waziri kwamba ndani ya wizara yake anayoiongoza, wapinga maendeleo hao wamo wezi.

Kwenye mishahara hewa kwenye huu mfuko wa wafanyakazi nitampa mfano, kuna *transaction* moja imetoka pesa imetiwa, halafu baada ya siku tatu imetolewa. Yeye *PhD holder* kazi hii nampa yeye akafanye *research* ya haya ninayosema, halafu kama kashindwa kupata *funds* anijie mimi nitampa baadhi ya vitu vya kumsaidia. Ninayasema haya kwa ushahidi, lakini kabla sijatoa *documents* zangu nilizonazo, namwachia yeye kwanza akafanye utafiti.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuongezea, wizi huu unanikera na unaniudhi, lakini namuamini na ni mwanamapinduzi, ni mtoto wa mkwezi na mkulima akalifanyia kazi, kama kashindwa aje. Ninachoheshimu kwamba ni Serikali ya Chama cha Mapinduzi, lakini Mhe. Waziri hivi unavyoniudhi kama ingekuwa ni chama cha upinzani kinaongoza nchi hii basi ningewaita waandishi wa habari nikatoa ushahidi nilionao. Lakini Mhe. Waziri namjua ni jembe, naheshimu Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kwa sababu na mimi ni sehemu ya hiyo, bado namuachia Mhe. Waziri akafanye kazi hiyo.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, toa hoja kama una swali uliza au kama una hoja. Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mhe. Hassan Khamis Hafidh. Nataka nimuhakikishie kwamba hivi sasa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Mahesabu, keshaanza kupita katika wizara mbali mbali na kuangalia zaidi suala zima la watumishi hewa. Tumeanza na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali tayari na Kikosi kazi cha Mkaguzi na Mdhibiti wa Hesabu sasa hivi kinaelekea Pemba katika Wizara hiyo hiyo ya Elimu na Mafunzo ya Amali, wakitoka huko wataendelea kwenye sekta nyengine au wizara nyengine. Hatimaye ripoti italetwa hapa tutaijadili.

Kwa hivyo, tutamuomba Mhe. Hassan Khamis wakati huo aje aichangie vizuri sana, na kama anazo taarifa za ziada sasa hivi na ushahidi basi atusaidie, ili pale ambapo pana matatizo tukawapeleka wakaguzi wetu, tukamwambia Mkaguzi na Mdhibiti aende pale kwanza akafanye kazi yake ili tuanze kurahisisha hii

kazi. Kwa hivyo, asiwe na wasi wasi, serikali iko makini na yeye najua ana uchungu sana wa nchi hii na *In sha Allah* tutafanya hivyo.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango pia anipe ufafanuzi kuhusu wizi wa fedha za mfuko wa wafanyakazi.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba Mhe. Hassan Khamis tusiwaite hawa wafanyakazi wizi, kwanza ni tuhuma, pengine kuna tuhuma. Hii tuhuma mimi naikubali naichukua kwamba tutakwenda kuifanyia kazi ili kujua kama kweli watu wanapoteza fedha hizo kwa sababu ya wizi au kitu chengine. Kwa hivyo, sasa hivi ni tuhuma ambayo naikubali na nimeshaichukua, tutaifanyia kazi na pia nitaonana naye ili kupata maelezo ya ziada yatakayonisaidia katika upelelezi wangu wa kupata kujua kwamba kweli kuna tuhuma ya namna hiyo katika ofisi.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, nimesikia lakini nilikua nasubiri kama ataniambia nifute kauli yangu ya wizi, lakini hakusema kwa maana hakuna kufuta, kwa sababu nisingefuta, lakini hakuniambia. Kwa hivyo, naomba tuendelee maneno yangu ameyasikia na ameyafahamu. Bado nasisitiza hawa watu ni wezi kwa sababu nina ushahidi. Ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Tunaendelea. Mwanasheria Mkuu.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, kama ambavyo Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango amejibu, na kama ambavyo Mhe. Hassan Khamis Hafidh amesimamia hoja yake, ni kwamba kinachozungumzwa hapa ni kama kuna tuhuma, na kama Mhe. Hassan Khamis anavyojua mtu anakuwa hana hatia mpaka anapotiwa hatiani, kila mtu yuko huru hana hatia mpaka anapotiwa hatiani.

Sasa tuhuma zake Mhe. Hassan Khamis, Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango amesema amezipokea atazifanyia kazi, na hao watu kama wanatuhumiwa watachunguzwa, halafu vyombo vitafanya kazi yake. Kilichokuwepo sasa hivi ni tuhuma, na hawa watu kwa mujibu wa sheria zetu ni kwamba wako *innocent till proving otherwise* Mhe. Mwenyekiti nakushukuru. *(Makofi)*

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mhe. Mwanasheria Mkuu kabobea sheria kwa kuwatuhumu wezi hawa. Ahsante.

Kifungu SF010401 Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji wa Wizara 4,923,355,000

Programu Ndogo

Mhe. Simai Mohamed Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa serikali imeazimia kwenda katika mambo na mpango wa kisasa na pia kwa siku za mbele kuanza kutumia mashine za *electronic system devices* kwa ajili ya kukusanya mapato, na hatuna shaka kwamba Mkoa wa Mjini ndio utakaokuwa mkoa ambao unaingiza mapato ambayo yanategemea na kufunga mashine nyingi.

Mhe. Mwenyekiti, swali langu ni moja tu. Nataka kufahamu, katika mchango wangu nilizungumzia suala la *fiber optic*. Nilisema nataka kufahamu kwamba wakati Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji inatengeneza barabara ya kutoka Mwanakwerekwe kwenda Fuoni, kwa makusudi au kwa bahati mbaya *fiber optic* ambayo imegharimiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na ililipiwa pamoja na Wizara ya Fedha na Mipango, inayotoka Mwanakwerekwe kwenda Fuoni.

Je, ni kiasi gani cha fedha katika ile *fiber optic* itahitajika ili kutengenezwa, na nani atalipa hiyo *fiber optic.* Je, ni Kampuni ya Zantel, serikali au nani.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, niliwahi kujibu swali hili hapa la Mhe. Simai Mohamed. Tulisema na kuahidi kwamba suala la kuharibika kwa mkonga kutokana na ujenzi wa barabara tutalifanyia tathmini ya ile *replacement cost*. Labda niiname sana wapate kusikia.

Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba niliwahi kusema kwenye Baraza hili, kwamba gharama kamili za ku-*replace* mkonga ule ulioharibika kutokana na ujenzi wa barabara ya Mwanakwerekwe - Fuoni, tutafanya tathmini kujua, baada ya pale ujenzi wa barabara ile kukamilika, bila ya kukamilika ile barabara sio rahisi kwenda kufanya tathmini hiyo. Kwa sababu kama ilivyoelezwa kwamba wakati ulipowekwa mkonga ule ulikuwa nje ya barabara. Lakini kama ilivyowahi kuelezwa hapa na Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwamba kutokana na ule utanuzi wa ile barabara, sasa mkonga ule hata kama usingeondolewa ungekuwa ndani ya barabara, ukawa chini ya barabara na hilo isingekuwa jambo sahihi.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Simai Mohamed Said akubali kwamba tutafanya tathmini, ili kujua *replacement cost*, lakini baada ya kumalizika kwa ujenzi wa

barabara, hatuwezi kwenda kuweka sasa hivi wakati shughuli za ujenzi wa barabara zinaendelea.

Mhe. Simai Mohamed Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti. Mhe. Mwenyekiti, naomba nitoe majibu ambayo alijibu Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, wakati tunachangia katika hotuba ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji.

Mhe. Mwenyekiti, namnukuu Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango alisema hivi; Mhe. Mwenyekiti, naomba kwanza Mhe. Simai Mohamed, akubali kwamba huo sio uzembe. Katika ujenzi wowote unapotengeneza unaweza ukatokezea uharibifu, kwa hivyo huo sio uzembe, na tunapotaka kujenga lazima saa nyengine uharibifu ni kitu cha kawaida, lakini fedha hizi nilisema kuna utaratibu wa e*mercency* wa hizi fedha, na zinaweza zikatoka kwenye mfuko mkuu wa Serikali na mfuko mkuu wa Serikali hizo ndio shughuli zake za *emergency*, mbali ya shughuli nyengine lakini mambo ya dharura basi mfuko mkuu ndio unaotufikia hii nimeitoa kwenye *Hansard.*

Lakini pia kuna majibu mengi hapa aliyojibu pia Waziri wa Nchi Afisi ya Rais naomba ninukuu tena Mhe, Simai akazungumza kuhusu barabara. Mhe. Simai barabara husika ilikuwa na upana wa mita sita, maendeleo yanayofanywa sasa hivi ni ya Wizara ni kwenda katika barabara yenye upana wa mita kumi na nne, na takriban miundombinu ambayo anaisema ilikuwa imejengwa mita mbili kutoka mita sita maana yake ilikuwa mita nane ya pale ambapo barabara ilikuwa na mita sita. Unapozichukua mita nane unapoongeza mita sita maana yake bila ya shaka yoyote kipande cha *fiber optic* kitakuwa katika eneo la barabara halipo, sasa ni kweli maendeleo ni kupanga na kupanga ni kuchagua, sisi tuliamua kupanga kwamba tuongeze upana wa barabara kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba haya yote yalipangwa katika mpango mzima wa barabara, lakini katika mzima ulioandikwa *fiber optic* pia palipangwa, lakini wakati barabara inakwenda kutengenezwa, *fiber optic* kutoka Mwanakwerekwe ambayo Mhe. Waziri wa Fedha anategemea hii kuitumia pengine huko mbele kutumia na kupata mtandao kwa ajili ya mambo yake ya kutumia *Electronic Fiscal Devices* katika Mkoa wowote pamoja na Fuoni na Mwanakwerekwe, lakini huu waya sasa hivi umeshaharibika na Mhe. Mwenyekiti, wewe ni shahidi pamoja na wajumbe hapa, kama unakumbuka niliomba sana kwamba waya huu ulioathirika mita zake zinajulikana, kwa sababu huu waya ulivyotandikwa unajulikana wote ni mita ngapi, na waya kutoka Pemba kutoka Kaskazini mpaka Kusini, ni *linear*, unajulikana ni mita ngapi, kwa hivyo mita

ambazo zimeathirika tayari mimi nina uhakika *ZANTEL* wameshawapelekea Wizara ya Fedha, au Wizara husika kuhusiana na matengenezo yake.
Tunataka kujua hizi gharama kama italipa Wizara kwa makusudi ambazo hizi zimeliwa, je, kutokana na makusudi haya Serikali inakubali kutumia hizi fedha, kwa sababu tayari tathmini imeshafanywa Mhe. Mwenyekiti naomba majibu.

Mhe. Waziri wa Fedha na Uchumi: Mhe. Mwenyekiti, naomba Mhe. Simai akubaliane na ukweli kwamba tathmini inahitajika, na pamoja na kwamba anasema unaweza kuujua urefu wa hii *cable* ilivyoharibika, lakini bado ziko gharama nyengine ambazo ni lazima kwa sababu tunahitaji pia pengine mkandarasi, wachimba misingi upya watakuja na bei zao mkandarasi wa kuuweka huo na kuu-*fix* upya watakuja na bei zao hivi sasa hatuzijui, hata kama utajua urefu wa *cable* yenyewe. Tunaomba atuachie baada ya kukamilika kwa barabara hiyo tutakuja na gharama kamili zitakazo *involve* katika ku-*replace cable* hiyo, hilo ndilo tunalolisema kwa sasa hivi ni tabu sana kuweza kujua gharama kamili za kurudisha mkonga huo katika sehemu hiyo iliyopata uharibifu.
Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Simai Mohamed nafikiri umeelewa vizuri, umeshajibiwa sana, Mheshimiwa hili tena hatuwezi kuendelea, Mheshimiwa kasema acha wafanye *research*, wachunguze wapate kujua hizo gharama kwa sasa hivi hawawezi kujua gharama, zaidi ya hilo sidhani kama utapata jibu jengine.

Mhe. Simai Mohamed Said: Mheshimiwa ninayo zaidi.

Mhe. Mwenyekiti: Nakusikiliza Mjumbe.

Mhe. Simai Mohamed Said: Hii ni haki yangu Mhe. Mwenyekiti ya tatu Mhe. Mwenyekiti, kweli ni sahihi majibu ameyatoa Mhe. Waziri, na mimi pia nimekwenda kwenye Hansard nikaangalia majibu yake kuweza kujiridhisha. Lakini suala langu ni kwamba hii *fiber optic* na kama nilivyozungumza hapa nilizungumza lugha hapa nikasema kama sio uzembe ni *negligent* lakini hapa nikavamiwa.

Lakini alichokisema ni kwamba *fiber optic* kutoka Mwanakwerekwe hadi kwenda Fuoni imeharibiwa kwa makusudi ambayo sasa hivi itasababisha hizi hasara, lakini pia sasa tunakwenda katika mpango mkubwa wa barabara kutoka Fuoni kwenda zake mpaka Tunguu. Sasa, je, Mhe. Waziri atwambie kabisa kule tayari ile *fiber optic* inatumika pengine katika Vyuo vikuu vilivyokuweko kule, Je, na ile *fiber optic* itararuliwa pia kwa makusudi.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba tu kiti chako kijielekeze sana katika kanuni, naomba sana Mhe. Mwenyekiti na ukisoma kanuni ya 58 fasili ya 5 sidhani kama jambo hili kuna haja tena ya kundelea kujadili jambo hili, tumeshalijadili katika mkutano huu tukafikia maamuzi na mimi nilikuwa naamini kwamba kiti chako kitaheshimu sana na kuelekeza kwa mujibu wa taratibu husika. Nilikuwa naomba muongozo kwenye hili Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kutoa ufafanuzi kuhusiana na hii hoja yake.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Simai hili tumeshalijadili nafikiri tumemaliza hapa tuendelee.

Mhe. Simai Mohamed Said: Mhe. Mwenyekiti, mimi sina tatizo tunaweza kuendelea naomba urudie Mhe. Mwenyekiti ilikuwa sijakusikia.

Mhe. Mwenyekiti: Nasemaje hili limejadiliwa na kama umepata nafasi ya kuuliza maswali umeshauliza mara tatu na tayari Mheshimiwa ameshakupa majibu, sasa jibu unalolitaka wewe halipo zaidi ya wewe unavyotaka.

Mhe. Simai Mohamed Said: Ni sahihi kweli Mheshimiwa Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Kwa hivyo tunaendelea.

Mhe. Simai Mohamed Said: Mheshimiwa naomba tuendelee lakini sijapata majibu ahsante.

Kifungu kidogo SF 010402

Mhe. Mwenyekiti: Hiki kifungu hatujapitisha ulikuwa hujasimama wala sijakuona hiki kifungu kimeshaulizwa tushamaliza ilikuwa tunaendelea sasa Mheshimiwa umesimama kwa ajili ya kifungu gani?

MUONGOZO

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Unajua anapoanza kifungu tu kinadakwa watu wengine hawapati kukamata, kwa hivyo bora kupitia kiti chako umruhusu mpaka amalize hata kama watapiga mara kumi huku, amalize kifungu tukielewe ndio tuweze kukikamata kwa sababu kama sasa hivi kataja SP tu watu tayari wamedaka, kwa hivyo ndio maana tukawa nyuma ya kukamata kifungu nafikiri nimeeleweka.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa tumekubaliana hapa watu wanakuwa wananyanyuka watu watatu nataja majina ya wale watu sawa, wakimaliza kama hawajajitokeza kwa mara ya kwanza ina maana kuna mtu huyu mmoja ndiye ninayempa nafasi sawa, kwa hivyo Mhe. Nadir alikuwa hajanyanyuka ndio hoja ipo hapo, umenifahamu Mhe. Abdalla, sasa tuache tuendelee.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Bado lakini kifungu ni watu watatu pamoja na hayo.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa tuendelee acheni ubishi uliokuwa hauna tija.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Kwa sababu anapozungumza tu hawahi kumaliza kifungu kinadakwa, kwa hivyo anapoangalia anakuwa mtu amechelewa kwa hivyo kama ni watu watatu…

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Abdalla Diwani Maulid nisikie mimi nikizungumza wewe usizungumze sijui umenifahamu, nimeshamuweka chini Mhe. Nadir tunaendelea.

Kifungu SF 010402 Progaramu ndogo ya kuandaa Mipango,
Sera na kufanya tafiti za sekta ya Fedha 1,161,447,000
Kifungu SF 010403

Mhe. Mwenyekiti: Tunaanza na Mhe. Omar Saif Abeid, halafu Mhe. Abdalla Diwani halafu Mhe. Nadir.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nashukuru kunipa nafasi. Nilipokuwa nikichangia kuhusu habari ya bandari ya Zanzibar kwamba ni moja kati ya kitovu cha uchumi wa nchi yetu, na nikaifananisha na bandari ya Dar es Salaam kama daraja la kwanza bandari ya Tanga daraja la pili, na kwamba bandari yetu tunaitegemea iwe ndio chanzo kikubwa cha kuingiza mapato.

Sasa swali langu lipo hapa, je, Shirika la Bandari kupitia bandari zake zote za Zanzibar ina mpango gani kwa kuichangia bajeti yetu angalau kwa asilimia 25% ifikapo mwaka 2017. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Fedha na Uchumi: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli alivyozungumza Mhe. Omar Seif lakini nimjulishe tu kwamba upo utaratibu wa mashirika haya kutoa *dividend* kwa Serikali, kwa maana ya kuingiza katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Kwa hivyo Shirika la Bandari ni moja katika mashirika hayo ambayo yanalipa *dividend* kwa Serikali kwa maana ya kuingiza

mgao wa *dividend* kwa Hazina kuu na Hazina ya Serikali kila mwaka jambo hilo linafanyika.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa jibu lake kwa hivyo tuendelee.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mwenyekiti, na mimi wakati nilipokuwa nachangia nilizungumza juu ya suala zima la *ZRB* wakati wa ukusanyaji wa kodi yao ya *harassment* kule mahotelini, wanakwenda mahotelini katika suala zima la kutathmini kodi zao wanakwenda na *SMG* na mapolisi wanawagongea watu milango kuwa-*harass*, tayari pale kuna kitengo cha elimu ya walipa kodi, kwa hivyo hawawatendei haki wale. Na nimesema kwa sababu sijasikia jibu lake hili Mhe. Waziri kalichukuliaje kwa sababu tunataka tulipe kodi kwa unyenyekevu, kwa hivyo naomba ufafanuzi katika hili.

Mhe. Waziri wa Fedha na Uchumi: Mhe. Mwenyekiti, maofisa wa *ZRB* kutembelea maeneo ya walipa kodi ni jambo ambalo lipo kwa mujibu wa utaratibu wa kisheria na pamoja na hilo alilolizungumza Mhe. Abdalla Maulid Diwani kwamba wako wafanya biashara lakini niseme wapo na wawekezaji wengine wa mahoteli ambao wakorofi hilo lipo, na wakati mwengine tunapata taarifa kwamba maafisa wetu wanapotembelea maeneo hayo ambao hutekeleza kazi zao kisheria huwa wanapata *harassment* na wakati mwengine huwa wanafukuzishwa mbwa wafanyakazi wetu, makosa hayo yapo na wakati mwengine kwa kukwepa hayo na kwa wale ambao tunajua ni kwamba wakorofi huomba msaada wa askari kwenda nao. Lakini si kwamba wanakwenda pale kivita na *SMG* kwenda kuwalazimisha, wanakuwa wanakwenda wanatumia askari hao kwa ajili ya usalama wao, hasa kwa wale wawekezaji wasiokuwa na nidhamu na wasiotaka kulipa kodi kihalali.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana ni kweli Mhe. Mwenyekiti unajua *This is Island Paradise.* Waziri wa Biashara alivyokuwa anapitisha bajeti yake alizungumza *Island Paradise* naomba kuja kustarehe. Leo hii Mheshimiwa unakiri kwamba kweli wanakwenda na *SMG* nafikiri haiashirii jambo zuri, nafikiri labda angetoa kauli haiwezekani anataka watu wa kodi wanaokwenda kukusanya kodi lakini hawaruhusiki, uthibitisho mimi ninao Mhe. Waziri hata ukitaka kesho nitakuletea. Kwa sababu miongoni mwa maafisa ambao wanafuatana nao na haya mambo yanawakera ndio niliokutana nao wakanipa hizo taarifa, na bado yanafanyika, kwa hivyo lazima twende na *voluntary compliance*, watu walipe kodi vizuri, elimu ya walipa kodi itolewe vizuri, tuondokane na mambo kama hayo. Hayaleti sifa nzuri mtu katoka

Marekani, Uingereza na Ujerumani anakuja pale mkusanyaji kodi anakwenda na *SMG*, nafikiri hatufanyi jambo zuri, baada ya kukusanya kodi tunafukuza watoaji wa hiyo kodi, tuendelee Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Kwanza namshukuru Mheshimiwa kwa kusema tuendelee lakini Mhe. Mwenyekiti naomba niweke ufafanuzi sikutumia neno kwamba askari wetu wanakwenda na *SMG*, nilisema kwamba Maafisa wetu kwa wale wakorofi ambao wanawajua wao wenyewe huwa wanaomba msaada wa ulinzi wa Polisi, na nilitumia neno la kwamba hawaendi pale kivita isipokuwa wanakwenda kwa ajili ya kuweka usalama wa hao maafisa wetu lakini pia na usalama wa hao wawekezaji. Kwa hivyo si suala la vita wala sijataja *SMG*, hiyo nafikiri aliitaja mwenyewe Mhe. Abdalla Maulid Diwani. Sisi hatujataja hivyo kwa hivyo *hansard* iweke rekodi hivi.

Mhe. Nadir Abdullatif Yussuf: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, mimi kwanza nampongeza sana Mhe. Waziri Dkt. Khalid kwa majibu yake mazuri aliyonipa ya *ATM* lakini nitaomba tu nichangie kidogo halafu nina swali langu moja kidogo tu la kawaida aje anijibu.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa hapa hatutaki maelezo umenifahamu lete hoja ama kama kuna swali uliza swali.

Mhe. Nadir Abdullatif Yussuf: Haya naleta kwa kuwa mchango wangu nilitoa kwamba wananchi wengi hasa wa mashamba wanapotaka kwenda ku-*withdraw* hata elfu tano au elfu kumi wanabidi wapande daladala kwenda zao mjini, nilimuomba kwamba zile *ATM* zifunguliwe Kaskazini na mashamba mengine ili wananchi wasipate tabu na alinijibu vizuri kwamba watafungua ndio maana nikampongeza.

Lakini swali langu jengine hoja yangu ipo hapa, zile *ATM* mtu hata aki-*withdraw* elfu mbili anachajiwa mia nane au elfu moja, aki-*withdraw* laki nne anachajiwa mia nane elfu moja, ni sababu zipi zinazofanya chaji hizi kuwa kubwa hata kwa *amount* ndogo, sijui ameshanifahamu Mhe. Waziri.

Mhe. Mwenyekiti: Amekufahamu.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, kwanza benki yetu hii ya *PBZ* ni benki ya kibiashara, kwa hivyo wanafanya kazi kibiashara, lakini vile vile kuna *percent* fulani ambayo inakatwa kutokana na *transaction* hiyo anayoitaja, kwa hivyo *percentage* ile inakwenda kama umetoa elfu moja kama umetoa elfu tano ni *percentage* ile ile tu. Kwa hivyo sioni hoja ya kusema

kwamba anayetoa kidogo anakatwa nyingi au sawa sawa na anayetoa nyingi kwa sababu inaendana na *percentage* kile kima ambacho kimewekwa.

Mhe. Nadir Abdullatif Yussuf: Mhe. Mwenyekiti, mimi sitaki kubishana na mzee wangu na bosi wetu lakini unapo- *withdraw* kwenye *ATM any amount* inatoka *same charges* ikiwa mia nane mia nane, hata ikiwa laki nne ikiwa elfu kumi, sasa wananchi wale wenye mshahara mdogo wanaumia. Mimi si-*force* lakini ningeomba sana angekaa na watu wa benki akaangalia zile *charges* aidha ziwe *free* aidha ziwe ndogo zaidi, kwa sababu mtu aki-*withdraw* mara kumi tu basi kashachajiwa zaidi ya elfu kumi, na *ATM* zetu hakuna unazoweza ku-*withdraw* moja kwa moja milioni moja, mwisho laki nne na laki tatu, na kwenda chini.

Mhe. Mwenyekiti: Hilo sasa jengine hilo ulilolisema sahihi la mwanzo Mheshimiwa ameshakujibu, hizo ni shughuli za kibenki kwa hivyo naomba uturuhusu tuendelee.

Mhe. Nadir Abdulatif Yussuf: Mimi ilikuwa maelezo yangu ni hayo kama ni ombi upande fulani naomba tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Ameshalichukua Mheshimiwa tunaendelea.

Kifungu SF 01010403	Programu ndogo ya kusimamia sekta ya fedha na mapato yatokanayo na kodi	124,494,000

Kifungu SF 010404

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa Suleiman Sarhan na Mhe. Hassan Khamis

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi kwanza nimshukuru sana Waziri wa Fedha kwa jitihada zake za kunijibu na kujibu wajumbe wengi vizuri sana, ingawa mimi nilimuandikia majibu mengine ya kuandika lakini mengine sikupata majibu, lakini niendelee na hii hoja moja.

Mheshimiwa mimi natoka jimbo la Chake Chake pale Pemba na kwa kweli kuna suala liliongelewa hapa la kuhusu lile jengo la Wizara ya Fedha liliopo pale Tibirinzi. Mhe. Waziri wa Fedha alipoongea hapa alizungumza kuhusu habari ya jengo lile ambalo liko pale Darajani kuhusu ubovu na hatari ya maisha ya watu, na lile jengo ambalo lipo pale Tibirinzi kwanza lina aibu kila mtu anayepita hata wakipita viongozi kwenda Ikulu wanalitizama wanauliza

nini lile, anaambiwa ilikuwa Wizara ya Fedha limemeguka pana hoteli inalala watu ni hatari.

Nilimsikia Mhe. Waziri na Majibu yake alipokuwa anaongelea kwamba lile suala kama mkandarasi sijui kama tumemshinda halafu ameambiwa alivunje, sijui afanye kitu gani lakini mimi nataka kumuuliza tu kwamba kuna misemo miwili inasema *bora lawama kuliko fedheha* na *lililopita si ndwele tugange yajayo*. Sasa tusitafute ushahidi wa nanihii, mimi Mheshimiwa ningekushauri kama inawezekana kama yule bwana kaambiwa jengo lile alivunje yeye mwenyewe na kakimbia na hakuna utaratibu wa kumpata au inachukua muda mrefu. Je, nikikuletea mtu akalivunja kwa gharama zake halafu yale malighafi zote akachukua yeye akakuwekea kiwanja safi vipi suala hili Mheshimiwa.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Mhe. Suleiman Sarahan alinileta *note* hiyo lakini nimjulishe tu kwamba suala hili bado liko kwenye taratibu za kimahakama na Mahakama tayari imeshatoa kauli kwamba jengo hilo libomolewe kwa gharama kwa huyo mkandarasi aliyejenga jengo lile na sisi tumesema bado tunaendelea na hatua za kukaza hukumu na kumfuatilia huko aliko.

Kwa hivyo, kwanza kwa sababu suala hili liko kwenye taratibu hizo, ningemuomba Mheshimiwa atuachie na tusianze kuanzisha utaratibu mwengine wa ubomoaji wa jengo hilo, na haturuhusiwi kulivunja kwa sababu liko kwenye taratibu za kimahkama.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mimi Mhe. nilimuomba tu kama mwenyewe anaona halina dhara na halina matatizo sawa, lakini mimi nimeliona kwa sababu napita, nikiliangalia nalihisi limeshakuwa na matatizo, sasa inakuwa yule bwana amesafiri mimi nimemwambia tu Mhe. Waziri gharama atatoa mwenyewe huyo mtu atalivunja atasafisha, baada ya kumtafuta yeye huyo mtu atakuja kukuwekea, hataki pesa yako. Lakini kama unaona bado taratibu zinachukulika sawa, lakini mimi nilikuwa ninamshauri kama kutakuwa na mtu ambaye ataliondoa jengo lile na uchafu ulioko pale amuachie kiwanja chake basi yupo. Sasa sijui kama mwenyewe kama keshajibu sawa, kama ataongeza sawa.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nilikuwa na hoja hii hii lakini nitaongezea tu hapo hapo. Hapa Mhe. Gavu amesema tusitumie neno uzembe, siutumii, lakini nitatumia neno ...

Mhe. Mwenyekiti: Twende hoja Mheshimiwa kama una swali uliza tusirudie, Mheshimiwa kaa hebu nikwambieni. Mnajua mnakuwa mna hadithi nyingi tunapoteza muda, hatuna muda wa kusema hadithi na kurudia mambo hayo kwa hayo, hebu twende kwenye *specific point,* twende kwenye mstari.

Sasa nyinyi kila saa mnarudia hayo hayo ili tuanze kulumbana hapa, Mheshimiwa nenda kwenye *point* moja kwa moja, hoja uliyonayo izungumze, hayo ya uzembe yamekwisha sasa.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, ahsante lakini muda hatupotezi ndicho tunacholipiwa Mheshimiwa kuja kuwatetea wananchi.

Mhe. Mwenyekiti: Lakini Mheshimiwa Kanuni inakataza, ni Kanuni sio tu kwamba mimi ninazungumza, lakini Kanuni zetu ndizo zinazotukataza Mheshimiwa, kwa hivyo tufuate Kanuni basi, haya endelea.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mheshimiwa mimi naomba kusema kwamba hizi ni pesa za walipa kodi, mkandarasi huyu kama hayupo kama yupo, lakini je, serikali inafanya utaratibu gani wa kuzipata pesa zetu au ndio zimeshapotea katika angute.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, suala hili tumesema bado liko Mahkamani uamuzi umeshatoka wa kwamba mkandarasi huyu arudishe fedha zilizotumika zilizotolewa na serikali, lakini vile vile alibomoe kwa gharama yake, hiyo tayari, sasa kinachofanyika sasa hivi ni kukaza hukumu, na sisi tumeshasema kwamba tunafuatilia huko huko aliko kupitia Ofisi yetu ya Kibalozi, lakini pia kupitia Mahkama Kuu. Upo utaratibu wa mahkama kwa mahkama kuwasiliana kumpata mtu huyu, hilo ndio tunalolifanya ili kuziokoa fedha za umma.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Hassan hili hatuwezi kulijadili baada ya hapa, nimeambiwa kwamba hili suala liko mahkamani. Tuiachie mahkama ifanye kazi, majibu yatakayokuja kutoka mahkamani ndio tunaweza kuyajadili, sasa hivi hatuwezi kulijadili, naomba tuendelee.

Kifungu SS010404	Programu Kuu ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Wizara Pemba	1,075,573,000
	Jumla ya Fungu	68,249,529,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Kifungu 02 Mfuko Mkuu wa Serikali

Kifungu PF 0201 Programu Kuu ya Usimamizi ya Mfuko Mkuu wa Serikali

Kifungu kidogo SF 02

Mhe. Simai Mohamed Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, mimi nitachukua muda mdogo tu, wakati anatoa majibu Mhe. Waziri alizungumzia suala la deni la taifa, na nafikiri hapa ni eneo lake. Lakini katika hotuba ya Waziri wa Fedha na Mipango alipoisoma kuhusu mapendekezo ya bajeti ya Serikali kuhusu Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa Fedha 2016/2017 ukienda katika ukurasa wa 37 alizungumzia maeneo 3.

Sura ya bajeti ya mwaka 2016/2017 inahusisha mapato ya jumla ya shilingi bilioni 841.5 yakiwemo mapato ya ndani na shilingi bilioni 482.4 mapato kutoka nje na shilingi bilioni 324.8 fedha kutokana na misamaha ya madeni na shilingi bilioni 1.3 na mikopo ya ndani shilingi bilioni 33.

Kwa upande wa matumizi kiasi hicho ni shilingi bilioni 841.5 kinatarajiwa kugawanywa kwa shilingi bilioni 400.45 kuelekezwa katika matumizi ya kazi za kawaida na shilingi...

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa toa hoja unasoma hotuba ambayo tayari Waziri ameshaisoma.

Mhe. Simai Mohamed Said: Sawa Mwenyekiti, hoja yangu mimi kuhusiana na deni la taifa, alizungumza kwamba deni la taifa linaongezeka kutokana na kuanguka kwa shilingi yetu. Swali hapa nilitaka kujua kama alivyozungumza mfuko kwenye deni la taifa alisema kwamba hili halina *account* maalum ambazo kuna madeni ambayo kama alivyozungumza kuhusu suala la *airport* hizi fedha ambazo zina mikopo zinalipwa huko kwa huko hapa wanakuja pengine hao watu wanaohusika kuja kufanya hiyo kazi.

Sasa hapa ukiangalia katika mikopo ya ndani ni bilioni 33, sasa ukiangalia katika deni la taifa lililotoka mwaka jana nafikiri lilitoka kutoka milioni 316 mpaka kukaribia bilioni 390 na kitu nafikiria kama bilioni 50 au 60 hizi ziliongezeka kutokana kwamba kuanguka *almost* kama *more than* 50 *billions.* Sasa nilikuwa nataka kujua hizi fedha za bilioni 33 hizi zinakuwa zinalipwaje na zinakaa katika mfuko gani.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Sina hakika kama nimemfahamu vizuri maana swali lake limechanganyika sana na maelezo, lakini tulivyokuwa tukizungumza suala la kwamba hatuna *account* ya madeni na bado narudia kwamba hatuna *account* maalum ya madeni, lakini tuna *account* ya Mfuko Mkuu wa Serikali ambayo ndio hii hapa.

Masuala ya Mikopo ya Nje ni mikopo ambayo sisi tunakopa na tunairipoti hapa, lakini mikopo hiyo sio kwamba zile fedha zinakuja moja kwa moja na kuingizwa kwenye *account*. Lakini fedha hizo hutumika na matumizi yake ni kwamba yanatumika moja kwa moja kutoka kwa yule anayetupatia fedha kwenda kwa *contractor* au *supplier* anayetoa huduma. Lakini kwenye ripoti tunaripoti kwamba ni madeni ambayo yamepokelewa na serikali, kwa maana ya kwamba ni deni la taifa lakini si kwamba zinaingizwa katika *account*, huo ndio utaratibu ambao niliuzungumza, lakini kuna fedha ambazo zinapatikana katika mikopo ya ndani nazo fedha hizo zinakaa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mhe. Simai Mohamed Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, mimi nimemfahamu kwa kiasi fulani, lakini sasa kuna mikopo wanachukua ambayo pia inakuwa katika *foreign currency* ambayo wanatumia serikali katika huduma zao tofauti, barabara pia wanachukua mikopo katika kuagizia vitu. Sasa katika hizi fedha ambazo zinatakiwa ilipe mikopo ya nje hizi fedha ambazo kwa mfano tumechukulia katika huduma ambazo serikali imezungumza mikataba inayofungwa na *airport*, lakini pia wanachukua mikopo ya fedha kutoka nje. Sasa fedha hizi wanapotaka kuzilipa wanaziweka katika mfuko gani, kuna *treasury bonds* wanazochukua, kuna mikopo wanachukua hata benki za ndani tumeona hapa wamezitaja katika bajeti bilioni 33, hizo fedha za nje ambazo wanachukua mikopo ambazo ndio deni la taifa, kwa mfano katika hili deni la taifa...

Mhe. Mwenyekiti: Umeshauliza swali lako, Mhe.Waziri anataka kukujibu.

Mhe. Simai Mohamed Said: Mhe. Mwenyekiti waziri anakuwa mnyonge na mimi pia mnyonge.

Mhe. Mwenyekiti: Amekuelewa, atakujibu.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, kwanza madeni ya nje ni dhima ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa hivyo Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndio inayokopa. Lakini kuna utaratibu wa ndani wa *all lending arrangement* ambao tuna-*sign* baina ya

Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Zanzibar kwa maana sisi tunalipana wenyewe. Lakini deni lile linakuwa *serviced* na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa sababu wao ndio *borrower* wa fedha hizi.

Mhe. Simai Mohamed Said: Mhe. Mwenyekiti, naomba tuendelee.

Kifungu kidogo SF 020101	Programu ndogo ya Usimamizi wa Mfuko Mkuu wa Serikali	83,529,900,000
	Jumla	83,529,900,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Fungu F03 Tume ya Mipango

Kifungu PF0301 Programu Kuu ya Kuratibu Mipango ya Kitaifa na Maendeleo ya Watenda kazi

Kifungu kidogo SF03

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. Kwanza nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa umakini wake na huku tunaulizana huko mbele kama ataendelea kama hivi huenda baadhi ya wajumbe tukamchagua kuwa atakuwa ndio Mwenyekiti wa Mawaziri wa Dkt. Ali Mohamed Shein kwa umakini wake.

Mhe. Mwenyekiti kama kuna kitu kilichonivutia leo kuona mawaziri wote leo wako *full* kufanya kazi hii kusimamia bajeti hii, haijawahi kutokea mawaziri kama hivi leo.

Hoja yangu uratibu wa mpango wa kitaifa kupunguza umaskini, hapa kifungu hiki cha kupunguza umaskini ni kilio cha muda mrefu ambacho kinanikosesha usingizi mimi, kuhusu wale ng'ombe wamefikia hatua gani na hiyo *fine* ni shilingi ngapi, huu ni kupunguza umaskini kifungu hiki. Ng'ombe wale ni shilingi ngapi *fine* yake, na niiombe serikali ipunguze, hivi sasa kuna sikukuu keshokutwa watu wanapata shida kujua utaratibu wao. Nataka kauli ya serikali, kote nimekaa kimya nimetulia hapa tu.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku swali hilo halihusiani na bajeti hii.

Utaratibu

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, kuhusu utaratibu kiangalie kifungu kinasemaje mimi nimezaliwa shamba, nimesoma shamba, nimekulia shamba lakini kwa muda huu ninaishi mjini, kiangalie hiki kifungu ukisha unipe elimu pamoja na makatibu wakusaidie, mimi ni mshamba Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Mawaziri mna maelezo ya hili.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, kwanza katika siku ambayo nitakuwa mpole sana, ili nimjibu Mhe. Jaku aelewe, kwamba pamoja na maelezo yake aliyoyatoa kifungu hiki hakina uhusiano wowote ule na suala alililiuliza, la kwanza. Na ni vizuri tunaposisitiza kwamba tufuate utaratibu na kanuni lazima wajumbe wako wa Baraza la Wawakilishi tuheshimu hilo.

Sasa kuhusu suala hili la ng'ombe, yeye kama Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi, anayo haki ya kuuliza swali la msingi kwa Waziri anayehusika naye ni mimi. Kwa hivyo afuate utaratibu, aulize swali atajibiwa na atapata maelezo ya kutosha. Sasa kumjibu katika kifungu hiki sioni kama kuna mantiki.

Mhe. Mwenyekiti, nasisitiza tufuate utaratibu. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku kaa kwanza, Mhe. Waziri mimi ninafikiri nimemfahamu sana Mhe. Jaku.

Hoja yake anayojenga hapa kwa sababu kifungu hiki kinahusiana na masuala ya kuondoa umaskini Zanzibar. Hoja yake kubwa ndio iko hapo, na kwa sababu hiyo Mhe. Jaku anafahamu vizuri sana kuhusiana na MKUZA ambao kwa kuondoa umaskini Zanzibar ndio maana anauliza swali hili wafugaji wetu ni maskini, na ndio suala hilo ambalo linazungumzwa. Sasa Mheshimiwa naomba utujibu katika msingi huo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mheshimiwa mimi ninakiheshimu sana kiti chako, na ukisoma kanuni ya 59 (1) inaelezea jambo ambalo nimelisema.

Sasa kama kila mtu anaweza akaamua tu kusimama na kusema lolote, mimi nadhani Mwenyekiti tufuate utaratibu Kanuni ya (59). Kwa hivyo mimi ni

vizuri kama unaniomba, nyote mnazo kanuni Waheshimiwa Wajumbe, Mheshimiwa kama unaniomba nitoe maelezo, kwanza jambo hili Mhe. Jaku amekuwa akilizungumza sana hapa, na kiti chako kinatoa muongozo wa namna gani jambo hili litafika.

Mhe. Jaku siku ya mwanzo alizungumzia suala la serikali kutoa kauli, utaratibu wa serikali kutoa kauli umeelezwa vizuri sana, kauli za serikali na taarifa za serikali zitatolewaje.

Mhe. Spika, bado hajatwambia sisi kama serikali kwamba leteni kauli hiyo kwa utaratibu ambao upo kwa mujibu wa kifungu cha 43(1) na taarifa ya serikali kwa mujibu wa kifungu cha 44(1).

Sasa mimi nadhani Mheshimiwa kama Mhe. Mwenyekiti, unaruhusu hilo kwamba hata yale maamuzi na muongozo wa Spika, tuuweke kando na tuweze kutoa maelezo kabla ya amri ya Mhe. Spika, basi mimi niko tayari kutoa maelezo ya serikali, lakini lazima tufuate hizi kanuni zetu.

Na mimi hofu yangu ni kwamba tukianza kufanya vyenginevyo maana yake hii *precedent* itakuwepo, kwa maana hiyo hatutafuata utaratibu. Ninavyojua mimi Mhe. Spika, juu ya jambo hili ametoa muongozo, sasa tuliache jambo hili Mhe. Spika, muongozo alioutoa baada ya Mhe. Jaku kuleta hoja serikali ipate muda wa kutayarisha majibu na maelezo au kauli au taarifa tuilete ndani ya Baraza hili la Wawakilishi, tusiende kwenye mambo mengineyo.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri hili tulilizungumza kweli kama ulivyosema, na mimi ndio hoja imekuja wakati mimi niko kwenye kiti, na baada ya hapo Mhe. Spika, tulikubaliana kwamba serikali ilete hoja Barazani, hoja hiyo haijafika. Kwa sababu hoja hiyo haijafika ndio masuala kama haya yanakuja. Ningeomba Mheshimiwa hapa tusifanye hayo majadiliano.

Namuomba Mhe. Jaku atuachie tuendelee, tumalize hili Mhe. Spika anayo mamlaka ya kukubali hoja hiyo ije na tutakaa tutalizungumza ndani ya Kamati zetu za Uongozi, tutalizungumza hili nafikiria Waheshimiwa Wajumbe hata nafikiri wote wanaona iko haja ya taarifa ya serikali kuhusiana na ng'ombe iletwe Barazani. Kwa hiyo, naomba sana, sana Waheshimiwa Wajumbe.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mwenyekiti..

Mhe. Mwenyekiti: Nimekuomba Mheshimiwa ukae tuendelee tumalize wizara hii. Naomba muheshimu kiti changu sasa hivi, nakuombeni sana, niko *serious*

kabisa, sitaki miongozo mengine hapa. Ninachokisema ni hiki tuachie wizara hii ipite, kifungu hiki isiwe ndio sababu ya kuzuia wizara hii isipite, hili jambo uwezekano wa kulizungumza na taarifa tukaipata haraka iwezekanavyo ndani ya Baraza hili.

UTARATIBU

Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata): Mhe. Mwenyekiti, mimi naungana na kauli ya Mhe. Jaku lakini pamoja na busara zako sina tatizo, isipokuwa kuna kauli iliyotoka kwa Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ kidogo sikuridhika nayo, hasa aliposema kwamba kiti hicho Mhe. Spika mumekubaliana kwamba kanuni itengwe au utafutwe utaratibu. Kiti hicho kuanzia Spika, Naibu Spika na Mwenyekiti ana haki ya kubadilisha kanuni au kutengua kwa ajili ya kusuluhisha jambo fulani, kwa nini aitengue yeye Mheshimiwa kasema haiwezekani.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, bado Kanuni ya 43 (2) pia tunaweza tukaendelea kuitumia. Lakini Mhe. Mwenyekiti, hapa ukiacha kauli ya serikali Mhe. Jaku aliwahi kuja na hoja na tena hoja ya dharura, na kawaida ya hoja ya dharura Mhe. Mwenyekiti ina maana kunakuwa kuna jambo la dharura linaweza likaleta athari kwa jamii.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, kama kauli ya serikali mpaka tunamaliza bajeti hii haijatoka, basi naomba hoja ya Mhe. Jaku ije ijadiliwe ili tuweze kutoa ushauri, kwa sababu Mhe. Mwenyekiti sasa hivi huko mitaani hali ishakuwa mbaya, mbaya, mbaya sana, tukisubiri kauli ya serikali waende wakakae, wakaandae huku maafa mengi yatakuwa yameshatokea. Kuna malalamiko mengi ya wananchi, kuna manung'uniko mengi sasa hivi mpaka mali za serikali zinaanza kuvurugwa, mali za wananchi zinaanza kuvurugwa, hali za wananchi ziko mashakani.

Mhe. Mwenyekiti, mimi bado naomba kama serikali hawajatayarisha hiyo kauli basi kesho ije ile hoja ya Mhe. Jaku ili tuijadili tupate kuishauri vizuri serikali katika utekelezaji wa jambo hili.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, kiti unachoongoza ni hiki hapa Katiba ya Zanzibar, Ibara ya 88 Baraza la Wawakilishi pamoja na kuongoza shughuli zake zote kutokana na vifungu vya Katiba moja ya jukumu hapa waziri asifikirie kuwa tutamfunga sisi au tutampiga faini, mimi sina uwezo wa kumfunga waziri wala kumpiga faini. Ajibu wananchi wajue tatizo ni hilo tu, Katiba inatuongoza moja ya majukumu yetu ni kuhoji mawaziri.

Mhe. Mwenyekiti: Sawa Mhe. Jaku tumekuelewa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi na pia nimshukuru sana Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ na wajumbe wote ambao wanazungumzia suala hili.

Mhe. Waziri amesema kwamba serikali haina tatizo na kuleta kauli ya serikali katika muda huu wa kipindi hiki kabla ya kuahirisha Baraza letu. Kwa hiyo, nataka niwahakikishie wajumbe na wewe Mhe. Mwenyekiti kwamba serikali itafanya hivyo, kauli ya serikali itakuja na kwa njia moja au nyengine sisi tuliomo humu ndani tumeshaisikia *concern* ya wajumbe na tumeisikia *concern* ya wananchi.

Kwa hivyo, serikali italitafakari jambo hili na kauli yake itakuja na nina hakika tutafikia muafaka mzuri kwa maelekezo ya Mhe. Waziri hapa ameeleza vizuri mwanzo na tutamalizia vizuri. Kwa hiyo, nawaomba isiwe kutafautiana katika dakika ya mwisho, tumeanza vizuri bajeti yetu, tumeanza vizuri kipindi kizima hiki cha bajeti na nina hakika tutamaliza vizuri, na siku zote serikali yetu ina usikivu mkubwa kwa Waheshimiwa Wajumbe, ina usikivu mkubwa kwa wananchi, tutafikia muafaka hili jambo. Mheshimiwa naomba wajumbe watupe nafasi jambo hili likatafakariwe vizuri tuje na majibu sahihi. Ahsante sana.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, mimi nimshukuru sana Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais naweza kusema mtaalamu makini, lakini kuja itakuja kesho au kesho kutwa lakini mimi namuomba tu atwambie kati ya kesho au kesho kutwa huo ni muda mrefu, wiki ya pili nahangaika na usingizi, mimi nakula dawa ya usingizi kwa suala hili, halinipi raha.

Mheshimiwa nakuheshimu sana tena sana, ni mtaalamu katika mawaziri, nambie ni lini nipate kujua na wananchi wapate kujua, ni hapo tu Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, nataka nimuhakikishie Mhe. Jaku kabla ya kufunga Baraza hili tutaleta taarifa, siku zilizobaki kidogo, karibu tutamaliza nina hakika tulete kitu chenye msingi, kitu kizima, kitu kilichokuwa kina uhakika, kitawafurahisha wajumbe wetu na wananchi wetu kwa jumla.

Hatuna nia wala dhamira mbaya ya kugombana na wajumbe au kugombana na wananchi. Dhamira ni kutatua tatizo linalojitokeza kwa misingi mizuri, na mambo ambayo tunayazungumza hapa Mheshimiwa sote ni kwa ajili ya kuwahudumia wananchi wetu, serikali ipo kwa wananchi, Waheshimiwa Wawakilishi wapo kwa wananchi, nia yetu ni kuondoa kila tatizo ambalo wananchi wanalikabili. Kwa hiyo, tunaomba Waheshimiwa Wajumbe watuelewe kwamba jambo hili litamalizika tutaleta kauli yetu hapa kabla ya kuahirisha kikao hiki cha Baraza. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, kwa kauli ya serikali aliyotoa Mhe. Waziri ambaye ninamuamini naomba tuendelee.

Kifungu SF 030101	Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango ya Kitaifa na Kupunguza Umasikini	1,421,046,000
Kifungu SF 030102	Programu Ndogo ya Maendeleo ya Watenda Kazi na Masuala ya Idadi ya Watu	467,305,000
Kifungu SF 030103	Programu Ndogo ya Ufuatiliaji na Tathmini ya Mpango wa Maendeleo	871,502,000
Kifungu PF 0302	Programu Kuu ya Usimamizi wa Uchumi Mkuu	
Kifungu SF 030201	Programu Ndogo ya Ukuzaji wa Uchumi	2,274,300,000
Kifungu SF 030202	Programu Ndogo ya Mashirikiano Baina ya Sekta za Umma na Sekta Binafsi	100,000,000
Kifungu PF 0303	Programu Kuu ya Utawala na Uendeshaji wa Tume ya Mipango	
Kifungu SF 030301	Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji wa Tume ya Mipango	777,825,000
	Jumla	**777,825,000**
	Jumla Kuu	**5,911,978,000**

(*Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Naibu Spika, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha Makadirio ya Fedha ya wizara yangu bila ya mabadiliko, sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza liyakubali makadirio hayo. Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, Mhe. Waziri ameshatoa hoja sasa niwaulize wanaokubaliana na hoja hiyo wanyooshe mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kwanza nichukue fursa hii adhimu kumpongeza Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kwa kupitisha bajeti yake, lakini nimpongeze sana kwa kuweza kujibu masuala mengi ambayo natarajia kwamba Waheshimiwa Wajumbe mengi wameridhika nayo kutokana na kauli zao. Kwa hiyo, nimtakie kheri yeye na watendaji wake katika utendaji wa shughuli zao za kikazi, lakini niwashukuru na mawaziri wale waliochangia kumsaidia Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango.

Waheshimiwa Wajumbe, bado tuna mswada ambao tunatakiwa tuupitishe hii leo, kwa hiyo ningemuomba Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kutengua Kanuni ya Muda ili tuweze kuendelea na mswada wa Mhe. Waziri wa Fedha kumpa uwezo wa kuweza kutumia fedha hizi ambazo tumemkubalia hii leo na baada ya hapo Mhe. Waziri wa Fedha atakuja kuwasilisha. Baadaye tutachangia wajumbe wachache watapata fursa ya kuchangia, na hivyo hii leo tutamaliza na mswada huo.

Kesho tukijaaliwa tutaanza na mswada wa Wizara ya Afya. Ingawa hiyo kesho mimi ningeshauri na ushauri umetoka kwa watu wengi Waheshimiwa Wajumbe kwa sababu ilikuja hoja hapa na nafikiri namjibu Mhe. Jaku v ile vile na hoja ambayo ameleta Mhe. Hamza, kwamba waache Mhe. Waziri asome mswada wake pamoja na Mwenyekiti halafu watapewa siku moja ili kwamba angalau wajumbe muuelewe, kwa sababu ataposoma Mhe. Waziri mtakuwa na uelewa mzuri zaidi wa kuufahamu huo mswada, ili kupata fursa, hautochangiwa pale pale, tutakwenda zetu kwenye semina siku ya pili yake, kesho yake Waheshimiwa Wajumbe ndio mtapata fursa ya kuanza kuuchangia huo mswada. Kwa hiyo, itakuwa ni muda wa kutosha kwanza nafasi ya kuweza

kuuelewa vizuri mswada utakuwepo kwa sababu utaelezwa pamoja na kamati vile vile itatoa taarifa yake.

La pili, tutapata muda sasa wa kwenda na kuweza kuona kupitia siku ya pili ndio tutaanza kuuchangia. Nafikiri mtakubaliana na mimi kwa hilo waheshimiwa kwa sababu huu mswada ni mswada wa dharura.

Baada ya kusema hayo waheshimiwa sasa namuomba Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili atengue Kanuni ya Muda ili tuweze kuendelea na shughuli zetu.

KUONGEZA MUDA WA BARAZA

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa kwa mujibu wa orodha ya shughuli za leo bado kumalizika, na kwa kuwa tunayo shughuli muhimu ya Waziri wa Fedha ya kuwasilisha sheria ya kuidhinisha makisio na matumizi ya fedha, na kwa kuwa muda uliobaki haututoshi kufanya shughuli hiyo, kwa hiyo Mhe. Naibu Spika na Waheshimiwa Wajumbe naliomba Baraza lako tukufu tuweke kando Kanuni ya Muda ili tuweze kumaliza shughuli zilizo mbele yetu.

Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ametoa hoja, sasa niwaulize wanaokubaliana na hoja hiyo wanyooshe mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mswada wa Sheria ya Makisio na Matumizi ya Mwaka 2016

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Naibu Spika, naanza kwa kumshukuru tena Mwenyezi Mungu muumba kwa kutuwezesha kukutana tena kwa shughuli hii muhimu itakayopelekea nitimize wajibu wangu wa kikatiba, kwa maana kifungu cha 106 cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 kama ilivyorekebishwa kinachomtaka waziri mwenye dhamana ya fedha kuwasilisha katika Baraza la Wawakilishi mswada kwa ajili ya kuidhinisha matumizi ya serikali kila mwaka unapoanza.

Mhe. Naibu Spika, kwa heshima kubwa naomba sasa niwasilishe mapendekezo ya Mswada wa Sheria ya Kuidhinisha Makisio na Matumizi ya Shilingi Bilioni Mia Nane na Arobaini na Moja, Mia Nne Sabini na Saba Milioni na Laki Tano kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mwaka wa Fedha Unaoishia Siku ya Tarehe 30 Juni, 2017 na Kuruhusu Utoaji na Uhaulishaji wa Fedha hizo Pamoja na Mambo Yanayohusiana na Hayo.

Mhe. Naibu Spika, uwasilishaji huo wa Mswada wa Sheria ya Matumizi unaashiria kukamilika kwa kazi ya kupitisha Bajeti ya Serikali iliyofuatiwa na uwasilishaji, mijadala na hatimaye kuidhinishwa kwa bajeti ya kila wizara kama ilivyoelekezwa na Katiba ya Zanzibar.

Lazima nikiri kuwa katika mijadala yote hiyo Waheshimiwa Wajumbe kwa upande wao wamedhihirisha uwezo wao mkubwa wa kuisimamia serikali, kuwawakilisha wananchi wote wa Zanzibar katika chombo hiki muhimu na kusimamia maendeleo ya Zanzibar na watu wake. Wakati mwengine mumetuchangamsha sana mawaziri, na wakati mwengine mumetubana sana lakini tunaelewa hii yote ni katika kuwatumikia vyema wananchi. Nawapongeza sana Waheshimiwa Mawaziri na Waheshimiwa Manaibu Mawaziri kwa umahiri wao wa kujibu hoja za wananchi kupitia kwenu Waheshimiwa Wawakilishi…

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri kidogo naomba usite, nampisha Mhe. Mwenyekiti aje kuendelea na shughuli hii iliyobakia.

Hapa Mhe. Mwenyekiti (Mwanaasha Khamis Juma) alikalia kiti

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe.Mwenyekiti, mijadala yote hiyo imeongozwa na kusimamiwa na ama wewe binafsi ama mwenyewe Spika ama Mhe. Naibu Spika, au Waheshimiwa Wenyeviti wa Baraza hili.

Naomba upokee pongezi zangu za dhati kwako wewe na Mhe. Spika na Mhe. Naibu kwa uweledi mkubwa mliouonesha katika kuliongoza Baraza hili katika kipindi kifupi cha kupokea dhamana hizo. Kwa mchanganyiko tulionao wa wajumbe na uongozi wa Baraza sina shaka yoyote kuwa uwajibikaji na utendaji serikalini utaimarika zaidi na hivyo kutoa huduma bora zaidi kwa wananchi wote wa visiwa vyetu vya Unguja na Pemba. Tumalizie ngwe iliyobaki ikiwemo kupitisha mswada wa sheria ya matumizi ya mwaka 2016.

Mhe. Mwenyekiti, kupitishwa kwa mswada huu kutaiwezesha serikali kutekeleza mipango mliyoidhinisha kwa kazi za kawaida na kazi za maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti mswada huu una vifungu tisa. Kifungu cha kwanza kinazungumzia jina fupi la mswada. Kifungu cha pili kinatoa tafsiri ya maneno yaliyotumika katika mswada huo yakiendana pia na sheria ya fedha za umma nambari 12 ya mwaka 2005.

Kifungu cha tatu kinazungumzia utoaji wa shilingi bilioni mia nane na arubaini na moja mia nne sabiini na saba milioni na laki tano kutoka mfuko mkuu wa Hazina ya Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha nne kinazungumzia makisio ya fedha zilizokubalika, kifungu cha tano chenye vifungu vidogo vinne kinazungumzia uwezo wa kukopa kwa waziri mwenye dhamana ya fedha na kifungu cha sita chenye vifungu vidogo vitatu kinazungumzia uwezo wa waziri katika maombi ya ziada kwa lengo la kukubali matumizi mengine ya dharura pale haja itakapotokezea.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha saba kinazungumzia marejesho ya mkopo na riba. Kifungu cha nane kinazungumzia kukubaliwa kwa mipango ya maendeleo na kifungu cha tisa ambacho ni cha mwisho kinazungumzia kukubaliwa kwa fedha zilizopitishwa kwa matumizi ya maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo mafupi ya mswada huu na baada ya kukushukuru tena wewe binafsi na Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza hili naomba sasa Waheshimiwa Wajumbe waupokee, waujadili na hatimaye kuupitisha rasmi mswada huu ili uwe sheria ya matumizi ya serikali kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

Mhe. Mwenyekiti: Hoja imeshatolewa na sasa hoja ijadiliwe, wanaokubali. Waheshimiwa Wajumbe hoja imeshatolewa inakaribishwa michango ya kujadili hoja hiyo, na mchangiaji wa kwanza tayari nimemuona Mhe. Hamza Hassan Juma akifuatiwa na Mhe. Ali Suleiman Shihata.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi hii kwa kuweza kuwa mchangiaji wa mwanzo wa huu mswada wa kuidhinisha matumizi ya fedha.

Mhe. Mwenyekiti, kawaida Mabunge yetu ya Jumuiya ya Madola baada ya kupitisha bajeti za wizara mbali mbali bado hawajaruhusiwa mawaziri kuweza kutumia fedha hizi, mpaka tutakapoweza kupitisha mswada huu wa fedha hapa ndio tunatoa ufunguo ili waheshimiwa mawaziri yale waliyotuahidi hapa Barazani kwa ajili ya kwenda kuyatekeleza. Kwa hiyo naomba Waheshimiwa Wajumbe na mswada huu si lazima ujadiliwe na wajumbe wengi, unaweza ukajadiliwa na wajumbe wawili au watatu ili kuweza kutoa ile baraka.

Mhe. Mwenyekiti, lakini nilikuwa tu nataka kutoa ushauri katika huu mswada wa fedha. Kwanza tunamshukuru Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote pamoja na yote yaliyotokezea lakini nia yetu kama alivyosema Mhe. Waziri katika mswada huu ilikuwa nia yetu ni kujenga. Tayari Mhe. Waziri baada ya muda mfupi tutamruhusu kuweza kufanya matumizi karibu ya shilingi bilioni mia nane na arobaini na moja, mia nne na sabiini na saba na laki tano ili serikali yetu iweze kufanya kazi.

Mhe. Mwenyekiti, kitu ambacho ninachokiomba Waheshimiwa Mawaziri, kila mmoja alileta hotuba yake ya bajeti na ameahidi mambo mengi sana. Kwa hiyo kitu ambacho nilichokuwa ninakiomba Waheshimiwa Mawaziri wakae kupitia zile hoja na ahadi walizozitoa Barazani, kwa sababu hoja zile zile ndio zitakazokuja kuulizwa katika kipindi kitakachokuja, na kwa kweli wakiweza kuzizingatia vizuri nadhani wataweza kupunguza maswali lakini vile vile kupunguza mabuti katika hicho kipindi kinachokuja.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine ambalo ninaloliomba hasa katika hizi fedha za miradi ya maendeleo. Kama nilivyosema Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri wa Fedha ninakuomba watendaji wako Wizara ya Fedha wao ndio wanaotoa fedha za miradi ya maendeleo katika taasisi nyengine mbali mbali. Naomba sana taasisi ziaminiane ili kuweza kupunguza misuguano lakini vile vile kuweza kuitia hasara kwa sababu ambazo zinakuwa si za msingi sana.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hiyo naomba sana kwa ile miradi ya maendeleo ambayo fedha zake inabidi uwepo mchango wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwanza namuomba sana Mhe. Waziri wa Fedha aangalie sana ili fedha hizi zikipatikana mapema ile miradi itaweza kutekelezwa mapema na tutaweza kutekeleza ndani ya bajeti hii hii.

Mhe. Mwenyekiti, kitu chengine ambacho nilichokuwa nataka kumshauri Mhe. Waziri, katika mswada huu wa fedha kwa sababu ndio tunaruhusu matumizi ya fedha. Niwaombe sana watendaji wetu, bajeti hii tumeipitisha katika mazingira ambayo ni magumu sana. Waheshimiwa wengi hawakupata nafasi ya kwenda

katika taasisi mbali mbali za wizara ambazo wamekabidhiwa na Mhe. Spika, ili kuja kuweza kushauri vizuri. Lakini katika hili nimpongeze sana Mhe. Makamo wa Pili wa Rais, jana amefanya kazi kubwa sana, yaani amefanya kazi ya kizalendo na kazi ambayo imeweza kuwezesha wajumbe leo kuweza kuipitisha bajeti hii bila ya pingamizi yoyote.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hiyo naomba sana kwa wale watendaji kwa hizi fedha ambazo tutakazoidhinisha basi wawe makini sana katika matumizi yake, kwa sababu tunategemea maendeleo makubwa katika hii miaka mitano ya Mhe. Dkt. Shein ya kumalizia nafasi yake ili kumkabidhi Rais mwengine anayetoka Chama cha Mapinduzi ikifika mwaka 2020.

Mhe. Mwenyekiti, ili nisichukue muda mwingi sana, nilikuwa tu nataka niwaambie Waheshimiwa Mawaziri, nyote sisi marafiki zetu, nyote nyinyi ni ndugu zetu, wala hatuna ubaya na nyinyi, na tunaahidi tutakupeni mashirikiano makubwa sana kwa kila ambalo pale tunapohisi na mengine Mhe. Mwenyekiti, hatutasubiri wakati wa bajeti kuja kupiga buti, kwa yale ambayo tunahisi yatekelezwe ndani ya kipindi cha katikati tutakuwa karibu sana, kitu ambacho ninachokiomba simu zenu na simu zetu ndio marafiki wa kuweza kufanya kazi hizi, ikiwa tunapiga simu mpaka zinadata hazipokewi kazi kubwa tutakayokuja kuifanya kuja kusokotana hapa kwenye Baraza, jambo ambalo sitegemei litakuwa ni zuri.

Mhe. Mwenyekiti, la mwisho kabisa kabisa kabla ya yote namkumbusha Mhe. Waziri wa Fedha, leo tumebakisha wiki moja, fedha za mfuko wa jimbo bado hazijaingia na tunakamilisha Baraza hili na wananchi wetu wana kiu ya maendeleo, naamini Mhe. Waziri wa Fedha hili atakwenda kukaa na watendaji wake kwa ajili ya kuweza kulitekeleza, tukikosea *step* hapa Mhe. Mwenyekiti, tunaweza pengine ikaja ikawa mambo sio mazuri. Sasa kuna suala ambalo nataka nimalizie ambapo Mhe. Waziri, kuhusu suala la deni la viinua mgongo pamoja na stahiki za walimu.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri, alilizungumza sana na alilizungumza vizuri, Waheshimiwa Mawaziri pale naona kidogo wanampa ushauri na wanacheka cheka lakini kitabu cha *CAG* tunacho katika ukaguzi wa hiyo miradi.

Mhe. Waziri, alisema kwamba wanashirikiana na Wizara ya Elimu katika kulipa baadhi ya yale madai ya walimu. Mimi kitu ambacho ninachokiomba Mhe. Mwenyekiti, bajeti ya Wizara ya Elimu tumeiona, kwa kweli walimu ni wengi na bajeti ya Wizara ya Elimu haitoshelezi hasa yale mahitaji yao.

Mhe. Mwenyekiti, kitu ambacho ninachokiomba kwa yale madeni ya nyuma Wizara ya Fedha tunaomba wayabebe wao ili waweze kuwalipa walimu wale. Kwa yale mengine ambayo itakuwa stahiki zao katika kipindi hichi ambacho tulichokuwa nacho basi tunaomba Waziri wa Elimu pamoja na watendaji wake waweze kuwalipa hayo mafao. Lakini tukisema mzigo ule wa kulipa madeni ya nyuma tumuwachie Waziri wa Elimu aweze kuyalipa kwa kweli hatoweza kutekeleza yale mambo waliyotuahidi, na kwa kweli changamoto ziko nyingi za Wizara ya Elimu tunahitaji kuja kukaa na kuangalia tutaweza kumsaidia vipi Mhe. Waziri wa Elimu ili watoto wetu wapate elimu bora.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pamoja na yote nakushukuru sana, namshukuru Mhe. Waziri wa Fedha kwa usikivu wake na ninaamini tutaweza kufanya kazi vizuri ili haya yote ambayo yalikuwa ni malalamiko na manung'uniko ya waheshimiwa katika kipindi kinachokuja yasiwe malalamiko tena, kwa sababu waswahili wanasema zile changamoto basi ndio chachu za maendeleo huko tunapokwenda.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo machache nakushukuru naunga mkono hoja, ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Hamza Hassan Juma. Mhe. Ali Suleiman Shihata na wa mwisho kabisa atakayechangia katika mswada huu ni Mhe. Simai Mohamed Said.

Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata): Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu na mimi kupata fursa ndogo ya kuichangia hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango juu ya uidhinishaji wa matumizi na mambo mbali mbali katika serikali yetu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nachukua fursa hii kumpongeza Mhe. Waziri, maana yake ninajua Mhe. Waziri, hayuko peke yake, ana Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Taasisi mbali mbali. Mimi nina mambo mawili matatu kwa uchache kabisa.

Ninasema kwamba kauli yangu kila siku husema kwamba unachokikusanya ndio utakachotumia. Namuomba Mhe. Waziri, awe mkali sana na watendaji wake kwenye kupata fedha hizo zikusanywe na zifanyiwe kazi juu ya mahitaji mbali mbali kwa nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, katika nchi tunajua tuna matatizo mengi kama wizara zilizokuja hapa zote kila mmoja kaeleza yake na anahitaji Wizara ya Fedha

ndio impe fedha hizo. Kwa hivyo niseme kinachopatikana kikusanywe na kiwafikie walengwa wananchi wetu katika maeneo yetu.

Mhe. Mwenyekiti, makusanyo ndio hayo ya pato la serikali lakini na udhibiti wa mapato yenyewe vile vile ni uhai wa matumizi mazuri katika utekelezaji wa kazi zetu. Namuomba sana Mhe. Waziri, hili aliangalie kwa upeo wa mbali kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, tunaamini kwamba wizara zetu zote zilizosimama hapa kila mmoja inaitegemea Wizara ya Fedha ipate fedha itekeleze malengo yake. Niwaombe sana watendaji wetu au niwaombe Waheshimiwa Mawaziri na wao wawape msaada Wizara ya Fedha kile kinachopatikana kitumike kwa walengwa waliokusudiwa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi baada ya hayo machache ninamuomba sana Mhe. Waziri na Watendaji wake wajitahidi kukusanya mapato kama nilivyotanguliza mwanzo ili kukidhi mahitaji katika nchi yetu. Ahsante naunga mkono hoja asilimia mia moja.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Ali Suleiman Shihata, sasa Mhe. Simai Mohamed Said.

Mhe. Simai Mohamed Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Waziri na kutoa mawazo yangu kidogo juu ya mswada huu ambao umeletwa mbele yetu hapa.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza sina budi nikiri kwamba nikiwa mimi Mwakilishi mpya na ni kipindi cha mwanzo ninaingia humu ndani, kwa kweli nimejifunza mengi sana. Lakini kuna maeneo ambayo ningependa Mhe. Waziri na Serikali kwa ujumla wayaangalie.

Suala moja ambalo wananchi kwa kweli wengi ambao sisi wanatuamini hapa Wajumbe wa Baraza pamoja na serikali wamejenga matumaini makubwa sana juu ya serikali yao hasa katika mpango mzima ambao Mhe. Rais alipokuja kuhutubia hili Baraza na kutoa dira yake na mawazo yake kuelekea mwaka 2015 kuelekea 2020.

Mhe. Mwenyekiti, katika huduma ambazo zimekuwa ni kelele na za muda mrefu ni yale yale masuala ya afya, elimu na maji. Mimi niiombe sana serikali kwa kupitia kwa watendaji pamoja, tuombe ifikapo katika mwaka huu na huko miaka ya mbele waweke azma masuala ya maji, masuala ya umeme kupeleka

vijijini, masuala moja kwa moja ya elimu, kuhakikisha kwamba hawa wananchi wetu wanaweza kuzipata hizi huduma bila ya tabu yoyote.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia tuna mpango mkubwa wa masuala yetu sasa kuanza kuangalia ya rasilimali zetu zilizokuwa ndani ya bahari na zilizokuwa juu ya bahari, naongelea masuala ya uvuvi wa bahari kuu pamoja na masuala ya mafuta na gesi. Tunajua sote tuko hapa na tuna semina nyingi tumejipanga, lakini na serikali nayo pia ijipange kwa ujumla mzima kuhakikisha kwamba wanaelimisha wananchi wake pamoja na wafanyakazi ndani ya serikali.

Mhe. Mwenyekiti, kweli serikali imeazimia kuhakikisha kwamba safari za nje itazuia, lakini pale ambapo inapotokea fursa vijana wetu hasa na wataalamu wetu kwenda kujifunza kazi ambazo sisi hatuna utaalamu nazo basi tuhakikishe wanakwenda nje, wanajifunza na wanakuja kutusaidia na suala zima kabisa katika masuala ya gesi na mafuta kuhakikisha kwamba yale yote ambayo ni faida zinazotokana nazo masuala ya gesi na mafuta zile faida zote zinabakia katika nchi yetu, katika visiwa vyetu na wananchi wetu wanafaidika.

Mhe. Mwenyekiti, lakini mwisho ningependa kutoa tahadhari yangu pia katika mambo yote ambayo serikali inataka kuyafanya kwa ajili ya maendeleo kwa wananchi wake.

Nataka niseme kwamba nchi nyingi zinapotaka kufanya mambo hukusudia kufanya mambo kwa ajili ya wananchi wake, naomba sana mambo ya ku-*expand without control*, kufanya mambo kutaka tugeuke tubadilike katika kuwekeza nchi yetu, kuna mambo mengi, kwanza ni kupima kuangalia hapa tulipo sasa hivi, wapi tunakwenda na wapi tunataka kufikia. Kwa hiyo naomba sana Tume ya Mipango ifanye kazi ya ziada, masuala tuliyonayo mara hii kama masuala ya bandarini kurundikana kwa makontena haya sio mambo ambayo yanawafurahisha wananchi wetu, wafanyabiashara wanapata tabu sana.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo kwa hayo maneno madogo niliyoyazungumza na kwa mchango wangu nakushukuru sana Mwenyekiti namtakia Mhe. Waziri na Serikali kwa ujumla kazi njema, na *in sha Allah* mwaka ujao na mabuti kidogo kidogo labda yataongezeka, ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Simai Mohamed Said na sasa namuomba Mhe. Waziri.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mheshimiwa mimi nilikuwa kabla hajatoa hii idhini yake kulikuwa na kifungu kidogo hapa katika Gazeti Rasmi la Serikali hii ambayo 49 kutokana na marekebisho ya mfuko wa jimbo nambari nne ya mwaka 2012, kifungu cha (e)

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mheshimiwa nakushukuru kwa kunipa nafasi. Naomba nimsaidie Mhe. Sarahan, kwenye hoja ambayo ameitoa.

Kikawaida tunapoleta mswada wa fedha, tunakuwa tunauleta peke yake, sasa safari hii kidogo kutokana na mambo yalivyokuwa mengi tumechanganya mswada huu pamoja na marekebisho ya sheria mbali mbali; sasa ndio maana Mhe. Sarahan amenyanyuka kutaka kuuliza kwenye mswada wa sheria ya matumizi mbali mbali.

Sasa naomba nimwambie tunachojadili sasa hivi ni kwenye ukurasa wa 56 ambao ni mswada wa matumizi ya serikali na sio ule mswada ambao anazungumza yeye. Ule tutakuja kuujadili kwenye kikao kijacho cha Baraza, sasa hoja zake zote aziweke tutakuja kujadili kwenye kikao kijacho cha Baraza, nakushukuru.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mwanasheria, Mhe. Waziri tuendelee.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa ufafanuzi kwenye maelezo yaliyotolewa na Mhe. Hamza, Mhe. Ali Suleiman Shihata na Mhe. Simai Mohamed Said.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nikubali kwamba tunapokea ushauri uliotolewa na Mhe. Hamza Hassan Juma na vile vile tunakubali suala la kuhakikisha kwamba michango ya SMZ kwa miradi ya maendeleo inapatikana mapema.

Hiyo hasa ndio dhamira yetu na ndivyo tunavyotaka iwe, lakini wakati mwengine hutokewa na matatizo kwa sababu mbali mbali ambazo huwa hazitegemewi wakati tunapopitisha bajeti yetu, lakini tutajitahidi sana kuhakikisha kwamba mapato yanakusanywa kwa ukamilifu wake na pale tutakapoimarika kimapato basi pia michango yetu ya serikali katika miradi ya maendeleo nayo itaimarika na kutolewa mapema zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusiana na suala la fedha za Mfuko wa Jimbo kwa mwaka 2015/2016 nalichukua na tutakwenda kulifanyia kazi, lakini kwa mujibu wa

sheria ile tunatakiwa majimbo yetu yawe yamerudisha *returns* kwa pesa zile zilizotolewa huko nyuma. Sheria iko wazi, kwa hivyo Waheshimiwa Wawakilishi wafuatilie kuona *returns* zao ziko sawa waziwasilishe Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa Katibu Mkuu kwa mujibu wa sheria inavyoelekeza, na pale fedha hizo zitakapopatikana basi moja kwa moja watapata fedha hizo. Kwa wale ambao majimbo yao yatakuwa yana matatizo basi sheria imeelekeza, kwamba hakutatolewa fedha nyengine mpaka *returns* za fedha zilizotoka nyuma ziwe zimetoka kwa usahihi wake.

Mhe. Mwenyekiti, suala la madeni na viinua mgongo bado niseme kwamba, hili tunalichukua na kama nilivyoahidi pale mwanzo tunalifanyia kazi kwa bidii kubwa sana.

Kipindi kifupi tu tayari tumeshatoa karibu shilingi bilioni tisa na zaidi na tutatoa shilingi bilioni tatu nyengine zitakuwa karibu shilingi 12.5 bilioni. Dhamira yetu kama nilivyosema mwanzo kuhakikisha kwamba tunamaliza madeni hayo na tunafanya juhudi kubwa sana kuona kwamba watu wetu wanapata mafao yao bila ya tatizo lolote.

Suala la bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuwa ni ndogo. Nakubali na kama ilivyo kwa wizara nyengine kama Wizara ya Afya nayo vile vile bajeti ndogo; lakini Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi nao watasema bajeti ndogo.

SADC Countries walipitisha azimio la bajeti, kwa mfano Wizara ya Kilimo iwe asilimia 10 ya bajeti yetu ya serikali. Haya tunayajua na yote ni vipaumbele, lakini tutaimarika zaidi na migao kwa sekta hizi muhimu pale tutakapoimarika kimapato, ukusanyaji wa mapato utakapoongezeka basi na hili nalo tutalifanyia kazi, ni wazo zuri.

Masuala ya madeni ya walimu. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali haina uwezo na sisi tuangalie uwezekano wa kuwasaidia. Nilisema hapa kwamba tutakaa na Waziri wa Elimu kuyaangalia madeni yote hayo, lakini niseme tu kwamba tuna mpango na dhamira ya kwamba kila mwezi tuwatilie fedha fulani Wizara ya Elimu kwa ajili ya ku-*offset* madeni ya nyuma ya walimu ili walimu wetu waweze kufanya kazi zao kwa vizuri. Kwa hivyo, hilo tutalifanyia kazi na tutakaa naye Waziri wa Elimu na watendaji wao, pamoja na Wizara ya Fedha na Mipango na watendaji wetu ili suala hili likamilike kwa haraka sana.

Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) amesema tuwe wakali kwenye mapato. Sawa tunachukua ushauri huo. Pia alizungumzia kwamba umuhimu wa Sekta ya

Uvuvi, Bahari Kuu na Mafuta, nalo tunalichukua. Lakini suala la safari za nje nirudie kusema kwamba safari za nje hazijasimamishwa wala hazijasitishwa, safari zipo lakini serikali inachosisitiza ni zile safari ambazo zitaleta tija. Kwa hiyo, safari bado zipo na hasa katika masuala haya ya mafuta na gesi ambayo tunaona ni masuala muhimu zaidi, basi safari hizi *In sha Allah* zitaendelea kuwepo na naamini hazitaondolewa baada ya kujenga. *(Makofi)*

Suala la Tume, ingawaje Tume yetu inafanya kazi vizuri sana lakini bado tunachukua ushauri wa kuzidisha bidii ili tume hii iweze kufanya kazi zake vizuri zaidi. Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe hoja imetolewa, sasa naomba kuwahoji wale wanaokubaliana na hoja hii, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba kutoa taarifa kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Kutunga Sheria ili kuupitia Mswada huu kifungu baada ya kifungu.

KAMATI YA KUTUNGA SHERIA

Mswada wa Sheria ya Makisio na Matumizi ya Mwaka 2016

Kifungu 1	Jina fupi
Kifungu 2	Tafsiri
Kifungu 3	Utoaji wa Shilingi 841,477,500,000
Kifungu 4	Makisio ya Fedha zilizokubalika
Kifungu 5	Uwezo wa Waziri Kukopa
Kifungu 6	Uwezo wa Waziri Kukopa
Kifungu 7	Marejesho ya Mkopo na Riba
Kifungu 8	Kukubaliwa kwa Mipango ya Maendeleo
Kifungu 9	Kukubaliwa kwa Fedha zilizopitishwa kwa Matumizi ya Maendeleo

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, ilivyokuwa Kamati ya Kutunga Sheria imeupitia Mswada wangu kifungu kwa kifungu na kuukubali bila ya marekebisho, sasa naliomba Baraza lako tukufu liukubali. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

Mhe. Mwenyekiti: Hoja imetolewa, naomba niwahoji wale wanaokubaliana na hoja hii wanyanyue mikono. Wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mswada wa Sheria ya Makisio na Matumizi ya Mwaka 2016

(Kusomwa kwa mara ya tatu)

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kuwa, Mswada wa Sheria ya Makisio na Matumizi ya Mwaka 2016 usomwe kwa mara ya tatu. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa nawaomba radhi, kwa hiyo naomba kuwahoji, wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono. Wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Mswada wa Sheria ya Serikali ulisomwa mara ya tatu na kupitishwa)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe nawashukuru sana wale wote waliochangia na pia nimpongeze Mhe. Waziri na nimtakie kila la kheri katika ufanyaji wake wa kazi.

(Saa 9:15 mchana Baraza liliahirishwa hadi
tarehe 28/06/2016 saa 3:00 asubuhi)